

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tano – Tarehe 8 Novemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wetu wa Tano, leo ni Kikao cha Tano. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Moja kwa moja tunaanza na maswali na leo tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali litaulizwa na Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum. Dkt. Thea tafadhalii.

Nimekuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 49

Kuongeza ajira kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu

MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. DKT. THEA M. NTARA
aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ajira kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu hasa katika sekta ya kilimo kwa kuwa mikopo ya elimu ya juu imewezesha wanafunzi wengi kuhitimu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ajira kwa wahitimu wa Vyuo Vikuu zinaongezeka hususan katika sekta ya kilimo, Serikali imetekeleza mipango ifuatayo: -

(i) Kutoa mafunzo ya kilimo cha kisasa kuitia programu ya kukuza ujuzi nchini, ambapo jumla ya vijana 12,580 katika Mikoa 17 nchini, wakiwemo wahitimu wa fani ya kilimo wamepatiwa mafunzo ya kilimo cha kisasa na sasa wapo tayari kuanza biashara ya kilimo na kutumia teknolojia na ujuzi wa kitalunyumba.

(ii) Kuwezesha wahitimu kupata uzoefu wa kazi nje ya nchi (*internship*), ambapo Serikali kwa kushirikiana na Ushirika wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (*SUGECO*), wamewezaresha wahitimu 703 kwenda nchini Israeli na Marekani. Kati ya hao, wahitimu 311 wamerudi nchini na wamejiajiri katika maeneo mbalimbali nchini.

(iii) Kupitia Benki ya *TADB* na mikopo ya Halmashauri, baadhi ya wahitimu waliopatiwa mafunzo nje ya nchi wamepatiwa mikopo ya jumla ya Shillingi Milioni 170 na wanaendelea na shughuli hizo.

(iv) Kupitia Vituo vya Uatamizi kwa wahitimu (*Incubator Centres*) katika Mikoa ya Morogoro na Pwani,

wahitimu 1,000 wamepatiwa mafunzo ya uanzishaji shughuli za kilimo na ujasiriamali na;

(v) Kupitia kilimo cha vizimba (*block farming*), wahitimu 39 wamepatiwa fursa ya kuanzisha shughuli za kilimo. Kati ya hao, wahitimu 30 wamepatiwa fursa ya kushiriki katika shamba la hekari 1,500 lilitopo Mkoani Morogoro Mvomero. Aidha, wahitimu Tisa wamepatiwa fursa ya kushiriki katika shamba la kahawa Mkoani Songwe.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha wahitimu wengi zaidi wanaendelea kuwezeshwa kuajirika lakini pia kujajiri, kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa, Serikali imetenga zaidi ya Shilingi bilioni 54 ili kuwawezesha wahitimu 1,500 kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi ikiwemo fani ya kilimo. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Patrobass Katambi. Mheshimiwa Ester Bulaya muuliza swalii.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, nipo.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya. Kama kuna mtu amewasha *microphone* huko hebu aizime.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, nipo.

SPIKA: Upo Mheshimiwa upo, kaa kwanza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Utakubaliana na mimi kwamba tatizo la ajira kwa vijana kwa nchi hii limekuwa kubwa na la muda mrefu na Serikali *ilishaji-commit*, wakati nikiwa Mbunge wa Vijana kipindi kile wakati tunapitisha hapa Sheria ya Baraza la Vijana. Kwamba, kila Hal mashauri itatenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya vijana hasa ambao ni *graduate* waweze kwenda kujajiri wenyewe. Lakini ardhi yenye rutuba ya daraja la kwanza, daraja la pili wamekuwa wakipewa wawekezaji. Hii ardhi ambayo vijana wanaitumia unakuta wamepewa na Mjomba, Shangazi na Bibi.

Je, lini Serikali mtatimiza ahadi ambayo mmeweka kutenga ardhi kwa vijana na kuwawezesha ili asilimia kubwa ya vijana waweze kujiajiri wenyewe? (*Makof*)

Swali la pili; Serikali tulishatunga Sheria ya Baraza la Vijana na Vijana wanakosa chombo chao cha kujadili Kitaifa bila kujali itikadi zetu na Rais alishasaini. Je, ni nini kigugumizi cha kushindwa kutenga bajeti ya uanzishaji wa Baraza la Vijana kuanzia Taifa mpaka Kata? Tunahitaji *commitment* ya Serikali hatutaki ahadi. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Patrobass Katambi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. PASCAL P. KATAMBI): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali kwa agizo hilo la Serikali lilitolewa kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tayari imekwisha kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za vijana katika Halmashauri 84 zimekwisha tenga maeneo kwa ajili ya shughuli hiyo na eneo ambalo ni la mfano katika uzinduzi wa programu hii ya kutengewa maeneo kama agizo la kwenye Halmashauri nchini, lilitanyika hivi karibuni pale Kahama – Zongomela, kuna eneo kubwa ambalo vijana wanafanya shughuli mbalimbali pale zikiwemo pia za kilimo lakini pia biashara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anauliza ni lini Serikali sasa itaenda katika kukamilisha mchakato wa kupata Baraza la Vijana ikiwa sheria tayari. Tayari eneo hili ni agizo la Mheshimiwa Rais ambaye alizungumza alipokutana na vijana pale Mwanza, alitoa maelekezo na maelekezo hayo yanafanyiwa kazi na kwa kipindi chote tayari tumekwishaanza na mabadiliko kwa sasa. Tumeshafanya mabadiliko ya sera ya vijana ya mwaka 2007 na hatua ya pili itakuwa kwenda katika kuangalia uhitaji wa sasa katika sheria kama italazimika kuweza kufanya mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, hatua ya tatu itakuwa sasa kuangalia kulingana na mazingira yaliyopo kama kutakuwa na ulazima kwa wakati wa sasa kuendana na *situation* iliyopo katika mahitaji ya vyombo vingi pia vya Kimataifa kama tutaweza tukaandaa Baraza la Vijana kwa kipindi hiki, lakini tayari michakato hii tayari tumekwisha kuianza kwa upande wa Serikali. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Thea nimekuona. Siku nyinyine uwe unawahi Mheshimiwa.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana nisamehe kwa hili. Mimi nilikuwa naomba niulize kwenye hizi takwimu. Nimezisoma hizi takwimu ukiangalia hii wanaita sijui *block farming* pamoja na *incubation centers* nimeona ziko Mkoa wa Pwani na Morogoro. Je, hamuwezi mkatoa jedwali linaloonesha mmesaldia vijana Mikoa gani na vijana wangapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mimi nimeuliza ajira. Hata ukiangalia haya majibu nimeuliza ajira wananilettea ujasiriamali mimi nataka ajira rasmi kwa vijana. Ni lini watajipanga kwa hilo? Ahsante. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Ujasiriamali siyo ajira?

SPIKA: Ndiyo ukweli wenyewe sasa sijui tunafanyaje yaani? Na mimi niliona tangu mwanzo nadhani hili likajibiwe upya hili swali ndiyo ukweli yaani. Kwa sababu, swali lake linasema je, Serikali ina mpango gani kwanza wa kuongeza ajira? Kwa hiyo, kinachotakiwa hapa ni mpango lakini wao wametumia muda mwingi sana kueleza tulifanya hivi, yaani mambo ambayo yalipita. Kumbe huyu anataka mpango wa jinsi tunavyokwenda mbele katika kushughulikia jambo la ajira na pia tumejishughulisha zaidi na ujasiriamali na kadhalika.

Hebu tutalipangia Mkutano ujao wa Bunge ili likae vizuri kwa sababu ya *sensitivity* yake ni ajira kwa vijana. Ahsante sana. (*Makof/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunahamia TAMISEMI Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 50

Hitaji la Zahanati Kata ya Ng'ambo - Tabora Mjini

MHE. JACQUELINE K. ANDREA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Zahanati katika Kata ya Ng'ambo ili yopo Tabora Mjini?

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge mtaona Kanuni zetu, nadhani sijui Kanuni ya 49 hii, inasema wakati swali linalohusika litakapofikiwa katika orodha ya shughuli, Spika atamuita Mbunge mwenye swali hilo au kama hayupo, Spika atamuita Mbunge mwingine ye yote aulize swali hilo kwa niaba ya Mbunge mwenye swali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nikikuita una swali ni pale pale unasi mama ili uulize swali lako, Ukizubaa sekunde nne, tano ye yote atakayesi mama mimi nitampa aulize swali lile hata kama upo humu ndani.

Kwa hiyo, wengine wanazungumza hawafuatilii utajikuta swali lako linaulizwa na mtu mwingine au inatakiwa uwahi utaratibu ndiyo huo. (*Makofi*)

Pia kwa upande wa Vyama huwa ni muhimu ku wahidi pia, kama ni Mbunge wa CCM ameuliza swali lakini hayupo, Mbunge mwingine ye yote wa CCM ku wahidi kusimama au wa Upinzani Mbunge mwingine ye yote wa Upinzani ku wahidi kusimama. Nikiona hakuna mtu ali yesi mama ni wa upande mwingine basi anapewa huyo huyo wa upande mwingine, maana yake Kiti kinakuwa hakina *option*, maana Bunge zima kasimama mtu mmoja tu sasa utamuachaje? Kwa hiyo tuende hivyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na majibu ya swali la Mheshimiwa Jacqueline Kainja, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI Mheshimiwa David Silinde, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Andrea Kainja Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati kwa fedha kutoka Serikali kuu na fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetoea fedha shilingi billioni 27.75, kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati 555. Ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilipokeea fedha ya shilingi milioni 150, kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati ya Ituru, Igosha na Igombe.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga fedha shilingi bilioni 35.15, kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 758 nchi nzima. Ambapo Halmashauri ya Manispaa Tabora imetengewa shilingi milioni 100 kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya Zahanati ya Zaire na Zahanati ya Kapunze kila moja shilingi milioni 50. Aidha, kupitia mapato ya ndani Manispaa ya Tabora imetenga fedha shilingi milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha zahanati ya Mtendeni na Zahanati ya Igambilo, kila moja kwa shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyojengwa na wananchi kote nchini. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora inashauriwa kutenga fedha kutoka katika mapato ya ndani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa zahanati katika Kata ya Ng'ambo ili kusogeza huduma kwa wananchi.

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Bado sijakuita.

Sasa nakuruhusu imetuchukua muda kwa sababu, yaani asilimia 99 ya jibu halikuwa lenyewe. Alikuwa anapiga piga tu, sasa nilikuwa natafuta kama tuendelee nalo au nao wakaliandike upya.

Naendelea kusitiza Waheshimiwa kuhusu Wasaidizi wetu kuandika majibu halisi ya maswali yaliyoulizwa. Majibu ni mazuri lakini yanaeleza vitu ambavyo havikuulizwa. Wameelezea zahanati na nini ambazo zimejengwa ambazo siyo, swali linauliza kuhusu Kata ya Ng'ambo basi. Tuendelee Jacqueline. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. JACQUELINE K. ANDREA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba na wewe umeweza kuona hili swalii halijajibiwa na mimi nimegundua hivyo, lakini nimpongeze Waziri kwa majibu mazuri yanayoonyesha namna gani Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan imeendelea kupanga bajeti kuendelea kuhakikisha maboma ambayo yanatakiwa kukamilishwa yakamilike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu nipatiwe majibu mazuri, ambayo yanaendana na swalii langu ili niweze kuridhika sasa kwamba ni lini Serikali inaweza ikaona kuna mpango mzuri kwenye hizi Kata ambazo ni kubwa hazina zahanati ili wananchi hawa waweze kupata zahanati na siyo kwamba kuna maboma hakuna hata hayo maboma ambayo yanatakiwa kukamilishwa yaani ni ujenzi mpya, Serikali ina mpango gani na njia ipi madhubuti kuhakikisha kwamba Kata ambazo ni kubwa mfano, Kata hii ya Ng'ambo ambayo iko Tabora Mjini na zingine nyingi ambazo sijaziainisha zinaweza kupata ufumbuzi huo? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri David Silinde, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sasa Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwanza tunamaliza ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Tarafa zote nchini. Tangu uhuru tulikuwa tuna Tarafa 570 na tulikuwa na Tarafa 363 tu pekee ambazo zilikuwa na Vituo vya Afya na katika Awamu ya sasa hivi tulikuwa na Vituo vya Afya kama 207 ambavyo Serikali tayari imeshapeleka fedha kwa awamu mbili ambazo nafikiri kila Mbunge anazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukija kwenye *level* ya zahanati kwa kila Kijiji lengo la Serikali ambalo tumeliweka na ndiyo maana nimejaribu kuelezea hapa fedha ambazo tumezitenga ni kwa ajili ya kwenda kumalizia zahanati ambazo zimeanzishwa na nguvu za wananchi na nyingine zimeanzishwa na mapato ya ndani ya Halmashauri na ndiyo maana kwenye swalii hili la msingi lilipokuwa linaulizwa, tumemshauri Mbunge wa Jimbo na Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Tabora kwamba, hamasisheni wananchi mkishirikiana na vyanzo vya ndani muanze ujenzi ili sisi kutoka Serikali Kuu tulete fedha kwa ajili ya kumalizia hiyo zahanati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukisema kwamba tutajenga zahanati vijiji 12,000 kwa wakati mmoja kwa sasa hivi hatuwezi kudanganya kwenye hilo, ukweli wetu ni kwamba tunamaliza Vituo vya Afya Tarafa zote, tunamaliza Hospitali katika Halmashauri zote halifu kwenye ngazi ya vijiji tutapeleka fedha, kwenye vijiji vyote ambavyo zahanati wananchi wamepeleka nguvu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hilo ndiyo jibu letu, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana nakushukuru. Jibu hilo ndio ambalo sasa lingeandikwa. Mbunge hamasisheni watu wenu, anzeni na sisi tutakuja inakuwa *perfect* haina shida. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli ninyi Wanyamwezi sasa hata zahanati na hii Kata kubwa mnayosema iko Tabora Mjini Manispaa, Mnispaa nzima hamuwezi kujenga zahanati? Wakati Kongwa tunajenga Zahanati sisi masikini kabisa wakati ninyi ni Toronto nzima haiwezi kujenga zahanati? (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kidogo. Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk Mbunge wa Tumbe.

Na. 51

Kuhamasisha Utunzaji wa Mazingira Bahari ya Hindi

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vikundi vyatyananchi ili kuhamasisha uhifadhi wa mazingira hasa katika fukwe za Bahari ya Hindi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari ina mpango wa kushirikisha wananchi kuititia Ofisi ya Makamu wa Rais. Pia Serikali imeandaa mkakati wa kuhifadhi mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Aidha, kufuatia utekelezaji wa mkakati huu na kwa kutambua umuhimu wa ushirikishwaji wa jamii katika kuhifadhi mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani, Serikali kuititia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanzisha vikundi vyta usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi vinavyofahamika kwa jina la "Beach Management Units" – BMUs. Vikundi hivi vimeanzishwa katika ngazi ya Kijiji/Mtaa kwa mujibu wa Kifungu cha 18 cha Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003. Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi una jumla ya vikundi 157 ambapo Tanga ina vikundi (31), Pwani (46), Dar es Salaam (23), Lindi (46) na Mtwara (11). Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Hili jibu *perfect*. Mheshimiwa muuliza swali, Mbunge wa Tumbe.

MHE. AMOUR K. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza sijajua kwa nini mikoa ya Zanzibar haijaorodheshwa hapa, lakini pia sijajua Serikali inawezeshaje makundi haya 157 ili kumudu kazi hii ngumu sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Kwa kuwa zipo dini ambazo zinajinasibu na kujitahidi kusema kwamba kila kitu kitakachotokea duniani kwenye vitabu vyao wameeleza: Je, Serikali imeshaona umuhimu wa kuwashauri viongozi wa dini katika kuondoa tatizo hilo ambalo ni gumu sana hata pale Zanzibar ambapo visiwa ndiyo vinaondoka?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khamis Amour Mbarouk kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Amour kwa juhud yake ya kufuatilia masuala ya mazingira kule visiwani Zanzibar. Suala lake la kwanza ni kweli kwamba ipo haja ya kuhamasisha vikundi mbalimbali katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na tayari tumewasiliana na wenzetu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kule Zanzibar kwa ajli ya kuhamasisha wananchi wa Kanda za Pwani ili kusudi kuanzisha vikundi kama hivi kwa lengo la kutunza mazingira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kwa kweli tunachukua hoja yake hii kwamba upo umuhimu wa kushirikisha taasisi za dini. Tumeanza kuwaita viongozi wa dini na kuzungumza nao kuhusu suala la utunzaji wa mazingira. Kwa mwelekeo ambao tunakwenda nao sasa, ni lazima tuzishirikishe taasisi za dini kuhusu suala la utunzaji wa mazingira, kwa sababu wao kwa asilimia kubwa wanaka na wananchi. Kwa hiyo, tutawaomba viongozi wa Makanisa ama Misikiti iwe ni sehemu ya mahubiri yao ya utunzaji wa mazingira ili mazingira yetu yawe salama kwa maslahi ya Taifa letu. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, uliza swali la nyongeza.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Huko nje hasa katika ukanda wa bahari, sisi tunatokea kwenye visiwa, hali ni mbaya sana kuhusu masuala mazima ya mazingira. Wakisema kwamba waanzishe vikundi, kwamba vikundi ndiyo viwe vinasimamia mazingira katika kukusanya taka, bado elimu haijafikiwa. Yaani wananchi walio wengi wanazalisha taka, lakini hawana taaluma ya utunzaji wa hizo taka hasa kwenye upande wa mazingira. Je, nini kauli ya Serikali juu ya

usimamizi wa masuala mazima ya utoaji wa elimu ya usimamizi wa mazingira? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asya, ni kweli kabisa anachokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba elimu bado ni ndogo, lakini tumieandaa programu maalumu za kutoa taaluma kwa wanavikundi na wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, jibu langu la pili la nyongeza nilisema kwamba tutaenda mpaka kwa taasisi za dini ili suala la taaluma liwe na wigo mpana. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba taaluma hiyo ya utunzaji wa mazingira itafika nchini kote.

SPIKA: Tunashukuru sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi.

Na. 52

Ujenzi wa Barabara ya Mwembe – Mbaga – Mamba Myamba

MHE. DKT. DAVID M. DAVID aliuliza:-

Barabara ya Mlimani kutoka Mwembe – Mbaga hadi Mamba - Myamba ni kero kubwa kwa wakazi zaidi ya 150,000 katika Majimbo ya manne; Same Magharibi na Same Mashariki ambapo zaidi ya 70% ya wakazi wake wanaishi milimani.

Je, ni lini barabara hiyo yenye urefu wa Km 120 itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami nyepesi (*Surface dressing*) ili kufanikisha shughuli za maendeleo katika Wilaya ya Same?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Mlenge, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mwembe – Myamba hadi Ndungu ni barabara ya changarawe yenye urefu wa kilometra 90.19. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 1,848.97 kwa ajili ya kuifanya matengenezo mbalimbali barabara hiyo. Vilevile, ujenzi wa Daraja la Yongoma liliokatika wakati wa msimu wa mvua umekamilika kwa gharama ya shilingi milioni 453. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Mathayo David, nimekuona mwuliza swali.

MHE. DKT. DAVID M. DAVID: Mheshimiwa Spika, nashukuru majibu ya Mheshimiwa Waziri kidogo yanaleta matumaini kwa mbali, lakini kwa kuwa hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne japo haijawahi kuwekwa

kwenye llani ya Uchaguzi; lakini kwa kuwa *TANROADS* kila mwaka inapoteza mabilioni ya fedha, kwa mfano mwaka huu barabara hii imetengewa shilingi bilioni mbili, lakini vifusi vipowekwa baada ya mvua kunyesha usiku mmoja tu, kifusi hiki kinazolewa na maji ya mvua na wananchi wa milimani ambapo ni asilimia zaidi ya 65 ya wakaazi wa Wilaya ya Same wanakosa mawasiliano na pia Serikali inaingia hasara:-

Je, upembuzi yakinifu wa barabara hii utafanyika lini ili Serikali isipoteze mapato lakini wananchi wa Mwembe, Mbaga, Bonja mpaka Mamba waweze kupata mawasiliano pale mvua zinaponyesha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Tunafahamu kwamba Sera ya Serikali ni kuunganisha mikoa kwa mikoa na Wilaya kwa Wilaya; vile vile nchi hii na Wilaya hizi za nchi hii kuna tofauti ya mazingira, kwa mfano Wilaya ya Same kuna malima mingi sana, Lushoto kuna milima mingi; Mbinga kuna milima; Kagera na maeneo ya Arusha kuna milima mingi sana: Sasa kwa nini Serikali isichukue ikafanya upembuzi yakinifu wa barabara zote za milimani kusudi wananchi wa milimani waweze kupata usafiri wakati mvua zinanyesha? (*Makofi*)

SPIKA: Kwa makofi hayo, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwenye maeneo ya miinuko vifusi huwa vinasombwa na maji. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna barabara za lami na za changarawe na za udongo. Azma ya Serikali ni kuwa na barabara zote za lami, lakini uwezo huo bado hatujakuwa nao na kwa hiyo Serikali inatengeneza barabara

kwa kiwango cha lami, kila mwaka tunatenga fedha ili barabara hizo ziweze kutumika.

Mheshimiwa Spika, bajeti aliyoisema ya bilioni mbili siyo tu kuweka kifusi, ni pamoja na kutengeneza mifereji, madaraja pamoja na makalavati ili barabara hiyo iweze kutumika kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema, tunatafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na hatimae usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, pengine nitoe maagizo kwa Meneja wa *TANROADSM* koa wa Kilimanjaro aweze kuainisha yale maeneo yote korofi na yenyé miinuko mikali ili tuweze kufanya matengenezo *surface dressing* ama hata kujenga barabara hizo kwa zege kama ilivyofanyika maeneo mengine kama Mikoa ya Manyara, Ruvuma, Kigoma, ukienda Morogoro; maeneo ambayo ni korofi basi barabara zinajengwa kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mikoa, ni kwamba kama tulivyoainisha kwamba tunaunganisha mikoa na mikoa kwa kiwango cha lami, hiyo ndiyo sera ambayo tunayo, lakini wazo la maeneo kwenye miinuko, basi tulichukue na tukiona kama fedha itatosha, basi Serikali itafanya hivyo. Azma ni kuhakikisha kwamba barabara zote zinajengwa kwa kiwango cha lami bila ya kujali eneo eneo na eneo. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Tulibakize swali hili huko huko Same. Tumetoka Magharibi sasa twende Same Mashariki, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kupata nafasi. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kutumia pesa nyingi sana kujenga Daraja la Yangoma ambalo lilikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi waliopo kwenye barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulingana na ubora wa Daraja la Yongoma lililojengwa ambalo Naibu Waziri, Mheshimiwa Waitara, alikuja tukaenda kuliona. Kweli Serikali hamwoni kuna umuhimu wa kujenga ile barabara iwe na hadhi sawa na lile daraja lililowekwa pale? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa kupongeza kazi nzuri ambayo imefanyika ya kujenga lile daraja. Pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kujenga daraja hilo maana yake ni maandalizi ya kuja kujenga pia barabara nzuri inayofanana na hilo kwa sababu hatutajenga tena.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kwenye jibu letu la msingi tumesema tunatafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili sasa hiyo barabara iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Hiyo hatua hatuwezi kuiruka, ni lazima tuifanye na ndiyo maana tunatafuta hiyo fedha. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Ushauri wa kitinii ni kwamba mtafute muda uende na Mheshimiwa Mathayo David, hebu mpitepite huko millimani ukuone kulivyo. Maana ni mazingira maalum sana, yanataka ufileke mara kwa maa ili uipate picha halisi.

Waheshimiwa nawaona, lakini kwa sababu ya muda naomba tuendeleee, bado tupo Wizara hii hii. Swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, uliza swali lako.

Na. 53

Kuweka Vivutio Maalum Bandari ya Mtwara

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Je, Serikali imeweka vivutio gani maalum ili kuwavutia wasafirishaji kutumia Bandari ya Mtwara kusafirisha mizigo ya nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Waitara, tafadhali.

NAIBU WIZIRA YA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika hatua za awali za kuvutia wasafirishaji kutumia Bandari ya Mtwara, Serikali imepunguza asilimia 30 ya gharama za tozo za bandari kwa shehena ya Korosho. Gharama hizo zinahusisha kupanga na kupokea shehena kwenda au kutoka melini, usafiri wa kati wa kusafirisha bidhaa kutoka melini hadi kwenye eneo la kuhifadhi mizigo na kinyume chake; kupokea na kupeleka mizigo kutoka kwenye mabehewa au malori kwenda melini; na upakuaji na uhifadhi wa mizigo kutoka kwenye meli.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imetoea punguzo la ada inayotozwa kwa matumizi ya gati kushusha mizigo ndani ya meli (*wharfage*) kutoka dola ya Kimarekani hadi nusu Dola na kurefusha muda wa makasha ya kupakia Korosho kuwa bure katika msimu wote wa korosho.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Serikali kuititia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*) imeendelea kutoa punguzo la tozo maalum kwa wasafirishaji wa makaa ya mawe na saruji ili kuifanya Bandari ya Mtwara kufanya kazi

katika kipindi chote cha mwaka. Serikali itaendelea kufanya tathmini na kuchukua hatua stahiki kwa lengo la kuvutia matumizi ya Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wasafirishaji kutumia punguzo hili la tozo liliolofanywa na Serikali kusafirisha mizigo ya nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia kupitia Bandari ya Mtwara. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Chikota, nimekuona. Maswali ya nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Ili Bandari ya Mtwara iweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuweza kushughulikia mzigoo mkubwa inategemea ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi Mbambabay.

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu radi huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, baada ya upanuzi mkubwa wa Bandari ya Mtwara, bandari hii sasa inakabiliwa na changamoto ya vitendea kazi vya kisasa:

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vitendea kazi vya kisasa katika Bandari yetu ya Mtwara?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI YA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Chikota kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mpango wa Serikali kujenga reli ya kutoka Mtwara kwenda Mbambabay; huu mpango ndiyo unaosimamiwa na watu wa TPA wanaufanyia kazi. Tunajua

umuhimu wa eneo hilo, Mheshimiwa Mbunge atupe muda, hili jambo tukalifanyia kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili anataka kujuua kama kuna mpango wa kununua vitendea kazi. Mpango mkakati sasa wa *TPA* wa kuweza kuboresha bandari zetu na hasa eneo la Mtwara, ni mpango ambaao upo katika mpango kabambe wa awamu ya pili na fedha zinaendelea kutafutwa na tumeshawaelekeza watu wa *TPA* waje na mpango mkakati wa maandishi twende kuboresha maeneo haya na bandari zote muhimu kimkakati kutookana na kupatikana fedha.

Mheshimiwa Mbunge tunaendeleza ushirikiano, jambo hili limepokelewa na Serikali na Kamati ya Bunge ya Bajeti imetoa maelekezo, vile vile na Kamati ya Miundombinu na tumelipa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano ya Technolojia ya Habari, swalii la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe. Mheshimiwa Mkundi.

Na. 55

Hitaji la Mawasiliano ya Simu – Ukerewe

MHE. JOSEPH M. MKUNDI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la mawasiliano ya simu katika maeneo ya Bukiko, Chabilungo, Kitale na maeneo mengine yenye tatizo hilo Visiwani Ukerewe?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri Mhandisi Andrea Kundo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, eneo la Bukiko lina mnara wa Halotel ulijengwa kwa ruzuku ya Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*). Eneo la Chabilungo linapata huduma za mawasiliano kupitia watoa huduma ambaa ni Tigo, Shirika la Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) pamoja na *Vodacom*.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) itafanya tathmini kwa mara nyingine katika maeneo ya Chabilungo, Bukiko, Kitale na maeneo mengine katika Jimbo la Ukerewe ili kubaini mahitaji halisi ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo, Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mkundi, swalii la nyongeza, nimekuona.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwanza kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini eneo la Bukiko ni kweli kupitia *UCSAF*, ulijengwa mnara wa Halotel lakini kuna shida kubwa; ule mnara unategemea umeme juu, kiasi kwamba nguvu ya umeme inapopungua kunakuwa hakuna mawasiliano, lakini vile vile kuna shida kubwa ya *Internet* kwa sababu mtandao ulioko pale ni wa 2G; Sasa naionomba Serikali niweze kujua, ni lini sasa Serikali itapeleka jenereta kwenye eneo lile? Vile vile iwasiliane na watu Halotel ili kuweka mtandao wa zaidi ya 2G kwa maana ya 3G na vyovyote itakavyowezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema kwenye majibu, ni kweli kuna shida kubwa ya mawasiliano kwenye maeneo mengi, kwenye visiwa vya Ukerewe; na Serikali imejibu kwamba itaenda kupitia maeneo yote yenye shida: Ni lini sasa kazi hii itafanywa

na Serikali ili timu iende kule, ifanye uchunguzi na hatimaye marekebisho yafanyike ili kuwe na mawasiliano mazuri kwenye eneo lile? Nashukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Habari, Mheshimiwa Kundo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu jenereta; kwanza kabisa ile *site* ya mawasiliano iwe imekamilika, hajjalishi kama ni umeme wa *TANESCO* au ni wa *Solar*, ni lazima *site* iwe na *backup generator*. Kwa vile Mheshimiwa Mbunge amelifikisha hili, basi Serikali inalipokea na tutalfanya kazi ili kujiridhisha na changamoto ambayo ameiongea.

Mheshimiwa Spika, vilevile ni azma ya Serikali sasa kuhakikisha kwamba, maeneo mengi nchini yanapata huduma ya *internet*, yaani kutoka katika huduma ya zamani ya *2G* kwenda *3G*. Hapo kabla Wizara tayari ilishatoa maelekezo kwa watoa huduma ili kuhakikisha kwamba, minara inayojengwa kuanzia sasa basi iwe na huduma ya *3G*.

Mheshimiwa Spika, tuna minara ya aina mbili; minara ambayo inatokana na ruzuku ya Serikali, lakini vilevile kuna minara ambayo inatokana na wawekezaji wenyewe. Ile ambayo inatokana na ruzuku ya Serikali tayari Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umeshaanzisha mchakato wa *ku-up grade* minara yote ambayo itakuwa ina *2G* kwenda kwenye *3G*. Pia Serikali imeelekeza kwa watoa huduma wengine katika minara ambayo sio ya Serikali, ihakikishe kwamba, inaona umuhimu sasa wa kuelewa kwamba, sasa teknolojia ya *3G* inahitajika kwa Watanzania wote. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Kule Msekwa nimekuona Mheshimiwa Mwambe, uliza swali lako.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hivi karibuni na katika Jimbo lote la Ndanda kuna matatizo sana ya *network* na hasa eneo la Ndanda ambako ndio Makao Makuu ya Jimbo na mtandao tunaotumia pale sana ni *Vodacom* pamoja na *Airtel* na *Airtel* kuna hisa za Serikali. Hata hivyo, wataalam walipopewa taarifa mpaka leo hawajaenda kufanya marekebisho. Sasa kwa nini Mheshimiwa Waziri asiwakumbushe watu wa *Airtel* kwenda kuufanya marekebisho mnara ule ili mawasiliano yawe bora?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Teknolojia ya Habari.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi ameomba Serikali tuongee na watu wa *Airtel* ili wakarekebishe changamoto iliyojitokeza. Tunaipokea changamoto hiyo na tutawasiliana na wenzetu wa *Airtel* ili kwenda kuifanya kazi hiyo changamoto. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tunahamia Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mhandisi.

Na. 54

Usafirishaji wa Viumbe Hai Kwenda Nje ya Nchi

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaruhusu usafirishaji wa Viumbe Hai nje ya nchi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa *EngineerMwanaisha Ng'anzi Ulenge*, Mbunge wa Viti Malum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Machi, 2016 Serikali ilisitisha biashara ya kusafirisha wanyamapori hai nje ya nchi. Tatizo kubwa lililosababisha maamuzi hayo lilikuwa ni matokeo hasi yaliyokuwa yakiendelea kujitokeza kutokana na kufanya biashara hiyo ikiwemo kuhamisha rasilimali ya wanyamapori nje ya nchi. Aidha, Serikali ilirejesha jumla ya shilingi 173.2 ya ada na tozo zilizolipwa awali na wafanyabiashara kabla ya kusitishwa kwa biashara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya kina kuhusu biashara ya usafirishaji wa wanyamapori hai nje ya nchi. Kufuatia tathmini hiyo, zuio la biashara litaondolewa ambapo biashara hiyo itafanyika kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Wanyamapori hai wataruhusiwa kusafirishwa kwa shughuli za utafiti na kidiplomasia tu.

(ii) Wanyamapori watakaosafirishwa nje ya nchi watakuwa ni wale waliokaushwa au mazao yatokanayo na wanyamapori hao.

(iii) Biashara ya wanyamapori waliokaushwa pamoja na mazao yake itafanywa na wafanyabiashara wenye miradi ya ufugaji wanyamapori ili kuhamasisha uanzishwaji wa miradi ya ufugaji wa wanyamapori.

(iv) Serikali itatoa muda wa miezi mitatu ili kuruhusu wafanyabiashara kusafirisha wanyamapori waliosalia kwenye mazizi na mashamba kabla ya zuio ambao walikuwa wanafugwa kwa lengo la kuwasafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Swali la nyongeza, Mheshimiwa *Engineer* Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, mionganoni mwa viumbi hai waliozuliliwa ni pamoja na vipepeo ambao sio maliasili, vipepeo wanaozalishwa na watu binafsi Wilayani Muheza, Mkoani Tanga. Je, Serikali iko tayari kutoa tamko rasmi kwamba, masharti waliyoyatoa yatawahusu viumbi hai ambao ni maliasili na vimbe hai wanaozalishwa na watu binafsi hayawahusu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mto Zigi, Mkoani Tanga, una mamba wengi ambao wanaua watu wengi kwa muda mrefu sana. Tangu nikiwa binti mdogo watu wanafariki na juzi tu kuna mtu ameliwa na mamba na vilevile watu watatu wameshaliwa na mamba miezi miwili iliyopita. Je, Serikali haioni haja ya kwenda kuvuna mamba wale hata kama mto ule hauko ndani ya hifadhi, lakini mamba ni maliasili? Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Lile la pili lile umechomekea Mheshimiwa, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ana majibu ya mambo haya, tafadhali majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanaisha kwa maswali mazuri ambayo ameyaelekeza kwa Serikali, likiwemo hili la wanyamapori hai. Nataka nimwondoe wasiwasi, tunaposema wanyamapori hai ni wanyama wa aina yoyote iwe mdudu, nani, anaposafirishwa nje ya nchi sisi kama Maliasili na Utalii tunatambua kwamba, hiyo ni rasilimali ya nchi na haipaswi

kuhamishwa kutoka eneo moja kwenda nje ya nchi. Kwa hiyo, nataka nimto wasiwasi na ndio maana hata hawa mamba pengine hawapo hata kwenye hifadhi, lakini kwa kuwa ni maliasili za Taifa lazima tuzilinde. Tunazilinda ili tuweze kuleta watalii ndani ya nchi waje kuona na tunapata mapato kutohama na vivutio hivi tulivyonavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi maswali yote nimeyajibu kwa pamoja, lakini hili la kuvunwa mamba nimtoe wasiwasi, mwezi uliopita tulikuwa tuna tathmini ya kukusanya *data* ya mamba wote ambao wamekuwa wakisumbua wananchi. Tayari tuko kwenye mkakati wa kwenda kuwavuna, hivyo muda wowote ninavyosema kuanzia sasa, tutatuma wataalam wa kwenda kuvuna mamba hao. Naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwanaisha usome vizuri hili jibu; kwa kifupi ni kwamba, usafirishaji wa viumbehai hautakuwepo. Katumia tu maneno mengi marefu ya kueleza Mheshimiwa Naibu, ndio maana yake na kama utakuwepo sio viumbe hai watakuwa ni wale waliokaushwa, maana yake ni viumbe mfu. Ahsante sana.

Tunaendelea na Mambo ya Ndani ya Nchi, swali la Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo. Tafadhali.

Na. 56

Hitaji la Magari ya Vituo vya Polisi Vunjo

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Vituo vya Polisi vilivyopo katika Kata za Kilema, Kirua Vunjo, Kahe na Marangu katika Jimbo la Vunjo vinapewa usafiri?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nimekuona.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa magari katika vituo vya Polisi vilivyo katika Jimbo la Vunjo ambavyo ni Kilema, Kiruavunjo, Kahe na Marangu kama vyanzo muhimu katika kutendea kazi. Kwa kupitia mkataba wake wa kampuni ya *Ashok Leyland* ya nchini India, Jeshi la Polisi linategemea kupokea magari 369 na pindi magari hayo yatakapofika kipaumbele kitatolewa kwa vituo vya polisi vyenye uhitaji mkubwa ikiwemo kituo ama vituo vilivyo katika Jimbo la Vunjo. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Nawapongeza sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi jinsi mnavyojibu maswali. Kifupi, *direct to the point*, hongereni sana na wengine basi tuige hiyo, tujielekeze zaidi kwenye swalii, tutajikuta tunaokoa muda wa Bunge.

Mheshimiwa Kimei nimkuona.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, licha ya majibu mazuri yaliyotolewa na Wizara. Swalii la kwanza; Jimbo la Vunjo ni jimbo liliilo mpakani. Majimbo yaliyo mpakani yanakuwa na changamoto tofauti kidogo, kwa mfano, magendo na unajua Wachaga wanavyopenda magendo. Dawa za kulevyaa zinaingia halafu kunakuwa na uhamiaji haramu. Kwa hiyo, kuna umuhimu na tunaomba Serikali ituhakikishie kwamba, itachukua hatua gani ili kuimarisha ulinzi kwenye vituo vya polisi kwa kuongeza polisi pamoja na kuongeza bajeti kwa sababu, wanahitaji kuchukua za haraka wakati mambo kama yale yanapotokea?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili ni kwamba, kule Vunjo unywaji wa gongo, ulaji mirungi, bangi, dawa za kulevyaa umekithiri kwa sababu, *of course* watu hawana ajira wengi,

Iakini ukweli ni kwamba, imekithiri sana. Najua kwamba, Serikali za Mitaa zinafahamu jambo hili, iakini linahitaji *national effort* na tunataka tuombe Wizara iweze kutueleza inachukua mikakati gani ya kuweza kushughulikia tatizo hili la unywaji pombe kali, bangi na vitu vyote kama hivyo, *otherwise tutapoteza kizazi?*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, niku-*caution* tu kabla hujajibu swali hilo ni zito, hii gongo hii matatizo makubwa yameanzia kule Rombo mpaka akinamama wakaandamana, sasa Vunjo nako wanalamika hii gongo, nini.

Je, Mheshimiwa Waziri anachouliza unasubiri mpaka wanawake wa Vunjo nao waandamane? (*Kicheko*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Vunjo, Dkt. Charles Stephen Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatutasubiri mpaka tufike sasa watu waanze kuandamana. Serikali kupitia Jeshi la Polisi tuna mikakati madhubuti ambayo tumelfanya na tunaendelea kuifanya. Ya mwanzo, ni kuhakikisha kwamba, tunafanya doria za mara kwa mara ili lengo na madhumuni kuweza kukamata na kukomesha hizo tabia pamoja na kwamba, zinakuwa na changamoto kidogo, iakini tutajitahidi katika kuhakikisha kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaendeleza sasa suala zima la ulinzi shirikishi; lengo na madhumuni sasa jamii iweze kutumia fursa ya kuchukua nafasi ya kuelimisha vijana wao ili sasa vijana waweze kupunguza hii, iakini kikubwa zaidi tunachukua hatua za kisheria. Kwa hiyo, wale vijana ambaa wanafanya hili, basi tutawachukulia hatua za kinidhamu, hatua za kisheria, ili vijana waweze kuachana na tabia au

vitendo vya utumiaji wa dawa za kulevya na utumiaji wa hiyo gongo kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nadhani maswali yalikuwa mawili, lakini yote yalikuwa yanaangalia kwenye gongo na bangi na masuala mengine. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Nathibitisha kwamba, gongo ni kero kwa akinamama Kilimanjaro, eeh, mwakililishi wa akinamama wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Shally Raymond uliza swali lako, tafadhali.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Niseme nimepokea kwa furaha taarifa njema za magari 369 ya Polisi yatakayokuja. Swali langu. Je, katika magari hayo na ukizingatia kwamba, Kilimanjaro ina kata 169 na za mlimani ziko kama 110 zikiwemo kata za kule Siha, zikiwemo kata za Moshi Vijijini, Kata za Same, Kata za Mwanga na Kata za kule Rombo. Je, Serikali iko tayari sasa kupatia zile kata za mlimani ambazo haziko mjini magari hayo?

SPIKA: Waheshimiwa, magari yale hayaingii kwenye yale makorongo kule gongo inakotengenezwa. Hata magari yakija sasa kule korongoni, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, inasogezea wananchi huduma za ulinzi na usalama popote walipo. Moja mionganoni mwa mambo ya msingi ambayo Serikali imeazimia kufanya kwanza ni kuhakikisha kwamba, tunatengeneza vituo vya polisi, lakini pili kuwatafutia magari ya polisi ambayo yatakwenda kufanya doria katika maeneo mengi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mionganoni mwa maeneo ambayo yatafika haya magari tutajitahidi sana maeneo hayo ameyataja na

huko kwenye mkoa wake magari haya yafike ili yaweze kutoa huduma. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. kule Msekwa nimekuona Mheshimiwa Mtemvu, uliza swali lako sasa.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, wananchi wengi wa maeneo ya pembezoni katika Jimbo la Kibamba, hasa maeneo ya Mpijimagohe kule Mbezi, Tegeta A kule Goba na maeneo ya Ukombozi kule Saranga, wameanza kujenga maboma ya vituo vya polisi kwa ajili ya usalama wa maeneo yao. Je, Serikali ni lini sasa itakuwa tayari kukamilisha maboma yale ili wananchi wale wapate usalama katika maeneo wanayoishi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Tafadhalii Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu tena swali la Mheshimiwa Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mambo yote ambayo yanaelezwa au vitu vyote ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kufanyiwa wananchi kutoka katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, hasa kwenye Jeshi la Polisi, ni mambo ambayo yanahitaji fedha. Tukizungumza vituo vya polisi, fedha, tukizungumza magari, fedha, tukizungumza nyumba za askari, tunahitaji fedha. Nimwambie tu mheshimkiwa Mbunge kwamba, kwa sasa tunakwenda kutafuta fedha na tumeshaanza hiyo michakato ya utafutaji wa hizo pesa. Lengo na madhumuni ya kufanya hivyo ni ili tuweze kumaliza maboma yote nchini ambayo yanahitaji kumalizwa kuwawezesha wananchi kupata huduma za ulinzi na usalama. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Kwa sababu ya muda tuhamie Wizara ya Kilimo, swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis. Mheshimiwa Kamishna uliza swali lako.

Na. 57

**Utaratibu wa Kununua Mazao kwa Mkopo
kutoka kwa Wakulima**

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaondoa kabisa utaratibu wa kununua mazao kwa mkopo ambao unaendelea kutumiwa na baadhi ya Taasisi jambo ambalo linasababisha manung'unico kwa Wakulima?

SPIKA: Jibu la swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, nimekuona.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibuu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomari Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ni Taasisi za Serikali pekee chini ya Wizara ya Kilimo ambazo imekuwa ikizitumia kuchochea soko la mazao ya wakulima hasa mazao ya nafaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia *NFRA* na *CPB* imetumia jumla ya bilioni 119 kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya nafaka ambayo yatauzwa katika masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Oktoba, 2021 *NFRA* imetumia jumla ya bilioni 37 kununua jumla ya tani 75,000 za mahindi na *CPB* imetumia jumla ya bilioni 12 kwa ajili ya tani 27,000 za mahindi na ununuzi unaendelea. Aidha, ununuzi huo umefanya katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa, Katavi, Shinyanga, Arusha na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, *NFRA* na *CPB* hazitumii utaratibu wa kukopa wakulima wa nafaka kwani, zimekuwa zikinunua nafaka kutoka kwa wakulima na vikundi vyा wakulima na

kufanya malipo mara baada ya mapokezi ya nafaka katika vituo vya ununuizi. Katika msimu wa 2021/2022 taasisi hizi zinaendelea na ununuizi wa nafaka kutoka kwa wakulima na vikundi vya wakulima kwa utaratibu wa malipo ya fedha taslimu na si kwa njia ya kuwakopa wakulima.

SPIKA: Mheshimiwa Fakharia, hawawakopi wakulima. Swalii.

MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nimepokea maelezo yake aliyonipa katika swali langu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza; kwa kuwa, Serikali inafahamu kwamba, suala hili la mikopo linaathiri sana wakulima wetu. Je, Serikali haionti kwamba, sasa ni wakati wa kuwafungulia milango wakulima kuweza kuuza mazao yao wao wenyewe ikiwa ndani au nje ya nchi ili kuweza kunusuru mazao yao kuharibika? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kwa kuwa, Serikali inawajali wakulima na inawathamini. Je, kwa nini Wizara haitengi bajeti maalum kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima yale yanayorundikana majumbani ambayo yanakosa soko ili kuweza kuwasaidia wakulima wao kunusuru nguvu zao na maharibiko ya mazao yao? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swalii hilo fupi, Mheshimiwa Bashe, Naibu Waziri, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kufungua milango Serikali imefungua milango kwa mkulima mfanyabiashara ye yeyote wa mazao kuuza popote pale duniani na hatazuliwa na mtu yeyote. Wizara ya Kilimo tunatoa vibali vya *export* bure kwa ajili ya kuuza mazao ndani na nje ya nchi na hakuna mfanyabiashara wala mkulima yeyote atakayezuiliwa kuuza popote anapopata soko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongeza bajeti kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima, sisi kama Wizara kama utakumbuka mpaka sasa hivi Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuongeza fedha za kununua mazao pale ambapo linapojoitokeza tatizo na Serikali hununua mazao kwa sababu kubwa mbili.

Mheshimiwa Spika, moja kwa ajili ya kuhifadhi; lakini mbili kwa ajili ya ku-stimulate soko pale ambapo mazao ya wakulima yanaanguka bei. Na utakumbuka hapa Bunge lako Tukufu lilileta hoja na Wabunge walibuka na hoja ya ku-rescue zao la mahindi na Serikali na Mheshimiwa Rais akaidhinisha matumizi ya shilingi bilioni 100 ambazo tumeenda kununulia mazao na mpaka sasa tunanunua mahindi kwa shilingi 500 kupitia taasisi yetu ya NFRA na ununuzi unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hatua ya kununua mazao tutaendelea kuifanya kadri ambavyo bajeti itakuwa inaruhusu na Bunge lako Tukufu likitupitishia fedha sisi tutaenda kutekeleza *field*. (*Makofii*)

SPIKA: Swalii la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Ritta Kabati

Na. 58

Mchango wa Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi (Diaspora)

MHE. DKT. RITHA E. KABATI aliuliza:-

(a) Je Serikali inayo *database* ya kutambua idadi ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi?

(b) Je nini mchango wa Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania katika kipindi cha miaka mitano?

SPIKA: Mheshimiwa Mbarouk Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki naomba kujibu Swalil Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitumia mifumo mbalimbali ya kutambua Watanzania wanaoishi nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na usajili wao kupitia Balozi zetu na Idara ya Uhamiaji kwa kutumia usajili wa hati za kusafiria za kielektroniki. Hadi kufikia Januari, 2021 idadi ya Watanzania wapatao Milioni moja na Laki Mbili (1,200,000) wanaishi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania wamekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Kwa mfano katika kipindi cha miaka mitano iliyopita michango yao imehusisha sekta mbali mbali zikiwemo; Sekta ya Fedha, Sekta ya Afya na Sekta ya Nyumba. Mfano, takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (*BoT*) zinaonesha fedha za kigeni (*remittance*) ambazo zimetumwa kupitia mfumo rasmi kutoka kwa Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano ni takriban Dola za Kimarekani bilioni 2.3 sawa na shilingi za Tanzania trillioni 5.3.

Mheshimiwa Spika, aidha, michango ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi katika Sekta ya Afya kwa kipindi cha miaka mitano inahusisha utoaji wa vifaa tiba, madawa, vitabu vyatua masuala mbalimbali ya afya na mafunzo ya elimu ya afya bora kwa wauguzi na madaktari kwenye hospitali za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Sekta ya Nyumba Watanzania wanaoishi nje ya Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano wamenunua nyumba zaidi ya 135 zenye thamani ya shilingi za Tanzania bilioni 29.7 kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*). Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Ritta Kabati nimekuona na Mheshimiwa Nusrat utamalizia swali.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulizie maswali mawili.

Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake lakini pia niwapongeza Watanzania kwa michango mizuri ambayo wamechangia nchi yetu wanaoishi nje ya nchi. Kwa kuwa *Diaspora* wakirudi nchini huwa wanachukuliwa kama wageni kwenye nchi yao.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutoa hadhi maalum kwa *Diaspora* kushiriki ujenzi katika uchumi na uwekezaji kabla hatujaweza kupewa uraia pacha?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, watanzania wanaoishi nje ya nchi wanapopata matatizo kwa mfano kesi, wamekuwa wakipatiwa msaada gani ukiwepo msaada wa kisheria?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje Balozi Mbarouk.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge ambaye ni mdau mkubwa sana wa *diaspora* kwa namna anavyowasemea na kuhakikisha fursa nyingi kwa wana *diaspora*. Wizara yetu kwa kushirikiana na taasisi za Serikali zote mbili za Tanzania Bara na Zanzibar na kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi wanaoshughulika na mambo ya *Diaspora* tayari imeanza kufanya tafiti ili kupitia sera, sheria na taratibu za nchi kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa watanzania wanaoishi nje kupata hadhi maalum.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili la msaada wa kisheria wakati wanapopatwa na matatizo kama vile kesi ni kwamba Serikali kupitia balozi zetu zimekuwa zikiwasaidia watanzania wanapopatwa na kesi nje ya nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuwatafutia mawakili mabobezi na waaminifu kwa gharama zao; pili, pale kesi inapokuwa katika Mahakama ubalozi umekuwa ukifuatilia kwa karibu sana kesi hizo ili kuona watanzania hawa wanapata haki zao kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi husika.

Mheshimiwa Spika, mwisho pale wanapomaliza vifungo vyao au wanapopata msamaha ubalozi unafanya uratibu wa kuhakikisha kwamba wanarudi nyumbani salama, ahsante sana. (*Makofit*)

SPIKA: Mheshimiwa Nusrat nilikuona.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ahsante kimsingi suala la uraia pacha na *Diasporas* limefanyiwa mjadala mpana sana kwa muda mrefu sana. Sasa kwa sababu Serikali na niipongeze kwa kufanya jitihada ya kutambua mchango wa *Diasporas* na tunaamini kwamba wakifungua wakipewa hati maalum ama uraia pacha pamoja na kwamba kuna *restriction* ya katiba hawaoni sana ifike hatua lifikasi tamati suala la kujadili masuala la uraia pacha na *Diaspora* tulifanyie kazi sasa kwa sababu tumeona *impact* yake ni kubwa zaidi kwa sababu Serikali yenyeewe ndiyo imetuambia sasa hiyo ni ndogo tu tukifungua tutapata faida nyingi Zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali haioni kama imefika hatua tulifanye sasa kwa vitendo suala la kutambua kuwapa hadhi maalum ama kutambua mchango wa *Diaspora* kiuhalali? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje Balozi Mbarouk tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nusrat Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa watanzania wanaoishi nje ya Nchi na kama nilivyojibu hapo awali ni kwamba tayari saa hivi Serikali inafanya tafiti ya kuangalia vipi tunaweza tukaangalia uwezekano wa watanzania hawa kupewa hadhi maalum. Hivyo namuomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda kidogo ili kumaliza tafiti na taratibu hizo ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana muda wa maswali umekwisha sasa tunaendelea na shughuli nyingine naomba niwatambue wageni kuna wageni wa Mheshimiwa Pauline Gekul sina hakika kama wapo?

Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sanaa Ndugu Mussa Nyoni yupo ahsante karibu sana. Msanii wa muziki wa kufoka foka Frida Amani ahsante sana, hivi huu muziki ndiyo jina lake rasmi? Kuitwa wa kufoka foka *hip hop* si kizungu ni kufoka foka? Kwa hiyo kumbe nimepatia ahsante sana.

Meneja Ndugu Frank Mkuvalwa karibu sana, Mratibu Ndugu Salum Mohamed ahsante na msaidizi binafsi wa Frida Ndugu Brenda Baptist karibu sana, karibuni sana Dodoma wanamuziki. Ninyi vijana wetu karibuni, muendeleze juhudhi hizi japo sisi wazee hatuelewagi yaani ule muziki mimi sielewi kabisa, lakini taratibu taratibu mtatubeba na sisi kuingia huko.

Pia kuna wageni 39 wa Mheshimiwa Esther Matiko naomba msimame wageni wa Esther Matiko karibuni sana sana Dodoma hawa ni wanajukwaa wa jambo Tarime kutoka mikoa mbalimbali karibuni sana na mwakilishi Mheshimiwa Esther Matiko yupo nafikiri mmemuona anapokaa hebu simama wakuone bwana nashukuru sana yuko mjengoni hapa amejaa tele Wanatarime kwa hiyo wanashirikiana na Mheshimiwa Kembaki. Mheshimiwa Kembaki yupo? Leo

Mheshimiwa Kembaki hayupo endeleeni kuwapa Wabunge wenu ushirikiano ili tuweze kupata Tarime tunayoitarajia ahsanteni sana kwa kufika. (*Makofi*)

Kipekee nimtambue mjomba Mwita Mantago Mjomba karibu sana bwana binti yako yuko salama hapa anafanya kazi nzuri lakini pia yupo kiongozi wa *group* zima hili ndugu Charles Segere karibu sana karibuni wana Tarime jana ilikuwa tuwe pamoja lakini bahati mbaya sana mniwie radhi mambo yalichanganyika lakini iko siku tuendelee kuombeana kila la kheri na katika *group* hili kwa kweli wana CCM ndiyo wengi kwa hiyo nawashukuruni sana, na humu ndani kuna wana CCM wenzenu wengi sana pia ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mmepata dodoso fulani mmetawanyiwa kila mtu mezani kama hujalipata basi tukulee makatibu wangu angalieni kama kuna Mbunge hajapata mumpatие linatoka Wizara ya Teknolojia ya Habari kwa ajili ya taarifa fulani za Jimboni kwako ili waweze kufanya kazi. Basi watakopitapita vijana wetu muwagutue ili wawapatie hilo dodoso muweze kulifanya kazi.

Katibu!

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mwongozo!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Pareso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 76 kwa sababu ya muda naomba nisii some.

Kunataka kujengeka utamaduni hapa Bungeni wa Serikali kutokujibu kikamilifu maswali ya Wabunge na leo wewe mwenyewe umekiri hapo kuna maswali mawili

hayajajibiwa kikamilifu lakini hata huko nyuma tuna ushahidi wa maswali mengi ambayo hayajibiwi kikamilifu na ama wakiljaribu jaribu sana kuyajibu hayana uhalisia na wakiendelea kujitahidi kujibu ni tofauti na kitu ambacho Mbunge amekiuliza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Kanuni za Bunge zinatutaka Wabunge tupeleke maswali siku 21 kabla ya Mkutano wa Bunge maana yake inaipa nafasi Serikali au Waziri kulisoma swalii la Mbunge kulielewa na hata ikiwezekana kwenda *physically* kwenye eneo na kuona uhalisia na hatimaye kuja na majibu ambayo wananchi wanatamani kuyasikia kutokana na Mbunge ameyauliza.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako je, hivi tuna haja tena ya kuendelea kuwa na kipindi cha maswali na majibu ama tukifute kwa sababu ya haya yanayotokea? au basi kiti chako Mheshimiwa kiamue namna bora ya sisi Wabunge tukiuliza maswali yale ambayo ni matamanio ya wananchi wetu tunaowawakilisha tuweze kupata majibu sahihi ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana kwanza suala la kipindi cha maswali ni suala la kikatiba ni Katiba inayoagiza kwamba Waziri yejote atajibu maswali ya Wabunge yoyote yanayohusu *portfolio* yake kuhusu Wizara yake na maswali hayo ni maswali ya wananchi na ni namna mojawapo ya uwajibikaji wa Serikali siyo tu kwa Bunge hili bali kwa wananchi wenyewe.

Kwa hiyo jambo hili lazima litaendelea la maswali kwa sababu tumeagizwa na katiba yetu ya nchi tunaendelea tu kusisitiza kuhusu kwa sababu kwa kweli wanaojibu maswali siyo wanaojibu maswali hapa kwetu ni Waheshimiwa Mawaziri lakini majibu mengi wanayapata toka kwa wataalamu wao. Kwa hiyo, baadhi ya wataalamu kidogo wakae sawa na hilo ni jukumu leni Mawaziri kuwabana wataalamu wawape majibu ambayo kwa kweli yanajibu swalii na kwa kifupi iwezekanavyo inasaidia sana kutuokolea muda humu ndani na tuweze kupata maswali ya nyongeza

kadhaa na likishajibiwa kirefu inabidi tuende mbele hata kama mmesimama nyongeza inakuwa vigumu kuzitoa kwa sababu muda wetu ni mdogo humu Bungeni.

Ninatamani ingekuwa *possible* tukatembelea Mabunge ya wenzetu ya *Commonwealth* tukaona maswali na majibu tena wao hawana saa moja kama sisi, sisi saa moja tunatumia maswali 10 lakini wenzetu saa moja wangeweza kutumia maswali hata 40 ndiyo swali jibu swali jibu na hili inaenda kote siyo tu kwa Waheshimiwa Mawaziri hata sisi Wabunge tunapouliza maswali ya nyongeza tunakuwa na *story* na hadithi ndefu ambazo hazihitajiki pia ziwepo. Kwa hiyo, tuendelee kukumbushana tu umuhimu wa kuuliza maswali kwa kifupi kwa sisi Wabunge hata unapotunga swali nenda *specific* kama ambavyo tumesitiza siku zote unauliza nini moja kwa moja.

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge *story, story* hazihitajiki ngonjera hapana ni kujaribu tu kujibu lile swali kwa kadri tunavyoweza. Tunajua baadhi ya vijana wanaojibu maswali haya ni hawa vijana wamemaliza hii ambayo tunamlalamikia Mheshimiwa Prof. Ndlichako kuhusu elimu yetu, kwa hiyo wanajibu jibu tu utumbo utumbo sasa ukileta hapa inakuwa la kwako wewe haliwi la yule ofisa wako kule ofisini aliyeandika. Kwa hiyo, ni vizuri na wewe ukajiridhisha kwamba hili ndiyo jibu ambalo linatakiwa kujibiwa. (*Makof*)

Kwa hiyo mwongozo wangu ni huo kwamba sote kila upande kwa wakati wake tujitahidi kwenye maswali na majibu tukaenda *specific* tukumbuke kwamba kila kinachofanyika kinaingia kwenye *Hansard* ambayo itakaa kwa miaka mingi sana vijana wetu huko mbele watakuwa wanashangaa kwamba hili swali lilijibiwa Bungeni na hili jibu eti lilikuwa ni jibu la swali hili na ilikubalika yaani tunaingiza kwenye *records* kichekesho cha sisi wenyewe tusipojirekebisha.

Kwa hiyo, lazima kabisa tujitahidi tujibu swali *briefly as possible* kwa sababu likiwepo la nyongeza utafafanua zaidi tukiwa kwenye *floor* hapa na majibu marefu tujitahidi sana

kuyafanya yawe mafupi kadri inavyowezekana ahsante sana katibu tena turudie.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:
Kamati ya Mipango.

SPIKA: Kamati ya Mipango Waheshimiwa Wabunge.

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae.
Tunaendelea na uchangiaji wetu. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABADALLAH – KATIBU MEZANI:

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa
unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka
2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na
Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Majadiliano yanaendelea, lakini kabla hatujaendelea nilisahau jambo moja, nafikiri sote tumesikia habari ya Mitihani ya Vyuo vya Kati vya Afya kuvuja, jambo hilo ni jambo lisilokuwa zuri linaweza kupelekea tukapata huduma za Afya toka kwa watu ambao ni *unqualified* kabisa. Kwa hiyo nakuomba Mheshimiwa Nyongo Kamati yetu ya kawaida hebu ikae na Mheshimiwa Waziri wa Afya mfuatilie jambo hili kujua tatizo ni nini ili kuona mapendekezo ya jambo kama hili lisijitokeze tena. Mjitätidi mkae kabla ya ljumlahaa na tuwekane sawa kidogo kwenye upande huo tujue shida ni nini na nini inaweza ikawa *way forward* kwa maana ya kuishauri Serikali. Ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Mheshimiwa Tunza Malapo atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu

aliyetuwezesha kukutana leo na mimi nikapata kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba ya Kamati ya Bajeti wamechambua vizuri na kutoa ushauri mzuri sana kwa Serikali. Kwa hiyo pamoja na yote ambayo sisi Wabunge tutaendelea kushauri lakini Serikali itulie isome hotuba ya Kamati ya Bajeti kuna mambo mengi ambayo yatasaidia nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba ya Bajeti ukurasa wa 27 wameeleza Serikali imekuwa ikileta vipaumbele vingi. Serikali imekuwa ikileta miradi mingi ya mikakati, lakini ni kama tu inatajwa kwenye mpango, inatajwa kwenye bajeti, lakini haifanyiwi kazi. Kwa mfano, kule kwetu Mikoa ya Kusini kuna ule mradi wa *LNG* kuna mradi wa Reli ya kutoka Mbamba *Bay* mpaka Mtwara kila siku inatajwa. Kuna mradi wa Makaa ya Mawe wa Liganga na Mchuchuma kila siku ile miradi imekuwa ikitajwa, lakini haifanyiwi kazi ama haitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo mradi wa Makaa ya Mawe, huo mradi wa reli ungekuwa umetekelvezwa leo hii tusingekaa humu ndani Wabunge wa Mikoa ya Kusini kuliili Bandari ya Mtwara haifanyi kazi vizuri, kwa sababu mizigo ingekuwa ina uwezo wa kusafirishwa vizuri kwa njia ya reli, Makaa ya Mawe kila siku yangekuwa yanaingia pale bandarini kwa uwangi wake maana yake meli zingekuwa zinafika na leo tusingekuwa tunahangaika kwamba makasha hakuna, meli hakuna, korosho badala ya kusafirishwa Bandari ya Mtwara ziende zikasafirishwe Bandari ya Dar es Salaam. Haya yote ni kwa sababu kuna miradi ambayo ingetekelvezwa ingesaidia ku- *boost* Bandari ya Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja kuhitimisha atuambie huu mradi wa Reli kutoka Mbamba *Bay* mpaka Mtwara unakwenda kutekelezwa ama hautekelezwi? Kama hautekelezwi basi auondoe kwenye mpango, siyo kila siku tunauona lakini haufanyiwi kazi. Pia aje atueleze mradi wa

Makaa ya Mawe wa Liganga na Mchuchuma unakwenda kutekelezwa ama hautekelezwi kama hautekelezwi asifanye kazi ya kuandika kwenye mpango kila mwaka, mimi huyu leo nipo Bungeni mwaka sita tunauona, lakini haujawahi kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzetu wa Kamati ya Bajeti wameshauri kama anafikiri hawezu kutekeleza aandike vipaumbele vichache ambavyo vitatekelezeka akishamaliza basi ahamie kwingine si kila siku anaandika halafu hatekelezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na bandari naomba mtuangalie watu wa Mikoa ya Kusini hususani Mtwara kwa jicho la huruma, kuhusu pembejeo za kilimo ya zao la korosho, unakumbuka kulikuwa na mjadala mkubwa hapa wa *export levy* na nini na nini, mwaka huu watu wamelima hivyo hivyo ingawa pembejeo zimechelewa korosho zimepatikana korosho tulitegemea zitasafiri kwa Bandari ya Mtwara, lakini pana changamoto haya zinaenda huko Dar es Salaam lakini tunaomba kwenye msimu ujao mpango huu uende ukatueleze unakwenda kuhakikisha vipi pembejeo za wakulima iwe wa korosho, iwe wa mahindi kwa sababu wenzetu huko Mikoa mingine nao pia wanalia mbolea imepanda bei na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango ukaeleze unakwenda kujipanga kwa namna gani kuhakikisha wakulima wa Tanzania ambao ni wengi wanachangia Pato kubwa la Taifa ingawa wanafanyakazi katika mazingira magumu na hatarishi wanakwenda kuwawezesha namna gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyngine kuhusu madeni ya Wakandarasi. Ukitu kwenye mpango, ukisoma hotuba mbalimbali unakuta kwamba nchi yetu hii inapoteza pesa nyngi sana kwa sababu ya kuchelewa kuwalipa Wakandarasi. Wakandarasi wanakuwa wamefanya kazi wamemaliza wamepeleka *certificate* kule, lakini Wizara ya

Fedha inachelewa kutoa pesa. Inapochelewa kutoa pesa kinachotokea ni nini, kunakuwa na riba, kunakuwa na tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ripoti ya CAG amekagua miradi saba tu, karibia Shilingi Bilioni 14 zinapotea kwa sababu ya Wizara ya Fedha kuchelewa kuwalipa Wakandarasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano tu, ujenzi huu wa reli ya kisasa umetoa riba na tozo kama hasara karibia Bilioni Mbili na *point fedha* hizi Wizara ya Fedha ingekuwa inalipa kwa wakati maana yake hizi fedha zingekwenda kufanya mambo mengine ya maendeleo. Kwa hiyo, katika huo mpango tunamuomba Mheshimiwa Waziri atueleze anakwenda kuhakikisha *certificate* za Wakandarasi zikifika anawalipa kwa wakati na pia asizalishe madeni mengine. Wakandarasi wallowengi ni wafanyabiashara wadogo wadogo, wanakopa benki wakitegemea wafanyakazi warudishe zile pesa, usipowalipa kwa wakati unawakwamisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee mambo mawili ya mwisho, la kwanza sisi watu wa Kusini tuna Mto unaitwa Mto Ruvuma una maji safi na mengi kweli kweli, lakini nikikuambia jambo la kusikitisha katika Mikoa yetu ya Kusini hususani Mkoa wa Mtwara ndiyo Mikoa ambayo inaongoza kwa ukosefu wa maji kwa kiasi kikubwa. Huu mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma kuja Mkoa wa Mtwara umekuwa ukizungumzwa siku nyingi unaandikwa lakini hautekelezeki. Naomba kwenye Mpango aende akatueleze ana mkakati gani wa makusudi wa kuhakikisha mradi huu wa maji kuyatoa Mto Ruvuma kuleta katika Miji ya Mtwara, Mtwara Mjini, Nanyamba, Tandahimba na kwingine unakwenda kutekelezeka kwa namma gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na ile barabara yetu kila siku tunaiongelea ya kutoka Mtwara Mjini inapita Tandahimba, Newala mpaka Masasi ya kilometra 210, wamejenga kilometra 50 tu hizo zingine wanakwenda kuzimaliza lini. Tunaomba mpango uje ueleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la mwisho kabisa, sasa hivi Serikali imekuwa ikikusanya mapato yake mengi kupitia mifumo, unapokwenda ardhi utapewa *control number*, unapokwenda *TRA* utapewa *control number* na kokote kule, lakini suala hili nimekuwa nikiliongea Serikali inapoteza mapato mengi kwa siku kwa sababu ya mifumo mibovu ukienda utaambiwa *network ipo chini hatuwezi* kupokea pesa, mwananchi anarudi na pesa yake. Mpango uje utueleze umejipanga viyi kwenda kuhakikisha wanaboresha hii mifumo ikiwezekana kuwe na utaratibu wa kukusanya *offline* mfumo ukirudi vizuri basi pesa iingie kwenye mapato ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Huo ni mchango wangu kwa leo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Malapo na umeanza kwa kutukumbusha pamoja na mambo mengine mradi wa Liganga Mchuchuma, tuseme tu sisi kama Bunge kwa kweli binafsi kama Bunge tumechoka kusikia habari ya Liganga na Mchuchuma. (*Makofii*)

Kwa hiyo, tungeishauri Serikali tuna miezi mitatu mwezi huu Novemba, Disemba yote Januari yote kabla ya Bunge la Februari tunadhani miezi mitatu ni mingi. Kama itafika Februari Bunge lijalo Serikali haisemi chochote cha maana kuhusu Liganga, Mchuchuma. Sasa wakati huo sisi tutachukua hilo jukumu tutaunda Tume Teule ili tulivae wenyewe, kwa sababu ni miaka mingi *over the years* tunaomba hapa Bungeni jamani Liganga na Mchuchuma *over the years!*

Sasa imefika mahali ambapo sasa ni wajibu wa wananchi wenyewe na wawakilishi wa wananchi ni hawa, nadhani tuende hivyo, Serikali m jitahidi tuna miezi mitatu, miezi mitatu ni muda mrefu sana, tufike mahali ambapo sasa tutakuja Bungeni ama tuseme kitu kitakachoeleweka ama sasa Bunge liunde Tume Teule halafu tutakuja na ripoti Bungeni na wananchi wa Tanzania wataelewa kuhusu nini habari ya Liganga na Mchuchuma. (*Makofii*)

Tunaomba sana Serikali, jambo hili ni mradi wa kimkakati ni mradi mkubwa ni mradi unaweza kusaidia *ku-revamp economy* yetu kwa kiasi kikubwa mmesema Wabunge mara nyingi, sasa lazima tuvuke hapo kwenye Liganga na Mchuchuma tukumbushane wakati huo Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Nape Nnauye atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato Chumi.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye haya mapendekezo. Nianze kwa kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kazi nzuri waliyoifanya, kwa kweli wamefanya kazi nzuri na mimi ni matumaini yangu kwamba Serikali watazingatia ushauri waliopewa na Kamati hii ya Bunge wamefanya kazi nzuri sana, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kushauri maeneo mawili makubwa, eneo la kwanza ni eneo la Deni la Taifa. Kwa taarifa zilizopo ukialingalia taarifa za Benki Kuu, hotuba ya Waziri na hata Kamati Kudumu ya Bunge ya Bajeti inaonekana Deni la Taifa limefikia trilioni 64, pamoja na kwamba taarifa zote zinasema kwamba deni hili bado ni himilivu lakini...

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kidogo tu.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Halima.

TAARIFA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuwa na nia ya kumuungilia Mheshimiwa Mbunge, lakini ninataka nirekebishe kidogo Deni la Taifa kwa mujibu wa taarifa ya BOTiliyotolewa mwezi Septemba ni Trilioni 78, Deni la Serikali ndiyo Shilingi Trilioni 64 na tukiongeza na Trilioni 1.3 tuliyochukua mwezi Septemba maana yake Deni la Serikali

sasa hivi ni Triliuni 65.7 huko. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba uendelee na mchango wako mzuri. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo Mheshimiwa Nape endelea na mchango.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea, amefanya ufanuzi ambao pengine nilidhani sikuwa na haja ya kwenda huko, lakini hoja yangu ni nini, kasi ya ukuaji wa deni hili pamoja na kwamba tunaambiwa deni bado ni himilivu kasi yake siyo kasi nzuri, kwa sababu linaturepeleka mbele ya safari siku tutakapoanza kusema siyo himilivu utakuwa ni mzigo mkubwa usiobebeka na itakuwa ni shida kwa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nипитie takwimu kidogo na hapa kwa kuwa Serikali inakopa kwa niaba ya wananchi na maana yake ni kwamba watakaokuja kulipa ni wananchi na Bunge tupo kwa niaba ya hao watakaokuja kulipa, nadhani ni vizuri tukafumbua macho tuangalie hii kasi inakotupeleka halafu tuwe wakweli tuambiane ukweli tuchukue hatua mapema kabla ya mambo hayajaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka Awamu ya Tatu tulihangaika na hili suala la Deni la Taifa na Awamu ile walichukua hatua ya kuzungumza mpaka tukafikia mahali pa kusamehewa baadhi ya madeni. Wakati ule awamu ile kwa miaka kumi zilikopwa dola Bilioni Tisa. Awamu ya Nne zikakopwa Dola Bilioni Saba kwa miaka 10, Awamu ya Tano kwa miaka Mitano mpaka Sita zimekopwa Dola Bilioni Tisa kwa miaka mitano mpaka sita. Bahati mbaya mkopo huu ambao nautathmini wa miaka mitano, sita asilimia 40 ni mikopo ya kibiashara ambayo moja ya sifa yake ina riba kubwa, lakini inalipwa kwa muda mfupi, kwamba inaiva mapema mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii imepelekea hali ilivyo kwa sasa kama hizi takwimu ni za kweli, katika mapato yetu kwa mwezi tunatumia zaidi ya billioni 800 kulipa deni ambayo ni asilimia 44 ya makusanyo kwa mwezi. Sasa kama kasi

itaendelea hivi maana yake ni kwamba kuna uwezekano mkubwa asilimia ya makusanyo kwa mwezi yakawa yanatumika *ku-service* madeni na matokeo yake yakaathiri shughuli zingine za utoaji huduma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pamoja na kwamba inawezekana namba zilizowekwa kufikia kutostahimilika bado zinaturuhusu, lakini siyo vizuri kupuuza kwamba fedha tunazotumia kulipa madeni kwa mwezi ni hela nydingi ambazo zinaathiri shughuli zingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninayo mapendekezo yafuatayo: Pendekezo la kwanza ni kwamba Awamu ya Sita wameanza vizuri sana kwa kuweka uwazi wa pesa walizokopa zinakwenda kufanya nini kwenye shughuli zetu na mfano mzuri ni hii 1.3 trillioni imewekwa mezani kila mmoja anajua mpaka muuza mchima anajua imekwenda wapi. Sasa pendekezo langu kwanza utaratibu huu uendeleee, upongezwe, uigwe uendeleee tuweke wazi yale tunayoyakopa tunapeleka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hizi za nyuma ambazo zimekopwa na hakuna uwazi mkubwa sasa tuende kufanya ukaguzi kwenye *account* ya Deni la Taifa tujue kilikopwa nini, kimeenda wapi, thamani yake nini, uhalisi wa miradi inayotekelizwa na thamani tulioambiwa iwekwe mezani ili tuige mfano mzuri uliofanywa na Rais Samia. 1.3 Trillioni imewekwa mezani kila mtu anajua, hizi zingine za kibashara tuende tukague na sisi ndiyo walipaji kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wale waliotutuma hapa, hili la kwanza la Deni la Taifa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kilimo. Tunasema huu mpango unatupeleka kwenda kujenga uchumi wa ushindani na shirikishi. Sasa nilitegemea kama kweli tunasema shirikishi nguvu kubwa ingepelekwa kwenye sekta ambayo inakusanya watu wengi haya maneno yangkuwa na uhalisia, hali ilivyo haya maneno hayana uhalisia na mimi ni maombi yangu kwa Serikali mtakapoleta mpango na Bunge hili wengi wameletwa humu na wakulima

tukipitisha mpango ambao hauna nguvu kubwa kwenye kilimo tutakuwa tunawasaliti walio tuleta hapa na hili jambo siyo sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinachangia asilimia 26 ya *GDP* yetu, lakini zaidi ya asilimia 70 au 80 ya Watanzania wameajiriwa kwenye Kilimo. Asilimia 100 chakula nchi, tunategemea kilimo; viwanda na maeneo mengine yote yanategemea kilimo. Sasa kama hali ni hii; ukiangalia miradi yote ya kielelezo, nitajieni mradi mmoja wa kielelezo ambao unashughulika moja kwa moja na kilimo, hakuna. Sasa kama hatushughuliki na kilimo, tunashughulika na nani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014 mlisafikia mahali tulikuwa tunatenga mpaka shilingi bilioni 200 kupeleka kwenye kilimo kama fedha za maendeleo. Leo bajeti hii tunayomaliza, tumetenga shillingi billioni 80. Sasa badala ya kwenda juu, tunarudi chini, hii siyo sawa. Sasa mapendekezo; najua muda wangu unakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Serikali ilete mpango na bajeti inayojiungamanisha na walio wengi kwenye sekta yao. Tuanzie mahali rahisi sana; llani ya Uchaguzi inasema tunatakiwa mpaka 2025 tuwe na hekta 1,200,000 za umwagiliaji. Tuna 600,000. Mimi nilitegemea kwenye Mpango walau hata hekta 150,000 au 200,000 ingeonekana kama ndiyo mradi wa kielelezo wa kugusa walio wengi. Sasa ninyi hakuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siipingi miradi hiyo, lakini ni kweli inagusa walio wengi masikini katika nchi hii? Hapana. Inawezekana inasaidia kwa pembeni, lakini hebu tubadilishe mwelekeo. Mwalimu Nyerere alituambia maendeleo ni ya watu, hata kama tutabishana. Kwa hiyo, pendekezo langu la kwanza, mtakapoleta Mpango, njooni na namna ya kupata fedha za kuweka walau hekta 200,000 au 150,000 ili tuanze hatua ya kufikia hiyo 1,200,000. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, tumezungumza sana hapa suala la kuwa na mfuko wa kusaidia, au mfuko

wa ruzuku kwenye mazao. Dunia ikitikisika sisi wote tunayumba, kwa nini? Hatuna fedha ya kusaidia ruzuku kwenye mazao. Nilitegemea Mpango huu ungekuja na suala la Mfuko wa Ruzuku kwa mazoa yetu kama moja ya miradi elekezi ili tutoke hapa tulipo.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nape Nnauye, umetupa *food for thought* kwenye eneo la vipaumbele, ndiyo maana umeniona nahangaika hapa. Maana safari hii Waziri wa Fedha hajaweka kama tulivyozoea kwamba, kwa mfano kipaumbele cha kwanza safari hii ni kipi na kinachofuata ni kipi? Kidogo wameweka kwenye utaratibu tofauti kidogo na kawaida. Utaona maeneo ya kipaumbele kwa 2022/2023 la kwanza ni miradi ya kielelezo, inavyoelekea ni kipaumbele cha kwanza na imetajwa miradi yenye ya kielelezo.

Halafu kuimarisha mazingira wezeshi, halafu miundominu na huduma; reli, madaraja, na kadhalika; halafu usafiri wa majini, vivuko, bandari halafu usafiri wa anga, nishati hali ya hewa, *TEHAMA*; halafu miundombinu ya Kitaasisi, Utawala Bora na Utawala wa Sheria. Sina haja ya kuendelea, yaani kilimo kwenye kipaumbele cha safari hii ni hakuna kabisa. Kwa kuwasikiliza Wabunge toka wameanza kuchangia Mpango huu, tunaomba muende mkafumue kabisa, kipaumbele cha kwanza kiwe kilimo. (*Kicheko/Makof*)

Tulisema Bunge letu hili la miaka hii mitano, tunataka tufanye kitu kwenye kilimo. Kwa hiyo, tunawaombeni sana wenzetu, tusipokuwa na Mpango ambao unashughulika na kilimo biashara, siyo kilimo cha kula na nini, basi tutakuwa tuna taabu kidogo.

Mheshimiwa Nape wakati anachangia, nilitumia muda wangu mwingi kutafuta kwenye vipaumbele vyetu tuko mahali gani na Wabunge wengi wamechangia jambo hili. Tunaomba mkae mlipe kipaumbele cha aina yake. Kilimo ndiyo kinaweza kututoa na siyo kitu kingine. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Cosato Chumi, halafu Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. CASATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nianze mchango wangu kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais. Niliwahi kusema hapa wakati wa Bunge la Bajeti kwamba Mheshimiwa Rais kama Mkuu wa Nchi na Mkuu wa Dola, ndiye *Diplomat* namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu ametendea haki ile kuwa *Diplomat* namba moja, kwanza ambavyo mmewona anashiriki katika shughuli mbalimbali Kimataifa na matunda yake tumeyaona ikiwemo pamoja na huu mkopo ambao tumetoka kuzungumza na mchangiaji aliyejita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi kwa Mheshimiwa Rais kama *Diplomat* namba moja, nilikuwa napenda kutoa changamoto au wito kwa wataalamu wetu; kwa mfano nitanukuu hapa, wakati Mheshimiwa Rais akiwa kwenye Mkutano wa Mazingira kule *Scotland*, amesema kwamba tunapimwa kwa vitendo vyetu na siyo kwa ahadi kubwa kubwa. Mheshimiwa Rais alikuwa na uthubutu wa kuyaambia Mataifa makubwa ambayo yamekuwa yaki-*pledge* katika kuchangia masuala mazima ya madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi; na amesema, naomba kunukuu.

"Mabadiliko ya tabia nchi ni suala la dunia nzima na hivyo majawabu yake ni lazima yawe ya Kimataifa na hivyo tunatoa wito kwa nchi zilizoendelea ambazo ndiyo zinazoongoza kwa uchafuzi, zitekeleze kwa vitendo ahadi zao

za kupunguza madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwa kutoa fedha za kutosha kutuwezesha sisi nchi za kipato cha chini kufanikisha malengo yetu kwenye michango ya Kitaifa ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kwa uendelevu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa nilikuwa napenda kushauri wataalam, kuna fedha ambazo pamoja na kuwa nchi zilizoendelea hazitoi kwa kiwango kinachotakiwa, lakini kuna fedha zinazotolewa katika mifuko mbalimbali, nitaitaja baadhi kama vile *Climate Investment Funds, Green Climate Funds, Adaptation Fund* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mifuko hii ili uweze kupata zile fedha ambazo kwa namna moja au nyininge zitawezesha Taifa lako kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, zitawezesha nchi kama Tanzania, watu kama wa Iringa, watu kama wa Mufindi na Njombe ambaao wanapanda miti kwa wingi na hivyo kusaidia dunia kupunguza hewa ya ukaa ili uweze *ku-access zile funds*, lazima kuna vigezo kama Taifa uwe umepitia na umefikia. Baadhi ya vigezo lazima uwe na taasisi ambazo zimekuwa *accredited* au zimepata ithibati ambapo ndani ya ule utaratibu utaeleza zile fedha utatumiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Rais ameshafungua mlango. Kwa hiyo, pamoja na kwamba nchi hazijatoa fedha kwa kiwango kikubwa, lakini kile kiwango ambacho kipo kwa Taifa letu mpaka ninapozungumza sasa, ni taasisi mbili tu; ni *NEMC* na *CRDB* ambaao wamekidhi hivyo vigezo, wanaweza *ku-access* *hizo Fund*. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Mpango kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, (Mazingira) tuwezeshe taasisi nyangi ziweze kujengewa uwezo. Sisi watu wa Mafinga na Mufindi ambaao tunachangia kupunguza shida katika mabadiliko ya tabianchi tuweze *ku-access* zile *funds* ili kusudi ziweze kutusaidia katika kukabiliana na madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi kama Kenya, Rwanda na Morocco, wanapata mabilioni ya pesa kila

mwaka, kwa sababu tu wameweza kukidhi vigezo ambalo ni jambo la kawaida. Hapa nitoe wito kwa wenzetu wa Vyuo Vikuu, Taasisi za Elimu ya Juu, hebu zitusaidie katika kuona zinaweza kujengeaje uwezo taasisi mbalimbali; za Serikali na za binafsi ili tuweze ku-access hizo *funds* kusudi siyo tu watu wa Mufindi, Mafinga, Iringa na Njombe wanufaike, lakini Taifa zima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ambalo napenda kushauri kwenye Mpango, tunatumia pesa nyingi sana kuagiza sukari na mafuta ya kula. Kwa mfano, katika mafuta ya kula, tunatumia karibu shilingi bilioni 500 kuagiza mafuta kula. Kwenye sukari vivyo hivyo; kila mwaka tunakuwa na uhaba wa sukari na sukari inapanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwaandikia Mawaziri kadhaa kuhusiana na ushauri kwamba pamoja na ule mradi mkubwa wa Mkulazi, bado kama Taifa tuna maeneo ambayo tunaweza tukawekeza katika *small scale industry* na Taifa likajitosheleza kwa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala zima la mafuta ya kula, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, namwona kila mara anaenda Kigoma kwa ajili ya masuala mazima ya Mchikichi. Yaani kama Taifa, ninashauri sana Mpango kama uliyosema katika kilimo, hebu tujielekeze katika kupunguza kutumia fedha za kigeni kuagiza bidhaa ambazo hapa hapa nchini tunaweza tukazilisha ikiwemo sukari na mafuta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 126 wa Mpango, umesema mambo mbalimbali ikiwemo kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuboresha uvezeshaji wananchi kiuchumi, kukuza sekta binafsi na mwisho wa yote ni kuchochea maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa napenda kuishauri Serikali na Mpango kwa ujumla, wakati tunatengeneza mazingira ya uwekezaji kuvutia wawekezaji, ninashauri pia wawekezaji hawa tunaowavutia katika kule

kuwekeza kwao kuwe na mantiki na kusaidie kunyanya u maisha ya wananchi. Kwa nini nasema hivi? Ukija pale Mafinga tuna wawekezaji wengi sana kutoka China wamewekeza kwenye mazao ya misitu, lakini ile biashara namna wanavyofanya, pamoja na kuwa tunasema tupo kwenye soko huria, lakini soko huria ambalo haliwi *regulated* litakuwa soko holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninapozungumza, pamoja na Serikali ya Mkoa naya Wilaya kuwasaidia watu wanaouza magogo kwa Wachina, kuna kitu kinaitwa *betting*; yaani unaenda pale na gari lako, umepakia magogo, unamuuzia Mchima mwenye kiwanda, mnaanza kubishana. Anakwambia hii ni shilingi 700,000/=, wewe unamwambia hapana ni shilingi 900,000, laki saba na nusu, laki nane na nusu, inaitwa *betting*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naishauri Serikali watusaidie kuweka bei elekezi ili wale watu wanaouza magogo kwa wale wawekezaji waweze kuuza kwa bei ambayo itarejesha gharama zao na pia watapata faida ili kwenye ule ukurasa wa 26 tunaposema kuchochaea maendeleo ya watu, basi tuweze kuwa tumechochea maendeleo ya haya watu kesho waweze ku-*afford* huduma za afya, waweze ku-*afford* huduma za elimu na kadhilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo, nimalizie na suala la mbolea. Mimi nilifanya ziara katika baadhi ya maeneo, mwananchi mmoja alinishika hivi ananitingisha, ananiuliza, njibbu Mbunge; niuze madebe mangapi nipate mfuko mmoja wa mbolea? Kwamba debe la mahindi ni shilingi 5,000/=; mfuko wa mbolea shilingi 100,000/=. Yaani auze madebe 20 apate mfuko mmoja wa mbolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nami naungana na wewe na Mheshimiwa Nape, lazima Mpango ujielekeze kwenye suala zima la kilimo ambacho kinachangia pato la Taifa kwa asilimia 26.6; bidhaa zote zinazouzwa nje kilimo kinachangia asilimia 26; lakini zaidi ya asilimia 70 ya

wananchi wamejajiri kwenye kilimo; lakini leo hii mfuko wa mbolea ni shilingi 100,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali na kwa Mpango kwa ujumla, pamoja na kujenga viwanda, lakini pawe na uwezekano wa kuweka ruzuku kwenye mbolea.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru na ninasema, Bwana asipoulinda Mji, waulindao wakesha bure. Mungu ailinde nchi yetu. (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Umemaliza *in style*. Ahsante sana.

Nafikiri Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira mmesikia mchango wa Mheshimiwa Mbunge. Sijui kwenye *Adaption Fund* kama kumebadilika, lakini hata *President* wa ule mfuko alikuwa ni Mtanzania, Ndugu Muyungi. Mahela kibao, lakini wanaoomba, wanaoruhusiwa kwetu ni hao wawili; *NEMC* na *CRDB* basi. Ni kuwezesha tu *organizations* tupate zile fedha. Zikifika kule Wizara ya Fedha, kama nilivyokuwa nashauri siku za nyuma; zisihamie huko tena. Ziende kule zinakolengwa. Ni kujipanga tu, fedha zipo duniani huko ili kuweza kutusaidia.

Sasa kwa nini wakwetu ndio Mwenyekiti mwenyewe anayegawa, halafu Rwanda, Burundi, Kenya ndiyo wanapata fedha nydingi. Ni sisi wenyewe kujipanga kwenye namna ya kuomba zile fedha na kuzi-access.

Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, nilikutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia jioni hii ya leo. Kwanza kabisa, nami niungane na wengine wote ambao wametoa pongezi nyingi sana kwa mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu, Rais wetu ambaye kwa kweli amefanya mambo mengi sana makubwa na mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna usemi unasema kwamba mzigo mzungu umpe Mnyamwezi, lakini kwa kazi nzuri mama anayoifanya, inaonesha kwamba sasa tubadilike, tuseme kwamba mzigo mzungu mpe mwanamke na wanawake tumekuwa tukibeba mizigo mzungu sana na ninyi akina baba mnajua kwamba mizigo mzungu huwa haitushindi. Tuna imani kabisa mama hatashindwa. (*Makof/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitoe pongezi...

MWENYEKITI: Nilisikia kuna taarifa upande huu. Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, endelea na mchango wako. (*Makof/Kicheko*)

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawe ni lazima uunge mkono kwamba wanawake huwa hatushindwi, mizigo mzungu yote huwa tunaiweza. (*Kicheko/ Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea Mpango ili tuweze kuujadili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitakuwa sijatenda haki kama nisipompongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Dkt. Sillo na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti, kwa kweli wametuafanulia vizuri sana huu Mpango na ndiyo maana tumeweza kuuchangia vizuri. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri, wala hawakufanya kosa kuwachagua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa kweli niungane na wote, nianze mchango wangu kwa kuchangia Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo kama ambavyo imesemwa kwamba Watanzania zaidi ya asilimia 65 ni wakulima. Vilevile Sekta ya Kilimo inatoa ajira karibu asilimia 66.3; pia inachangia katika viwanda asilimia 60; na pato la Taifa ni asilimia 26. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wajumbe wote kwamba bado kabisa Wizara ya Kilimo hajjaweza kupewa kipaumbele cha kutosha. Bajeti ya Wizara ya Kilimo ni ndogo sana. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Siku zote tumekuwa tukilalamikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Tunao Mawaziri wazuri sana tu katika Wizara ya Kilimo; ni wazuri sana kwa sababu tunafanya nao kazi, lakini katika Kamati yetu ya Kilimo tunao wabobezi wazuri sana. Tuna Wajumbe wazuri ambao siku zote wamekuwa wakitoa michango yao, tumekuwa tukitoa michango yetu pale, tumekuwa tukitoa hoja zetu, tumetoa ushauri mzuri kuhakikisha kwamba kilimo chetu kiwe na tija, lakini je, hii michango, huu ushauri unachukuliwa wakati gani na kufanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumeona Mpango umekuja, lakini mambo mazuri ambayo tumeishauri Serikali yetu, bado hatujaona kama yamechukuliwa katika huu Mpango. Sasa nilikuwa naomba kuwepo basi na mkakati tuone yale tuliyoyashauri yamefanyiwa kazi kiasi gani? Yametekeleza kiasi gani? Kwa nini hayatekelezeki? Nini tufanye ili tuwe na mipango mizuri kuhakikisha kwamba kilimo kinaweza kuisaidia nchi yetu? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima nchini kwa kweli wamekuwa wakilima tu kilimo cha mazoea. Wakulima wetu wanalia, wakulima wetu wamekuwa wanafanya kazi kubwa, lakini hamna wanachokipata. Watu wanajuta hata kuwa wakulima. Ili kilimo chetu sasa kiwe na tija, tunahitaji tuwe na Mpango mzuri. Tuhakikishe tunakuwa na Maafisa Ugani. Tunaona wakulima wengi wanalima bila kuwa na elimu ya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda mkoa wetu wa Iringa unaona hata kusafisha mashamba wanachoma. Leo Iringa wanalia, misitu imeungua; ukienda Kilolo au Mufindi, sasa hivi tumeunguza mashamba mengi kwa sababu wakulima hawana elimu ya kutosha kuhakikisha kwamba wanafishaa hata mashamba tu kwa utaalamu. Vilevile wanalima kilimo ambacho hakina tija kwa sababu wanafundishana wao wenyewe. Kuna *shortage* kubwa sana ya Maafisa Ugani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuwepo na ruzuku katika pembejeo. Ukipanya ziara sasa hivi tatizo kubwa ni bei kubwa ya mbolea. Wananchi sasa hivi wameanza kuanda mashamba, bado mbolea iko bei juu sana, hawajui wafanye nini. Naomba ruzuku ya pembejeo ni muhimu sana tupate mbolea, bei iwe chini, lakini pia hata mbegu bora ziwe bei ya chini kabisa illi wakulima wetu waweze kulima killimo chenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuwepo na uzalishaji wa mbegu bora, lakini vilevile masoko ni tatizo kubwa sana kwenye nchi yetu. Wakulima wanalima mazao mengi lakini hawana uhakika wa soko la kesho litakuwaje, wanakuwa wanalima kwa hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba vilevile ujenzi wa vihenge pamoja na maghala, ni muhimu sana. Sasa hivi wakulima wengi hawana sehemu za kuhifadhi mazao yao, changamoto ni hiyo sasa mazao hayo yanashambuliwa na wadudu. Tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, alikuwa ametoa zile bilioni 100 kwa ajili ya soko la mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, unaona kutokana na kutokuwa na maghala sehemu ambayo wakulima wapo wameshindwa kwenda kuuza yale mahindi kwa sababu ukiangalia gharama ya kupeleka yale mahindi sehemu ya kununulia yale mazao, ni mbali na ni ghali, kiasi kwamba bado hawajafaidika, waliofaidika ni madalali ambao wao wanachukua mahindi wanayapeleka kwenda kuyauza kule kunakotakiwa kununuliwa yale mahindi. Kwa

hiyo niombe maghala ikiwezekana yawepo kila kata ili kusaidia wakulima kupata urahisi wa kuhifadhi mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wakulima hawakopesheki benki; benki zetu haziwakopeshi wakulima. Kwa sababu tunayo Benki ya Kilimo tulitegemea sasa hii benki ingekuwa msaada kwa wakulima, wangepewa ruzuku ya kutosha ili wakulima wakope kwa riba nafuu, lakini benki hii bado hatujajua sasa imekuja kumsaidia mkulima au imekuja kufanya biashara, kwa sababu bado riba iko juu sana. Kwa hiyo, naomba uwepo mpango mkakati kuhakikisha wakulima wetu wanakopesheka ili waweze kulima kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie kuhusu jitihada ya Serikali kulipa madeni ya wazabuni, lakini vilevile hata wazabuni wa pembejeo wengi bado wanadai. Nilitegemea hawa wazabuni wangelipwa kwa wakati ili waweze kuleta sasa hizo pembejeo kwa wakati na ziweze kufikia wakulima kwa wakati. Hata hivyo, wazabuni mpaka leo hii bado wanadai madeni makubwa, wanashindwa kwenda kununua hizo pembejeo, kuwasogezea wakulima ili waweze kulima kwa wakati. Misimu inakuja bado ukienda kuwaona wale wa pembejeo wanasema bado wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwepo mkakati madhubuti wa kuhakikisha kwamba wazabuni hawa wanalipwa. Wengi wao wamechukua mikopo benki, wengi wao wanatishiwa kuuziwa mpaka mali zao. Sasa naomba kwa kweli wazabuni wa pembejeo wapatiwe pesa zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano kuhusiana na mkulima wa nyanya, kwa sababu hata mimi ni mkulima wa nyanya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Wabunge wanapochangia tunapata nafasi ya kupitia hili kabrasha, kwa kweli safari hii hii kazi mngetutendea haki kidogo Wizara ya Fedha, hasa hii Sura ya Nne ya vipaumbele. Yaani mpango huu umejikita katika kutumia, *expenditure* zaidi; madaraja, reli, SGR, kutumia, lakini utatumia kutoka kwenye nini, si lazima mpango wako uwe unalenga ku-*boost* vipi kipato chako ndiyo utumie?

Sasa huko ndiyo hatukunanihii vizuri na hasa hii Sura ya Nne ndiyo kabisa. Mkaiangalile vizuri, ninyi wenyewe ndio Wachumi, *you might be right*, tunasema tu kwa sababu tunajadiliana, *you might be right*, lakini hata ukienda kwenye kilimo kwa mfano, ambayo iko mwisho huku, kwa dakika moja tu; kufanya tafiti za ugunduzi wa aina ya mbegu, kuongeza uzalishaji/usambazaji, kuimarisha huduma ya ugani, kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, kuimarisha upatikanaji wa masoko, viwavi jeshi na kadhalika kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa mitaji, kuimarisha usalama wa chakula, kuimarisha TEHAMA, wamemaliza.

Sasa hivi tunahangaika na jambo la mbolea linapasua kichwa, watu hawalali, hata kwenye Mpango wenu hapa kwamba kuna kushughulika na jambo la mbolea hakuna. Kwa hiyo hilo tatizo litakuwa *permanent* kwetu? Kwa hiyo, lazima mipango yetu iende na matatizo halisi ya watu. (*Makofii*)

Mwaka huu tunalalamika na mwakani tulalamike tena kuhusu mbolea na mwaka keshokutwa tena? Lazima kwenye mpango wetu tuoneshe namna gani tunakwenda ku-*solve* hiyo *problem* na kadhalika, vitu vyा namna hiyo kwenye kilimo.

Nilikuataja Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, utafuatiwa na Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. ABDULLAH ALI MWINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Natoa shukrani zangu za dhati kwa kunipatia wasaa kuchangia huu Mpango kwa dakika chache ambazo tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kuwepo leo hii. Pili, kuwashukuru Kamati kwa uchambuzi wao mzuri na kuainisha yale ambayo sisi kama Wabunge tuyatazame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri au mbaya Mheshimiwa Nape Nnauye na wewe mwenyewe kwa sehemu kubwa mmenifilisi yale ambayo nataka kuyazungumza, lakini nitagusia mambo fulani kuzungumza kiini cha nini tunachotaka kukifanya na katika killimo tutazame maeneo gani ili tuboreshe Mpango na tuboreshe maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za UVIKO-19 ni mtambuka. UVIKO-19 umetuathiri kiafya, kiuchumi na kijamii. Maisha ya walimwengu yamebadilika kama vile usafiri wa anga ulivyobadilika baada ya matukio ya Osama Bin Laden, usafiri wa anga umebadilika kabisa na UVIKO-19 maisha yetu ndani ya ulimwengu huu tulikuwa nao hayawezikurudi kama yalivyokuwa mwanzo. Athari zake zimekuwa kubwa ulimwengu mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sayansi inatuambia kwamba UVIKO-19 ni janga ambalo ni la kibaguzi, linaathiri rika tofauti, linaathiri watu wenye maradhi sugu tofauti, linaathiri maskini tofauti. Kwa hiyo lazima janga hili na utaratibu wetu wote huu tulikuwa nao tuuangalie kwa utofauti wake ambaa unaathiri sehemu mbalimbali. Kwa mantiki hiyo basi, tiba ya janga la UVIKO-19 ambayo ndiyo maudhui yetu yote haya ya hizi fedha tulizopewa, lazima ziangaliwe kwa maeneo ambayo limetuathiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu kwa ujumla maneno yote yanayozungumzwa; mpango wetu na

mipango yetu yote imepangwa na imelenga kutatua mambo makuu matatu. Mambo hayo makuu matatu ambayo Mwasisi wetu wa Tanzania hii amepambana nayo na sisi tunaendelea kupambana nayo; mambo makuu matatu ni yapi? Adui ujinga, adui maradhi na adui umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ukiutazama umelenga kutatua na umepambana na maadui wawili tu; adui ujinga na adui maradhi. Ukiangalia kipaumbele katika afya, kuna *intervention* kubwa sana kwenye afya. Ukiangalia kwenye afya kuna *intervention* kubwa, lakini umaskini haujaguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umaskini kwa Tanzania ni nini? Umaskini ni kilimo. Mheshimiwa Nape amezungumza vizuri katika hilo, lakini ningependa tu kugusia kilimo katika maeneo gani. Wajumbe wengi hapa wamezungumzia killimo katika sehemu moja, lakini kilimo ukikiangalia na athari zake ni sehemu kuu tatu. Kilimo awali, sehemu ya kwanza ya kilimo ni mbolea, mbegu bora, maji ya kumwagilia na kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kuu ya kilimo ya pili ni, Waingereza wanasema *post-harvest losses*, athari inayotokea baada ya kupata mazao yao. Asilimia 40 ya hasara yetu katika kilimo inapatikana baada ya kupata mazao na sehemu kuu ya tatu ni masoko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kuhimili hili janga la umaskini, ili tupambane na adui maskini kwa kupitia njia ya kilimo tuna mambo ya msingi matatu ya kufanya. Na hayo lazima Serikali kupitia mpango huu iwekeze katika hayo makuu matatu ili kupata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka iliyopita kabla ya mapinduzi yaliyotokea ya kisera, nitayasema Zimbabwe, hakuna nchi ulimwenguni ambayo ilikuwa inafanya vizuri katika sekta ya kilimo kama Zimbabwe. Nasema ulimwenguni, kwa nini? Zimbabwe ndio nchi pekee ambayo haikuweka ruzuku katika sekta ya kilimo. Kilimo chao kilikuwa kinakwenda

kibiasara, mazao yakawa rahisi, faida ikawa kubwa. Nini wamekifanya Zimbabwe ambacho sisi tunaweza kuiga tukafika huko walikofika wao? Hilo ndilo jambo la kwanza la kutazama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa walilolifanya Zimbabwe, unajua Nchi yetu ya Tanzania kwanza imejipanga vizuri zaidi kushinda Zimbabwe, kwa sababu kuna maeneo ambayo yako juu kama Nyanda za Juu Kusini, halafu kuna mabonde yanatiririka mpaka kwenye bahari na mito mingi inakwenda mpaka kwenye bahari. Jambo kuu ambalo Zimbabwe waliweza kufanya ni kuweka mabwawa. Kwa hiyo, *focus* iwe kuweka mabwawa ili tuweze kuwa na maji ya kufanya *irrigation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisayansi imethibitishwa na hiyo ndiyo njia rahisi zaidi kuathiri sekta ya kilimo; mabwawa. Zimbabwe watu waliobahati kufika Zimbabwe, utabiri wa hali ya hewa kila siku asubuhi na jioni mtaambiwa leo kutakuwa kuna mvua, lakini bwawa hili liko asilimia 50 limejaa, bwawa lile asilimia 75 limejaa, bwawa lile kule asilimia 100. Ilikuwa sehemu ya msingi kabisa katika uhai wa Nchi ya Zimbabwe. Sisi pia tujikite kwenye mabwawa zaidi kushinda visima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, *post-harvest losses*, tatizo lake nini? Ni maghala. Tuweke maghala, tuweke *cold storage*. Kwa sababu haya yatafanya mambo mawili makuu; kwanza tutaokoa yale mazao ambayo tumeshayavuna, lakini pili, maghala ndiyo *center* ya mauzo, ita-solve tatizo la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye maghala kutakuwa kuna wataalam wa vipimo, wanasema bwana mpunga wetu huu ni wa *grade* hii, unawekwa kwenye mtandao ili mnunuzi asipate tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, hakuna tatizo la soko, tatizo la soko halipo, kila kitu kinahitajika. Tatizo lililopo ni ufkishaji sokoni. Teknolojia tunayo ambayo

inaweza kuondoa hilo tatizo kabisa. Teknolojia ipo, tunaweza kulipa kimtandao; teknolojia ipo ambayo tunaweza kununua na *ku-grade* kila kitu kimtandao. Sasa tuta-*solve* mambo makuu mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuishauri Wizara ya Fedha kutazama upya, kama wengi walivyosema, suala la kilimo, lakini maeneo makuu ambayo tunapenda yaangaliwe na yatiliwe mkazo mkubwa kabisa ni mabwawa ya maji ndani ya nchi yetu, ghalia na *cold storage investment* ndani ya nchi yetu na mtandao wa kuwezesha sisi kuuza na kuhakikisha watu wote na sekta hii inaboreshwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, umeturahisishia. Tunaposema kwamba Mpango huu ujielekeze kwenye kilimo, kwa kweli ni mambo gani ambayo tunayazungumzia, kwamba tuone maeneo ya mabwawa na umwagilaji kwa ujumla, tuone kwenye maeneo ya mbegu bora, tuone kwenye maeneo ya hifadhi ya mazao yetu, lakini pia masoko na mengine ya aina hiyo. Ahsante.

Nilitutaja Mheshimiwa Festo Sanga, utafuatiwa na Mheshimiwa Condester.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuchangia Mpango wa Maendeleo. Nitajikita kwenye mambo mawili, jambo la kwanza litakuwa sekta ya kilimo, lakini pia nitazungumzia suala la umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kwenye sekta ya kilimo ambapo hata Mjumbe aliyepita ameishia. Kwanza niipongeze Serikali kwa kazi ambayo inaendelea na kwa mpango ambao imeusoma, lakini nataka kuzungumzia kilimo kwenye mambo ya mabenki, sekta ya mabenki ndani ya Taifa letu, jinsi ambavyo yana wajibu wa kuchangia kwenye kilimo lakini tumekwama hapo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ndicho kinachoongoza kwenye pato la Taifa kwa asilimia 26.9 kama ambavyo kwenye Mpango inaoneshwa, lakini mabenki ya Taifa hili ambayo tunafanya nayo kazi na yanachangiwa sana na Serikali ni moja kati ya maeneo ambayo yamekuwa yakikwamisha kilimo kwa muda mrefu kutohana na taratibu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabenki yanapokea mitaji kutoka kwenye Serikali yetu, lakini pia kwa kipindi hiki yamepunguziwa riba ili yaweze kuhudumia wakulima wa Tanzania na Watanzania wote. Lakini nataka nitoe takwimu chache, kwa mfano wa Benki za *NMB* au *CRDB* kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2018, Benki ya *NMB* imekopesha wafanyakazi kwa asilimia 54, lakini kwenye kilimo imekopesha kwa asilimia 4.0 tu. Mwaka 2019, Benki ya *NMB* imekopesha wafanyakazi asilimia 58, lakini kwenye kilimo imekopesha asilimia 5.0 tu. Benki ya *NMB* mwaka 2020 kwa wafanyakazi imekopesha asilimia 65, kwenye kilimo imekopesha asilimia 6.0 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya *CRDB* mwaka 2019 kwa wafanyakazi imekopesha asilimia 45, kwenye kilimo imekopesha asilimia 1.0. Mwaka 2020 kwa wafanyakazi imekopesha asilimia 48, kwenye kilimo wamekopesha asilimia 2.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia benki za mataifa yanayotuzunguka kwa mfano *Cooperative Bank* ya Kenya, mwaka 2019 kwenye kilimo wamekopesha asilimia 88. Mwaka 2020 kwenye kilimo wamekopesha asilimia 91...

MWENYEKITI: Hiyo ni *Kenya Commercial Bank*?

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naam?

MWENYEKITI: KCB?

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni *KCB*. Tunakwenda *ZANACO Bank*, Zambia; mwaka 2019 Benki ya Zambia, *ZANACO*, wamekopesha asilimia 53 kwenye kilimo. Mwaka 2020 wamekopesha kwa asilimia 65 kwenye kilimo. Sisi Tanzania tunacheza na asilimia 4.0 kwa mabenki yetu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa tuna swalii la kuijuliza, Wizara ya Fedha; ni wapi ambapo tunakwama kwenye kilimo kwenye Taifa hill? Mabenki yanatukwamisha. Wanapokea mitaji ya Serikali, wamepunguziwa riba, lakini wao wameshindwa kupunguza riba kwa wakulima wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoka Mkoa wa Njombe. Mkulima akienda kukopa anakopa kwa asilimia 17, 18 hadi 20 riba. Huyu mkulima leo ni nani atakwenda kukopa? Akienda kipeleka *collateral* hata ya shamba lake wanamkatalia, wanataka kuona *collateral* ya vitu ambavyo vinaonekana ambavyo ni vikubwa ambavyo wakulima wetu wa Tanzania wengi wanashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Wizara ya Fedha, wapitie mchakato upya kuangalia jinsi gani mabenki yanatukwamisha sisi Watanzania kwenye kilimo. Hizi benki zinatumia mitaji ya Watanzania mingi na *BOT* imewaondolea riba na wao wana wajibu wa kuondoa riba kwa wakulima wetu ili waweze kupata fedha, waweze kuendeleza kilimo, tofauti na hapo tutaendelea kulia. Wenzetu wa Kenya wametuacha mbali, wanakopesha asilimia 98 kwenye kilimo, lakini sisi tumekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umezungumza suala la mbolea hapa, natoka Mkoa wa Njombe, gunia la mahindi Makete gunia la mahindi linaunzwa shilingi 15,000, mkulima anaiuliza Mheshimiwa Mbunge ninatakiwa niuze magunia saba ili kupata mfuko mmoja wa mbolea lakini leo kwenye

Mpango hatuoni makusudi yoyote ya Serikali ya kutoa dharula, yakutoa hata ruzuku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alitusaidia tulipata kwenye mahindi bilioni 50 kwa ajili ya *NFRA*. Lakini bado tuna msiba hapa kwenye mbolea kwa sababu mwakani kama hatuta waokoa wakulima leo mwakani tutaingia kwenye *crisis* ya njaa. Kwa sababu wakulima hawawezi tena kulima, mabenki hayawakopeshi, mbolea hakuna, wanalia na mbolea tunaomba ruzuku sana kwenye hii mbolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, Serikali itusikilize, itafute fedha iweke kwenye ruzuku kwa wakulima, ili wakulima wetu hawa tuwaokoe mwakani tusiingie kwenye *crisis* Tanzania na itakuwa ni aibu, Taifa ambalo tuna ardhi ya kila kona lakini leo tunaingia kwenye *crisis* ya njaa kwa kukosa ruzuku kwenye mbolea hilo lilikuwa ni la kwangu kwenye Sekta ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nije kwenye Sekta ya Nishati, ukienda kwenye Sekta ya Nishati hotuba ya Waziri ukurasa wa 14, anazungumzia usambazaji wa umeme vijijini. Kwanza tushukuru kwamba ni kweli umeme vijijini umeendelea kusambazwa naonesha kwenye ripoti mmetumia zaidi ya Bilioni 88.1 kwenye kusambaza umeme vijijini. Lakini hoja inakuja, umeme huko vijijini umewafikia Watanzania haujafikia, kwa sababu asilimia kubwa umeishia kwenye taasisi, kwenye mashule zahanati lakini ukienda kufuatilia, hapa nimefanya uchunguzi wa haraka, *TANESCO*, *TANESCO* sasa hivi hawana bajeti ya kusambaza umeme kwenye makazi ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama Serikali inanisikiliza, ifanye sensa ya kujua ni Watanzania wangapi wamesuka umeme toka 2019 hadi leo wamekwamba kuunganishiwa umeme kwa sababu *TANESCO* hawana fedha. Tumewaachia *REA* wanatupa kilomita moja moja kuelekea kwenye Makanisa, Zahanati, Vituo vy'a Afya, ukishafika huko

makazi ya watu ambao ni wapiga kura wa Taifa hili wengi hawana umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamebaki kuomba nguzo kwa Wabunge, wanaomba nguzo kwa Wabunge, wanaomba angalau hawa watoe fedha maana yake wapo tayari kutoa fedha zao wanunua lakini *TANESCO* wamekwama hawana fedha za kwenda kusambaza umeme kwa wananchi. Na nimuombe Waziri wa Nishati afanye sensa kila jimbo, kila wilaya...

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa ipo upande gani, Mheshimiwa Nape nimekuona.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahishwa na mchango wa mdogo wangu nataka tu kumuongezea taarifa kwamba, pamoja na kwamba asilimia 78 *REA* wamesambaza umeme lakini ni asilimia 18 mpaka 20 tu ya Kaya zote zimeunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika watumiaji *potential*/milioni 11.4 waliouanganishiwa umeme ni milioni 2.8 peke yake. Kwa hiyo, hali ni mbaya pamoja na kwamba tumeufikisha vijiji lakini unaingia kijijini, umeingia Kaya mbili tatu sisi tunadhani umeme umefika lakini ukweli ni kwamba namba za vijiji zinatupotosha sasa twende kwenye namba za Kaya. (Makofi)

MWENYEKITI: Unapokea hiyo taarifa Mheshimiwa Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo taarifa kwa sababu ndiyo uhalisia uliopo kwenye majimbo ye tuna kwenye mikutano na Wabunge wenzangu wananiunga mkono. Kwamba hapa tu simu ambazo tunazipokea ambazo zinahusisha wananchi wakiomba kuunganishiwa umeme ni nydingi yaani Wabunge

ndio tumegeuka *TANESCO* kwa sasa, wakati *TANESCO* wanawajibu wa kupata fedha kwa ajili ya kusamba umeme kwa Watanzania. Kwa hiyo, tusijidanganye na namba ya kwamba tumefikisha kila Kijiji lakini je mpiga kura wa Tanzania hii, mpiga kura ambaye tunamtegemea 2025 atusaidie amefikishiwa umeme? Unakuta kwamba asilimia 90 wengi hawajapata umeme na wapo tayari kuunganishiwa umeme na wapo tayari kutoa fedha zao mifukoni lakini *TANESCO* imekwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono Mpango wa Bajeti lakini natoa mapendekezo haya; waangalie mabenki kwenye kilimo, waangalie ruzuku kwenye mbolea, lakini pili *TANESCO* wasijifiche kwenye kichaka cha umeme kufika kila Kijiji waende wakaangalie uhalisia wafanye sensa kila Mbunge alete hapa ni Kaya ngani ambazo hazijaunganishwa umeme halafu wataona maajabu yaliyopo. Mimi Makete nikanza nina zaidi ya nyumba 2000 zimesukwa lakini umeme toka 2019 hadi leo hazijaungwanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ni hayo mawili tu.
Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sanga. Nilikuwa bado nakumbuka mchango wa Mheshimiwa Abdallah Mwinyi kuhusu mabwawa, ni kweli ukibahatika *ukafly / low level* Zimbabwe, siyo ile ya kwenye baada mawingu hii ya chini kidogo utashangaa jinsi utakavyoona mabwawa chini ya ardhi, mabwawa ni mengi sana tofauti na sisi ukiruka hapa hata mpaka Kigoma ukikata hivi sjui utaona hata moja. Au ukitoka hapa kuelekea Mwanza hivi, ipo haja ya kuweka msisitizo wa kipekee kabisa katika mabwawa.

Mimi pale Kongwa ukiniuliza kama tuna bwawa hata moja sjui liko wapi? Mheshimiwa Olelekaita aliye Simanjoro kule sjui wapi bwawa? Vibwawa vidogo vidogo sana vya mvua ya siku mbili tu kimekauka, Simanjiro kule bwawa, bwawa hakuna kwa hiyo, iko haja kabisa tuwe na mabwawa mengi.

Mheshimiwa Condester atafuatiwa na Mheshimiwa Thea Ntara.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, nianze kutoa mchango wangu kwanza kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa namna ambavyo ameendelea kujitoa na kwa namna ambavyo ameendelea kuhakikisha anawafikishia Watanzania huduma mahali popote pale walipo. Lakini pia niendelee kuendelea kuwaomba wale ambao Mheshimiwa Rais amewaamini kama wasaidizi wake, Baraza la Mawaziri Wasaidizi mikoani na wilaya wahakikishe angalau wanakwenda na *speed* ya mama ili wasiendelee kumwangusha ili Watanzania wapate kile ambacho mama amekusudia kiweze kuwfikia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango wangu katika maeneo matatu kama muda utakuwa rafiki, nichangie kwenye eneo la Kilimo, Nishati lakini kwenye eneo la Teknolojia namna ambavyo tukitumia teknolojia vizuri inaweza kutusaidia *ku-speed up* maendeleo lakini pia ambavyo inaweza kusaidia kutoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kwenye eneo la kilimo, nitachangia katika maeneo mawili. Suala la kwanza ni kwenye pembejeo kama ambavyo waliotangulia wamesema. Kwa kuwa sisi Tanzania siyo kisiwa, tulipopata janga la *Corona* Nchi nyiningine zilipokuwa zimeathirika *automatically* na sisi Tanzania tuliathirika hata kama sisi hatukujifungia ndani tulien��lea kufanya kazi. Nchi nydingi ambazo zinazalisha mbolea pamoja na pembejeo zingine zilipata changamoto hizo, kwa ambazo zimepata changamoto hizo imesababisha hata vitendea kazi vya kilimo huko *especially* mbolea imekuwa ni changamoto. Kwa hiyo, tuiombe sana Serikali ambayo ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali Sikivu sana. Kwa sababu tuna wiki mbili tu tayari tumeshafika kwenye msimu wa kilimo, tunaombaa Serikali itoe fedha ya dharula kwa ajili ya ruzuku ya mbolea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili tunaomba kwenye Mpango ambao utakuja baada ya kutoa mawazo yetu 2022/2023, tunaomba viwanda vyetu vya ndani ambavyo vinazalisha mbolea viwezeshwe. Viwanda hivi vikiwezeshwa vitakuja kutusaidia kwenye nyakati kama hivi, hakuna mahali panapoonesha kwenye mpango kwamba baadhi ya viwanda vyetu vitawenza kuwezeshwa ili mbolea ambayo itatoka na kuzalishwa ndani Nchi yetu iweze kuwasaidia wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jambo la pili kwenye kilimo nichangie kuhusiana na masoko na hapa naomba niende kabisa soko la *DRC Congo*. Kwa kuwa mama ameonekana kuwa ni Mwanadiplomasia mzuri na katika kipindi kifupi hiki ameonesha namna ambayo ameonesha dunia kwamba tunaweza tukashirikiana na mataifa mengine. Tumuombe sana Mheshimiwa Rais, atusaldie kukaa na Nchi ya Zambia waweze katuondolea vile vikwazo ambavyo wafanyabiashara ambao wanategemea soko la Congo wanavipitia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaka kutoa takwimu ya namna ambavyo soko la Congo linaitegemea Nchi ya Tanzania kwa ajili ya kuwasambazia chakula, unaweza kuona hata zile bilioni 50 ambazo tulipoomba Serikali tulipoleta hoja hapa waliweza kutusaidia, tusingeweza kwenda kuitumia kwa ajili ya kununua mahindi kwa Watanzania, soko la Congo peke yake lilikuwa linatosha wafanyabiashara kununua mahindi ya kutosha na kupeleka Congo au kusindika unga wa mahindi na kusambaza kule. Soko la Congo linatamani Watanzania sisi tuwa-*supply* tani za unga kuanzia laki moja na hamsini mpaka laki nne. Na inaweze hapo tunaongelea Congo Lubumbashi peke yake labda Katanga na Kolowezi lakini hapo hatuongelei Congo Kinshasa, hatuongelei Goma ni hiyo Congo Lubumbashi peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa vikwazo hivi vitaendelea, vinaendela kuwanyima nguvu wananchi ambao wanazalisha mazao ya nafaka especially wale ambao wanatokea Nyanda za Juu Kusini mikoa yote saba.

Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itafuta namna nzuri ambayo itakaa na Nchi ya Zambia waelewane vile vikwazo ambavyo wafanyabiashara wanapata na kwenye biashara nyingine viweze kuondoka ili tuweze kutumia kwa sababu mizigo mingi ambayo inatoka Tanzania inakwenda kama *transit*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kumalizia niongelee suala la teknolojia. Suala la teknolojia, teknolojia ni kama muda hauwezi kushindana na muda, wewe unapotaka kushindana na muda wewe utapitwa na wakati. Unaweza ukaona, sasa hivi hata Bunge letu vitu vingi tunaendesha kwa kutumia kishkwambi, lakini unaweza ukaona Nchi ambazo zimeendelea teknolojia hii ilipaswa itumike kwenye Bunge la Nane, Bunge la Tisa au Bunge la Kumi. Lakini tupo Bunge la Kumi na Mbili mwaka 2021 ndiyo tunatumia teknolojia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kwenye teknolojia nataka niongelee kuna kitu kinaitwa *Block Chain Technology* na kwenye *Block Chain Technology* nataka nitoe takwimu ndogo tu ikiwa kama Nchi zetu zitatamani kuendana na kasi ya teknolojia iliyopo duniani, tusiwe tunachelewa kupokea teknolojia, mambo ambayo tunapaswa kuyafanya sasa hivi tunakuja kuyafanya baada ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu turudi miaka kumi iliyopita nyuma mwaka 2010. Mwaka 2010 wakati teknolojia ya *Block Chain Technology* inakuja, ndani ya *Block Chain Technology* kuna vitu vingi, watu wa kada mbalimbali wanaweze wakatumia *Block Chain Technology* lakini hapa niongelee suala la fedha ambalo naamini kila mtanzania tunafanya kazi ili tuweze kupata fedha. Ndani ya *Block Chain Technology* kuna kitu kinaitwa *Digital Currency*, *Crypto Currency* yaani *BitCoin*. Mwaka 2010 *bitcoin* ilikuwa inauzwa chini ya dola 5, ilikuwa inauzwa 0.5 *USD* ambapo mwaka 2010 dola ya Kimarekani ukilinganisha na fedha yetu ya Tanzania ilikuwa inakwenda kwenye 1,490 – 1500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa tafsiri yake kama Serikali ingesema sisi tumeilewa hii *idea* hebu tujaribu tu tuchukue bilioni 1 tuwekeze hapa kama vile ambavyo wananaunua hisa na nimegundua inawezekana hata *IMF* hizi Benki za Dunia wanavyotukopesha wao wanawekeza kwenye vitu kama hivi halafu sisi ndiyo wanakuja kutukopesha tunabaki tunalipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ingeamua kuchukua bilioni moja ikanunua *bitcoin* ambayo ilikuwa ni Dola 0.5 ya Kimarekani ukizidisha na thamani ya dola kipindi kile unapata kama 750 maana yake bilioni 1 ukigawanya kwa hiyo fedha unakuja kupata *bitcoin* laki moja ama elfu thelathini na tano hivi. Ukizidisha na bei ya sasa ya *bitcoin*, bei ya *bitcoin* ya sasa ni dola za Kimarekani 66,000 ambapo *almost* na fedha ya Kitanzania kama Milioni mia moja na hamsini na.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tafsiri yake kama Serikali sasa hivi ingeamua kuзиza hiso *bitcoin* laki moja na thelathini na tano n.k. tungekuwa na uwezo wa kulipa hilo deni la Taifa ambalo tunadaiwa sasa hivi hiso trillioni 70 na. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bei ya *bitcoin* sasa hivi ukizidisha na kama Serikali ingenunua *bitcoin* kipindi hicho inakuja karibu trillion 90. Kwa hiyo, unaweza kuona namna gani hatuvekezi kwenye teknolojia tunapitwa, 2010 na sasa tulipo siyo muda mrefu. Unaopomuongelea Mwekezaji kama Mark Zuckerberg's ambaye ndiyo mwanzilishi wa *Facebook* na sasa hivi hi *WhatsApp* kama kuna Watanzania 10 tu wangekwenda kununua hisa kwenye kampuni yake hata wakawa na *share* mojamoja sasa hivi ndiyo *trillionaire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuangalie namna gani tunaweza tukawekeza kwenye teknolojia na ni maombi yangu na mapendeleko yangu, vijana wengi wa Kitanzania waliopo huko na nilipata nafasi kufanya *research* kwenye nchi za *West Africa* mwaka 2016/2017. Kipindi kile Nchi za

Nigeria zilikuwa zina *burn* sana mambo haya ya *cryptocurrency* lakini sasa hivi tunavyoongea muda huu hata ukiongea na Ubalozi wa Tanzania nchini Nigeria. Nigeria wamepitisha *cryptocurrency bitcoin* ni mionganini mwa fedha ambayo inatumika na wameweuka katika mfumo mzuri hata kwa kutumia *local network* za Nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata Mnigeria asiyejua kusoma ambaye hana uwezo hawesi kutumia *internet* anaweza akafanya, kwa hiyo ni kitu ambacho katika mpango huu tunaomba kuona Tanzania waisome teknolojia ya *Block Chain Technology* ili waweze kuiwekeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kwenye nishati. Kwa kweli sisi Wabunge ambaao tunatokea vijiji ni kwenye umeme, kwa kweli kauli hii ambayo Serikali inasema sana umeme mpaka kwenye vitongoji inatutesa huko vijiji ni. Sera ya Serikali inasema kwenye kila Kijiji kilometra moja ya nguzo ambazo ziweze kupita. Lakini unagundua...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. CONDESTER M. SICHWALE: Dakika moja tu.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. CONDESTER M. SICHWALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini unagundua kwamba umeme haupiti kwenye nyumba kama inavyotakikana kwa hiyo wananchi wanajulia hiyo umeme kwa kila Kitongoji imekuwaje? Na vijiji vingine ni vikubwa ina vitongoji vikubwa kwa hiyo, bado hii kauli inatupa mkanganyiko wananchi wakisikia umeme kwa kila Kitongoji lakini ukienda uhalisia kule umeme kwa kila Kitongoji hakuna.

Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iliangalie jambo hili ikiwezekana umeme kwenye kila Kijiji angalau nguzo kilometra tatu. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Kamati yetu ya Nishati ilikuwa kesho mukutane na *TANESCO* lakini kesho nafikiri tuna ratiba maalum kwa hiyo muangalie namna mtakavyofanya ikiwezekana basi kesho kutwa lakini mzibebe hizi *concerns* mtakapokutana na wenzetu wa *TANESCO* ili muweze kuelewana vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Thea Ntara kabala ya Mheshimiwa Thea, Mheshimiwa amezungumzia habari ya soko la Congo. Tunaomba Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Bashe hilo soko la Congo linalosemwa hilo tujaribu sana kuli-*capitalize* na kikwazo chetu ni Zambia, hebu Serikali iongee na Zambia, sisi kupitisha tu mzigo pale ndiyo shida yetu, pale Zambia basi. Na soko ni kubwa Congo kwa sababu Wa-Congo hawalimi, wanapiga mayenu tu hata mpira wa miguu hawajui wa-Congo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Thea Ntara au anajua mpira! Hajui si mimi nashangaa Yanga wanahangaika. Mheshimiwa Thea.

MBUNGE FULANI: Wanajua mayenu.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Niende moja kwa moja kwenye kuchangia, mimi nitakwenda kwenye kilimo. Sasa kwenye Mpango, wenzetu wamesema kwamba wataimirisha mashamba makubwa yawe kitovu cha teknolojia kwa wakulima wadogo wadogo. Najiuliza haya mashamba makubwa yapo wapi, mangapi, halafu yapo wapi? Lakini nilifikiri katika Mpango, tunaongea hapa Mheshimiwa Nape amezungumza kuhusu kilimo na wewe mwenyewe umeongea. Hivi kwa nini tusiweke kwenye mpango sasa hivi, mashamba makubwa yaanzishwe na hawa vijana tunaosema hawana ajira nilizungumza, tuna vijana wengi hawana ajira Vuyo Vikuu hebu tuanze hilo kwa nini tunaogopa? Tufanye kama *pilot* hata katika mikoa miwili au mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya kuna hayo mabailiki ya hali ya hewa, kuna *Covid*, hivi wakati mwingine nawaza

tutapata shida ya chakula na tungkuwa na mashamba haya makubwa je, si yangetusaidia. Kwa nini tusiwekeze huko tunaogopa nini? Iwe kwenye Mpango tuwasaidie hawa vijana, watafanya *production* wao wenyewe watafanya *processing* halafu baadaye mambo ya *sales*. Ni kiasi tu chakuwekeza kuwapa matrektu na pembejeo, hebu tuanze sasa kuwa hizo *commercial farms* tunazungumza lakini tunazo ngapi? Tunazo ngapi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Thea huwezi kuwa na *commercial farms* kama huna mabwawa makubwa, ili pale mvua hajanyesha wewe una *supplement* kwa kumwagilia, mvua ikinyesha mnakwenda namna hiyo.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo unavyosema.

MWENYEKITI: Nakuunga mkono lakini, endelea tu.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Eheee! Mmmh!

MWENYEKITI: Taarifa, endelea nimekuona Mheshimiwa Tabasam.

TAARIFA

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba katika hili nataka kumwambia Mheshimiwa Mpango huu upo Misri, wenzetu wa Misri kwa kutumia maji haya haya yanayotoka katika Ziwa Victoria, kule kwao wamechimba bwawa, wanafunzi wanaotoka katika Vyuo Vikuu vya Kilimo wanakopeshwa kila kitu kwenda kufanya kazi hiyo. Nafikiri Tanzania na sisi tunaweza kwenda kujifunza kule tukaleta habari hiyo Tanzania.

MWENYEKITI: Taarifa hiyo Mheshimiwa Ntara.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani naipokea sana, nafikiri wewe ni Dokta. Tufanye hivyo, nafiriki tuisubiri wakati mwingine tunasubiri tamko lakini hebu tujipange tuone kwamba kila Kanda au kila mkoa. Wakati tupo Kahama tuliwaomba Kahama kwa sababu wale wanadiriki, wanathubutu, hebu waanzishe hilo. Tutamaliza au kupunguza hizi kelele za ajira. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili niende kwenye elimu. Suala liliozungumzwa nyuma kwamba tuboreshe mitaala, mitaala yetu ya elimu haijaka vizuri, tatizo ni moja kwenye Mpango sijaona sehemu wamesema watawekeza ili hawa watu wa *TARI* waweze kuboresha. Hawana fedha kabisa hivi watakaaje chini waanze kuboresha mitaala. Serikali iangallie ile mitaala ili iboreshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeona kuna ujanzi wa Chuo VETA kikubwa Dodoma, sioni wivu lakini nilitegemea kutakuwa na mpango wa kuimarisha ile *branch* ya *SUA* iliyoko Tunduru. Hayo ni maneno tu, kule Tunduru wanasema kuna *branch* ya *SUA*, siku moja nilliongea hapa Naibu Waziri wa Elimu ananiamba tutaongozana, mambo ya kuongozana siyataki, kwa nini tuongozane? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SUA* mmesema mmeanzisha *branch* Tunduru nilitegemea hapa angesema kwamba, tunaimarisha mpango wa *SUA* na nikuambie jambo moja wakiimarisha ile *branch* pale Tunduru itapanda baadaye kinaweza kikawa Chuo chenye *program* nyingi tu. Kuna korosho kule kwa hiyo, tutakuwa na *program* ya *chemical engineering*, tutakuwa na *program* ya mambo ya *crops*, tutakuwa na *program* ya *fisheries* inatoka kule *Lake Nyasa*. Lakini ile *branch* iko pale sijui ni jina tu hakuna kinachoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mpango wahakikishe kwamba watu wa Ruvuma, watu wa Lindi na

Mtwara kunakuwa na Chuo. Tunalalamika hapa kwenye Vyuo tukisema Kusini hakuna Vyuo tunaambiwa eti hivi Vyuo vilivyopo ni vya Kitaifa. Kama vya Kitaifa basi vijengwe kwenye Mkoa mmoja vyote vije Dodoma au vyote viende Dar es Salaam. Tunaomba kuwe na Chuo mtusaidie ile *SUA* pale Tunduru inyanyuke. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho. Nimeona kuna mpango kama alivyosema mwenzangu mmoja, huu mpango wa reli kutoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay* nimeusikia toka enzi hizo nikiwa Mwalimu nafundisha nasikia mpango, enzi za *Mtwara Corridor* nilikuwa namsikia Marehemu Profesa Mbilinyi nimeusikia, nimeusikia, nimeusikia! Sasa hivi kule Ruvuma wanangoja wanasesma na sisi tutaona treni? kwanza hawaijui! Nafikiri siku itakayopita watafikiri sijui ni bomu linapita sijui ni dudu gani? Sasa huo mpango uwe kweli waanze hata kwa kitu tuone tu wanafukua fukua matuta kule angalau, lakini isiwe mpango kwenye maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Dkt. Thea kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Waziri wa Nchi nafikiri kuna hoja imetolewa hapa hii habari ya kufuatana fuatana hii ya kuongozana ongozana hii itabidi tuiwekee utaratibu hii. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge sidhani kama nilikuwa nimetaja mtu. Mheshimiwa Felista Njau, utafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie mpango huu kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliusoma mpango na nimeuona lakini mimi kwenye kipengele cha miundombinu tumekuwa na adha kubwa. Barabara zetu zinajengwa kwa

kiwango cha lami kwa pesa nydingi lakini baada ya muda mfupi barabara zinakatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishauri hapa kwenye Bunge lililopita lakini nashauri tena kuwe kuna miundombinu ya mifereji pembedni. Barabara hizi zinakatika kutokana na maji hakuna miundombinu ya mifereji. Nilikuwa ninaomba kuwe kuna miundombinu ya mifereji wakati wa kuweka hizi bajeti ili barabara zetu ziwe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele cha miundombinu kuna kipengele ambacho hakijaguswa, Kipengele hiki ni cha majitaka. Kuna adha kubwa ambayo inakuja adha hii ikoje. Kwenye Kipengele cha majitaka mtandao wake ni mdogo mno ni mdogo nilizungumzia katika Jiji la Dar es Salaam, lakini sasa tunakwenda kwenye Miji na Majiji yanayokua kwa kasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukieleza suala la maendeleo ya watu ni lazima uoanishe na miundombinu thabiti. Nikisema hivyo ninaainisha Majiji yanayokua sasa hivi mfano, mtandao wa majitaka katika Mikoa ya Mwanza ni asilimia 3.1 na Jiji lile linakua kwa kasi. Mtandao wa majitaka katika Mji wa Moshi ni asilimia 5.8 ule Mji ulivyo mkubwa unakua kwa kasi. Iringa asilimia 11, Mbeya asilimia 0.6, Songea asilimia 3.7, Tanga asilimia 9.3, Tabora asilimia 0.1, Arusha asilimia 7.0 lakini inakuja Dodoma asilimia 11 ambako ndiko Wabunge wapo, huu ni mtandao siyo wa kuwafikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza kutoa mfano wa Jiji la Dodoma, Jiji hili linakua kwa kasi ya ajabu, linakua kwa maana ya watu, majengo na viwanda vidogo vidogo. Huwezi kutenganisha maisha ya binadamu na masuala haya ya majitaka. Athari hii itakwenda mbali zaidi kama tutaendelea kulifumbia macho wakati Dodoma mtandao wa majitaka ni asilimia 10 tu ya watu wote waliounganishiwa mtandao huu. Je, kesho yetu ikoje, kwa nini tunahangaika kuagiza madawa nje kwa ajili ya malaria, kwa ajili ya magonjwa ya *typhoid*, kwa ajili ya kichocho na magonjwa mengine

yanayosababishwa na maji, kipindupindu kwa nini ni kwa sababu hatujaweka miundombinu thabiti ya majitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawiwa kusema hili kwa sababu naangalia Dodoma inavyokwenda kulipuka kila mtu anakimbilia hapa. Sasa, watu wa *DUWASA* kupitia *research* wanasema hawana bajeti ya kujenga miundombinu mipya na kukarabati ya zamani hawana hiyo bajeti. Kesho yetu iko wapi? Ni kwa nini sasa mtandao huu haupo? Haupo kwa sababu ni gharama kubwa. Mtandao wa majitaka katika hili Jiji na Majiji mengine kwa mita 10 ni shilingi 100,000 ili uunganishiwe kutoka kwenye mfumo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukioanisha unapata kilomita Moja ni Shilingi 1,000,000/= mtu kama mimi mpiga kura wa kawaida, mtu aliyeko kijijini, mtu ambaye analia na msiba wa mazao hayajauzika, wamachinga wanapiga kelele wanapata wapi Shilingi Milioni Moja ya kuunganishiwa huu mtandao? Lakini ukiangalia ni asilimia 30 tu ya watu wote walionganishiwa kwenye huu mtandao, kwa hiyo asilimia 70 tupo tuna-*hang* tu. (*Makofi*)

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Njau subiri.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa.

TAARIFA

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anayechangia kuhusu Machinga namuunga mkono sana, kweli Serikali inapaswa iwaangalie machinga maana sasa hivi wanateseka sana. Ahsante sana. (*Kicheko*)

SPIKA: Yaani Maganga bwana. (*Kicheko*)

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninapokea..

SPIKA: Unajua huyo ni Musukuma ameona tu mtoto mweupe hapa! Mheshimiwa Njau endelea. (*Kicheko*)

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninapokea taarifa hii naendelea. Ni lazima tuweze kutibu haya mambo mapema kwa sababu hiki ni kipele cha *cancer*. Tunapoendelea kufanya maendeleo tujue kwamba, huku chini kuna vitu vingine vitatakiwa vifanyike ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo naenda kwenye kipengele cha Wakandarasi. Kipengele cha Wakandarasi imekuwa kama wimbo ni mazoea naomba tutoke kwenye mazoea. Kwa sababu, hili ni janga la Kitaifa tena kubwa. Nikisema hivyo tuna ripoti ya *CAG* ya Machi inasema miradi minne tu kutokana na kucheleweshwa kwa pesa za ile miradi tozo pamoja na faini ni Shilingi Bilioni 101.98 miradi minne. Tunakwenda wapi kama Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wataalam wapo ambao wanakaa....

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Halima taarifa.

TAARIFA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mchangiaji anayechangia vizuri sana, kwamba kwenye ripoti hiyo ya Machi kwenye suala la Wakandarasi *CAG* amesema taasisi 122 za Serikali zinadaiwa jumla ya shilingi trillioni tatu na zaidi huko. Kwa hiyo, endelea

na mchango wako mzuri Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa Felista.

MHE. FELISTA D. NJAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili. Nikisema hivi hili suala huwa tunapita tu *as if* hakuna kitu kinachofanyika, lakini Taifa limedidimia kwa kupoteza pesa nyingi nashawishika kusema hapa kuna kamchezo kanachezwa kati ya mlipaji na mlipwaji. Kwa nini nashawishika, kwa nini huu ugonjwa umekuwa ni endelevu wakati mikataba ipo, kwa nini wanavunja mikataba, kwa nini Wakandarasi hawalipwi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wakandarasi hawalipwi na adha hili inatokea na kila mwaka linatokea, huu ugonjwa umekuwa ni endelevu ifike mahali huu mguu wa *cancer* ukatwe ili mtu awe salama. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Felista Njau na hasa kutukumbusha eneo la majitaka kwa sababu huwa tunalisahau kwa haraka sana. Mheshimiwa Elibariki Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kushiriki kutoa mchango wangu katika mapendekezo ya mpango, lakini pia kwa mpango ambao tunaendelea nao kuutekeleza wa mwaka 2020/2021. Mimi ninakwenda kuzungumza maeneo mawili tu kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu la Tanzania idadi ya ajira ambayo ni *active employment* katika sekta ya kilimo ni zaidi ya Watanzania inakadiriwa kwa mujibu wa ripoti ya *SAGCOT*, inakadiriwa kwamba Taifa la Tanzania watu waliojajiri katika kilimo ambao ni *adult* wanacheza kati ya watu Milioni Saba mpaka Milioni Nane na wakati mwingine ripoti zingine zinaonyesha kwamba watu walioajiriwa

katika sekta ya kilimo wanafika milioni 9.6 mpaka milioni 10. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mara nyingi sana huwa nakufuatilia unapokuwa umekaa kwenye kiti chako unapokuwa unatoa dondoo za kuchomekea kwa upande wa Serikali. Huwa najifunza mambo mengi sana na huwa nayachukulia hayo madondoo unayoyasema huwa nayachukulia *in a very serious way*. Wiki iliopita ulitoa dondoo ambayo ilikuwa inatoa msisitizo wa kuikumbusha Serikali katika suala zima la kuangalia nini Serikali inaweza ikakifanya, katika suala zima la kuwasaidia wakulima wetu kutohana na hali ilipo sasa ya masuala mazima ya mbolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme neno moja. Pamoja na kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan, imefanya vizuri sana katika mambo ya *revenue collection* kwa kweli hilo tunawapongeza sana, hatukutegemea kama *revenue collection* zingeweza kwa utulivu lakini mapato yakaongezeka katika kukusanya. Tunampongeza sana mama na Serikali yake sana sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme neno moja, nilipokuwa Mbunge kwa Mara ya Kwanza mwaka 2015 wakati ninakaa kiti cha pale nyuma mchango wangu wa Kwanza kwenye Bunge lako hili Tukufu, nilliishauri Serikali ya Chama changu kama kweli tumedhamiria kumkomboa mkulima wa Taifa hili, mkulima wa nchi hii atakombolewa peke yake kwa Taifa kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwa kujenga mabwawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda mbali nikatoa mfano nilipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Igunga, tuna Mito inaitwa Mito ya Manonga inayounganisha Mikoa ya Tabora, Simiyu na Shinyanga, nikatoa mfano kwenye Bunge hilo *Hansard* zako zikipekuliwa zitasema. Mimi ninachojuiliza hivi kwa nini wenzetu upande wa Serikalini michango ambayo inaweza mkaichukua ikawapa hata ninyi Mawaziri *legacy* kwamba, mmeweza kulisaidia Taifa katika eneo fulani kwa

nini kila mara tunakuja kama vile tu show? Tunazungumza mambo ya msingi yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hayachukuliwi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana kama tu basi fulani kesho Mheshimiwa Nape naye pia atachangia aonekane ametimiza jukumu lake la kuzungumza Bungeni, kwa nini *constructive ideas* zinazotolewa na Wabunge Serikali hawazichukui na kutekeleza? Mimi hapo napata wakati mgumu sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kujenga mabwawa nimetoa mfano kwa Wilaya ya Igunga bwawa pekeyake la Mwanzugi, lenye ujazo wa maji millilita milioni 20 lina uwezo wa kuzalisha mpunga unaozalishwa na lile bwawa moja liliojengwa toka enzi za Hayati Mwalimu Nyerere lina uwezo wa kulisha nchi karibia za Afrika Mashariki katika mchele ninaweza nikasema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wewe ulikuja kuzindua kampeni kwangu hili huwa siachi kulisema. Ulikwenda kwenye Kata za lyumbu na Mgungira sisi kule tuna mabonde, tukijenga bwawa moja tunaweza kutoa ajira ya watu wasiopungua zaidi ya 25,000 ajira za moja kwa moja, lakini mchele unaweza ukasafirishwa kwa Mataifa zaidi ya matano. Serikalini jamani kwa nini hamtaki kuweka hizi *legacy*? Mheshimiwa Nape amezungumza hapa kwa uchungu sana, mimi nasema na Bunge hili niseme wazi mbele ya Wabunge hawa, tukimaliza vikao vya Bunge kama hatujazungumza *ultimatum* ya kuwasaidia wakulima juu ya *disaster* iliyoko mtaani ya mbolea tutahukumiwa na Mungu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge hili tutamaliza kukaa vikao vyetu vyote hatujaiagiza Serikali yetu iliyoko madarakani kwenda kuwasaidia wakulima, kuhakikisha ya kwamba kuna *subsidies* zinawekwa kupunguza ukali wa bei za mbolea pamoja na mbegu tutakuwa hatujalitendea haki hili Taifa. Nataka niseme kama tunaweza kuwaangalia wamachinga tukasema wamachinga tukapeleka Shilingi Bilioni Tano sijui ngapi, hapa leo tunazungumza *voters of this*

country. Lakini mimi mwenyewe huku cha ajabu nimeshangaa nimesoma huu mpango kwa kweli lazima tukosoane ili tuweze kwenda mbele lazima tukosoane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika sekta ya Kilimo na toka juzi nilikuwa namsumbu Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe nimemsumbu sana kwenye simu, nilipoona yuko *busy* Kaka yangu alinijibu tu kwa haraka haraka nimemtafuta Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo nikamwambia hebu naomba unipe takwimu masuala mazima ya mbolea na mambo kama hayo.

Ninachowenza kusema ni kwamba kama Serikali yetu itakuwa tunakuja Bungeni hapa Wabunge tunazungumza kutoa michango ya kulisaidia hili Taifa, lakini tunaonekana kwamba tu ni mazoea tu fulani atachangia, fulani atachangia, hatutalisaidia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kujenga mabwawa kwa ajili ya kuwa na *zone* za kilimo cha umwagiliaji wakati umefika msaidieni Rais, Mheshimiwa Bashe jengeni mabwawa angalau kila Mkoa pawe na mabwawa matatu makubwa. Kwa Dodoma jengeni bwawa litakalowasaidia wakulima wa zabibu, Singida kajengeni bwawa litakalowasaidia wakulima wanaolima mpunga pamoja na alizeti, pamba kwa upande wa Kanda ya kule kwa Wajomba zangu Wasukuma, Taifa hili litakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida kubwa tuliyonayo Watanzania sisi tuna tabia moja ambayo ni nzito sana naomba niiseme kwa ruhusa yako. Sisi ni wazuri sana katika kuzungumza lakini katika kutekeleza mambo yanayoweza kuleta mapinduzi ya maisha ya Watanzania tuna kigugumizi kikubwa sana. (*Makofi*)

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Olelekaita.

TAARIFA

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nimpe ndugu yangu taarifa tu hapa, kwa mujibu wa llani yetu mfano tu, kwa sekta ya mifugo tulisema tutajenga mabwawa 400 na *change* nyingi kidogo hivi, lakini kwa mwaka huu uliopita Wizara ya Mifugo peke yake wametengewa fedha ya kujenga mabwawa matano tu na ilitakiwa mabwawa 91. Sasa tukiendelea na *trend* hiyo kwa miaka mitano ijayo maana yake ni kwamba tutajenga mabwawa kama 20 hivi kati ya 450 na hiyo ni mfano tu. Kwamba tusipobadilisha mwelekeo na mipango ikaweza kujibu llani inavyosema maana yake tutakwenda hatutafanya vizuri zaidi. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Kingu?

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naipokea kwa unyenyekevu mkubwa kwa sababu ninajua Kaka yangu pia anatoka kwenye jamii ya wafugaji. Wafugaji na wakulima ni watu wamoja, ahsante sana kwa taarifa ninaipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nataka kumalizia kusema ni kwamba, chukulia tu mfano tunaposema kilimo kina ajiri *adult* kwa mujibu wa takwimu za *SAGCOT*, watu Milioni Nane mpaka Milioni Tisa ndugu zangu tunapozungumzia ajira ya watu Milioni Nane mpaka Milioni Tisa tunazungumzia ajira ya Taifa, yaani kama kuna jambo tunatakiwa tulifanye Bunge hili ni kuilazimisha Serikali yetu kwenda sambamba na matakwa ya wakulima ambao ndiyo *voters* wetu wengi walioitulo katika Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaambia Waheshimiwa Wabunge ikiwa tutakuja kwenye Bunge hili tukasahau kuwasemea wakulima, tukasahau kuwasemea wafugaji, tukasahau kuwasemea wafanyakazi na watu wengine, hakika mimi ninakuambieni vizazi vitaandika kumbukumbu na tutakuja kuhukumiwa, kwa sababu tutakuwa tumesahau

kundi la watu ambalo ndiyo wanabeba roho ya uchumi wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, tunajenga madarasa 3,000. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kama alivyosema Mheshimiwa Nape. Mama ameonesha uwazi wa hali ya juu katika mikopo aliyopata na namna mikopo illyotumika. Kwenye hilo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini madarasa haya 3,000 kuna jambo hapa kwenye Mpango sijalion...

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ndiyo, taarifa.

TAARIFA

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, madarasa ni 15,000 siyo 3,000.

MWENYEKITI: Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa?

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Tabasam aende taratibu. Haya ninayosema ni ya shule za awali, shule shikizi na kuna madarasa mengine 12,000 kwa ajili ya sekondari. Kwa hiyo, nilikuwa natoa takwimu katika...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umeisha, *wind-up*.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapo-*windup* ni kwamba madarasa 3,000 katika shule shikizi ina maana tunakwenda ku-*recruit* wanafunzi 120,000; wapi? Tuna madarasa 12,000 ya sekondari, ina maana tunakwenda ku-*recruit* wanafunzi 480,000; wapi? Kwenye Mpango

nilitegemea Serikali ituonyeshe namna gani imejipanga kuziba *gapla* upatikanaji wa walimu na vifaa vya kufundishia kwa madarasa haya tuliyoyajenga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipofanya hivi, tutajikuta tumejenga madarasa, wanafunzi wamekwenda, na jambo la uhaba wa walimu linazaliwa. Haya ni mambo ya *planning* na namna ya kuweza kutekeleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Masache Kasaka.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa. Sisi tunatokea kwenye maeneo yanayozalisha kilimo. Katika eneo hili, kila Mbunge atawajibika kuelezea yale ambayo ni ya msingi kwa ajili ya wananchi ambaa wanategemea sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeuangalia Mpango, haujawa na suluhisho la kudumu na kutatua kero ya wakulima hapa nchini. Kilimo kinahitaji mambo ya msingi; la kwanza ni suala la umwagiliaji. Mungu alitujalia kwenye maeneo yetu, karibu kila sehemu ya nchi yetu inapata mvua za kutosha na tunapata maji mengi yanayoishia kwenda baharini bila kuwa na mfumo sahihi wa kuyavuna yale maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na maendeleo ya sekta ya kilimo kama hatujawa na mipango thabiti ya umwagiliaji. Umwagiliaji pekee ndiyo utakaofanya kilimo kiweze kukua hapa nchini. Kwenye Mpango hatujaona mipango ambayo ipo ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la ruzuku ya mbolea. Bila ya kuweka ruzuku ya mbolea

hatutawasaidia wananchi. Bei za pembejeo ni kubwa kiasi kwamba uwezo wa kumudu kununua hizo pembejeo hawatakuwa nao. Tunaishauri Serikali iangalie umuhimu sasa wa kutenga fedha kwa ajili ya kuweka ruzuku ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na wakulima binafsi, bado wana kero nyingine kubwa sana ya ukosefu wa masoko. Eneo hili lazima Serikali waongeze fedha hasa za kununua mazao ya wakulima. Tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwawezesha wananchi waweze kulifkia soko la nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wa Mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi na Kigoma ni maeneo ambayo yana eneo kubwa sana la mwambao la Ziwa Tanganyika, na wanaweza wakapata soko kupitia nchi ya *DRC Congo*. Serikali haijatafuta soko hili vizuri na kuwawezesha wananchi wakapata nafasi ya kulitumia hili soko. Tunaishukuru Serikali imejenga bandari kule eneo la Karema, bandari ya Kasanga na kule Kigoma, lakini bado tunahitaji barabara ambazo zitaunganisha maeneo haya yaliyo na bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali imejenga barabara eneo la Kasanga kutoka Sumbawanga kwenda Kasanga, lakini tuna barabara ya kutoka Mpanda Mjini kwenda eneo la Karema ambako kunajengwa bandari. Eneo hili ni muhimu sana, ni vyema ijengwe barabara ambayo itasaidia kujenga mazingira ya soko l'ililoko nchi ya *DRC Congo*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia nchi jirani ya Zambia ina vikwazo vikubwa sana kwenye maeneo ya usafirishaji. Kwa hiyo, tukitengeneza maeneo ambayo yanaweza yakawasaidia wananchi kwenye maeneo hayo, yatasaidia sana masoko kuwa mazuri na yatavutia na kuhakikisha soko la *DRC Congo* tunalishika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iangalie maeneo mengine na kuongeza fedha za *NFRA* kwa ajili ya kununua mazao ya wakulima. Eneo hili ni muhimu sana ili tuweze kuwasaidia wakulima wawe na uhakika wa masoko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nyengine ambayo tunahitaji kuishauri Serikali ni sekta ya uvuvi. Kwenye eneo la uvuvi bado Serikali haijapeleka fedha wala kuwasaidia wananchi. Tukiwasaidia wakulima, wavuvi na wafugaji, ni maeneo ambayo yanaweza yakasaidia kukua kwa uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri kwenye uvuvi hasa nzungumzie Ziwa Tanganyika. Sisi wa Ziwa Tanganyika tunapakana na nchi ya Burundi, Kongo na Zambia. Wanufaikaji wakubwa wa hili ziwa ni nchi ya Congo *DRC*, Burundi na Zambia. Sisi ambao tuna eneo kubwa la Ziwa Tanganyika, sheria tulizoziweka sisi wenyewe, siyo rafiki kwa wavuvi wa wetu. Nichukulie mfano tu kwamba mvuvi wa Tanzania haruhusiwi kuvua mazao yake mchana, lakini nchi zinazotuzunguka wao wanavua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia, karibu mazao yote ya Ziwa Tanganyika, asilimia kubwa wasafirishaji wa mazao hayo ni nchi jirani ya *DRC Congo* ndiyo wanaouza au Zambia. Kwa hiyo, naomba zile sheria ambazo zinawabana hasa wavuvi wanaokatazwa kuvuna mazao kwenye kipindi cha mchana, waruhusiwe wawe wanavua mazao hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie eneo lingine ambalo ni katika kulisaidia Shirika la Ndege la *ATCL*. Shirika hili kama Serikali hawataweka dhamira ya kulisaidia, halitasimama. Shirika hili lina madeni makubwa, linadaiwa karibu shilingi bilioni 215 ambazo ni fedha zinazodaiwa za kipindi hicho cha nyuma shirika lilipokuwa limekufa. Mzigo huu bado shirika hili linao. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukue hili deni ili tuweze kulisaidia hili shirika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utapanda ndege kutoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam, nauli ya ndege kutoka hapa kwenda Dar es Salaam ni sawa na ya kwenda Dubai, kitu ambacho ni kigumu kwa Mtanzania wa kawaida kuweza kumudu kusafiri. Naomba hili Serikali waliangalie...

MWENYEKITI: Una maana gani Mheshimiwa Mwenyekiti?

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nauli ya ndege kutoka Dodoma, ukipanda ndege ya Shirika la Ndege la ATCL kwenda Dar es Salaam, nauli yake ni kati ya shilingi 500,000 mpaka shilingi 600,000 na mpaka wakati fulani inafika shilingi 700,000. Nauli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Dubai ni shilingi 500,000 mpaka shilingi 600,000. Sasa haiwezekani kwamba shirika hili utaweza kulibeba; na linakuwa na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Naona ni kengele ya pili.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba Serikali ilisaidie shirika hili kulipunguzia madeni makubwa ambayo yapo ambayo kimsingi tukilipunguzia litawenza kumudu kibiaishara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Naomba wenzetu wa Wizara ya Uchukuzi waliangalie hili jambo. Ni *very unfair* kwa nauli za namna hiyo. *Actually*, ni wizi tu, haiwezi kuwa nauli kubwa namna hiyo hivi hivi tu. Tuangalie! Anayeumia zaidi ni Serikali kwa sababu wao ndio wanaokata tiketi nyingi kuliko mtu ye yote. Kwa nauli za namna hiyo hata bajeti haiwezi kukaa.

Mheshimiwa Agnesta Lambert, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami kwa uchache niweze kuchangia katika Mpango huu. Ili Mpango wowote wa maendeleo uweze kutekelezeka kunahitaji nguvukazi yenye afya bora. Chombo pekee kinachoshughulika na masuala mazima ya kununua na kusambaza dawa na vifaatiba ni bohari kuu ya dawa yaani *MSD*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya *PAC* ya tarehe 18 Agosti, 2021 imeweka bayana jinsi ambavyo deni la Serikali kwa *MSD* imekuwa ni changamoto kubwa sana inayopelekea *MSD* ishindwe kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi. Deni la Serikali mnamo tarehe 18 Agosti kama nilivyosema, ilikuwa imefikia shilingi billioni 269. Baada ya *PAC* kuikaripia Serikali kwamba sasa inazorotesha ufanisi wa *MSD*, mnamo mwezi Septemba Serikali ililipa shilingi bilioni 39 tu kutoka katika deni la shilingi bilioni 269. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe mnamo mwaka 2018 na 2019 deni la Serikali kwa *MSD* ilikuwa ni shilingi bilioni 53.63 na kwa kipindi kile kwa mujibu wa *CAG*, alisema *MSD* ilikuwa na hali mbaya, mbaya, mbaya sana. Sasa linganisha deni lile la shilingi bilioni 53.63 na deni la sasa la shilingi bilioni 269; unaweza kuona namna gani *MSD* wana hali mbaya. Kama *MSD* ina hali mbaya, basi Watanzania tuna hali mbaya sana. Nimesema Serikali imelipa shilingi bilioni 39 tu mpaka sasa na kufanya *balance* ya deni liwe ni shilingi bilioni 230 mpaka wakati huu ninapokuwa naongea mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua, bila ya kuwa na nguvu kazi yenye afya bora, Mipango yote tunayoipanga hapa kamwe haiwezi kutekelezeka kwa ufanisi. Tumesikia au niseme nimesikia na nimesoma taarifa ya Kamati ya Bajeti na niseme naipongeza sana Kamati hii kwa sababu imefanya kazi nzuri sana, kwa msemo wa sasa

wanasema Kamati hii imeupiga mwingi sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya Bajeti inasema, *MSD* ina hali mbaya na hivyo basi, inahitaji shilingi bilioni 363.39 ili iweze kufanya majukumu yake kwa ufanisi. Yaani hapo *MSD* wanahitaji mtaji. Kwa lugha nyingine *MSD* hivi tunavyoongea haina mtaji kabisa na tupo hapa tunapanga mipango ya maendeleo ambayo wanaokwenda kuitekeleza hawana uhakika wa afya bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya bajeti inasema, bajeti inaelekeza kwamba Serikali itenye shilingi bilioni 150 ipeleke *MSD*. Hiyo ni sehemu ndogo angalau ya bajeti halisi ya shilingi milioni 363.93. Ni wazi kabisa, kwa changamoto ya *MSD* jinsi ilivyo, hata leo hii tukisema tupeleke shilingi bilioni 150, chombo ambacho hakina mtaji kabisa, shilingi bilioni 150 haiwezi kutosha kabisa, kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mawazo yangu, shilingi bilioni 150 haiwezi kutatua changamoto zilizopo *MSD*. Ni kwa nini nasema hivi? Tumesema *MSD* inahitaji mtaji wa shilingi bilioni 363.93 lakini inaidai Serikali shilingi bilioni 269 na kwa sasa imebaki shilingi bilioni 230 kama *balance* ya deni. Kwa hiyo, leo hii ukipeleke shilingi bilioni 150 *MSD*, kwanza unawaongeza *stress* tupu, kwa sababu hazitoshi kuagiza dawa, hazitoshi kulipa madeni na mwisho wa siku sasa wanabaki wanajiuliza, hizi fedha tuzifanyie jambo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Fedha inayohusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo 2022/2023 kwa maana ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, ameeleza katika ukurasa wa 14 mpaka ukurasa wa 15, naomba nimnukuu, anasema: "Upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94."

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yetu tuijulize, ni kweli tumefikiwa kwa asilimia 94? Kama haitoshi, Mheshimiwa Waziri wa Fedha akaenda

mbali akasema, "shilingi bilioni 234 zilitolewa kwa ajili ya kununua dawa na shilingi bilioni 26.3 kwa ajili ya vifaa tiba."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo *realistic*. Nayasema haya kwa sababu kuu mbili; kwanza, *PAC* imesema, Kamati ya Bajeti imesema na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa mnamo tarehe 10/10/2021 aliongea na Waandishi wa Habari akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa *MSD* pamoja na Naibu Waziri wa Afya, akawaelekeza na akasema baada ya kutoka kwenye ziara aliyokuwa anaifanya, alikuta kule chini kwenye Mikoa, kwenye kanda kwenye Wilaya, kote kabisa hali ni mbaya. Hali ilikuwa ni mbaya kweli kweli, na Mheshimiwa Waziri aliwaelekeza na kuwapa wiki moja wawe wametekeleza jukumu la kushusha dawa. Sasa hii asilimia 94 inatokea wapi? (*Makofii/Kicheko*)

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inatokea wapi? Je, tuamini Mpango, tumwamini Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuamini *PAC* au Kamati ya Bajeti? *Where?* Wapi? Ni nani tuweze kumwamini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa... (*Makofii/Kicheko*)

MWENYEKITI: Nusu dakika.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, nafahamu hivi karibuni tumepokea mkopo wa shilingi triliioni 1.3. Ili kuondokana na aibu hii iliyopo ya *MSD* nashauri mambo makuu mawili. Kwanza itengwe shilingi bilioni 600 zipelekwe *MSD* kwa sababu ya mambo makuu mawili; mosi, ikamalize *balance* ya deni la Serikali ya shilingi bilioni 230. likisha-*clear*

hiyo shilingi bilioni 230, ina maana kwenye hiyo shilingi bilioni 600 tutakuwa tumebakia na shilingi bilioni 363.93 ambayo ndio mtaji halisi wa *MSD* wanaouhitaji waweze kufanikisha majukumu yao. (*Makof*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Agnesta. Najua muda hautoshi. Ahsante sana, muda haupo upande wako.

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba wakati nakaa, Waziri anapokuja ku-*wind up* atuondolee mkanganyiko huu wa taarifa tatu; atuambie tuuamini Mpango, tumwamini Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuiamini *PAC* au tuiamini Kamati ya Bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Agnesta Lambert kwa ufuatiliaji na takwimu. Alisema Mheshimiwa Nape hapa mwanzoni mambo ya madeni pasua kichwa. Mwenyekiti Kakoso kasema tutoe mabilioni mangapi *ATC* na wewe unatuambia tutoe mabilioni *MSD* na wale wengine mabilioni, sasa jamani sisi wenyewe Watanzania tutakula nini sasa tukifanya hivyo? (*Kicheko*)

Ahsante. Mheshimiwa Miraji Mtaturu nilikutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2022/2023, ikiwa ni maandalizi ya bajeti ijayo. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema kwa kutujalia uzima kukutana jioni ya leo. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kujenga nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi ameendelea kuunganisha nchi yetu na dunia kuhakikisha kwamba, anashirikiana na nchi nyingine katika kuunganisha nchi yetu kidiplomasia. Sisi tumekuwa tukipata faida kubwa sana ya kimaendeleo na fursa lukuki za kusukuma mbele ajenda za maendeleo ya Watanzania na ukiangalia ni juzi tu tumetoka kupata fedha ambazo zinaenda kupunguza matatizo makubwa ambayo tunayo kwenye sekta mbalimbali ikiwemo elimu, afya, maji na huduma nyingine za kijamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze moja kwa moja kwenye Mpango ambao umewasilishwa na Waziri wa Fedha. Nichukue nafasi hii kumpongeza yeye pamoja na wasaidizi wake kwa Mpango waliotuletea ambao unatupa fursa sisi kuanza kuuchambua na kutoa maoni yetu; nikianza na dhima ya Mpango wenyewe ambao unaeleza kwamba, ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipita kwenye eneo hilo wengi wetu tumeeleza hapa, asilimia zaidi ya 65 ya Watanzania wanafanya shughuli za kilimo. Wote tusipoongelea kilimo maana yake tutakuwa hatujagusa Watanzania wengi ambao tunafanya nao kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili kama ulivosema mwenyewe kwenye mpango haijaleezwa kinagaubaga, ni namna gani Serikali imejipanga kuwekeza fedha za kutosha kuhakikisha kwamba, tunabadilisha kilimo ambacho kinaajiri watu wengi. Kwenye eneo hili tusipoongea kwa kina na kujadiliana kama Taifa hatuvezi kuvuka. Eneo ambalo unapata fedha kwa maana ya unaingiza pato zaidi ya asilimia 26 huwezi kuacha bila kuwa na mpango mahususi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo, ukiangalia eneo hili ni kwamba, tunapiga kelele sasa hivi, leo tunaenda kwenye msimu wa kilimo hatuna mbolea na mbolea iko juu sana, lakini juzi tumetoka kuazimia hapa kama Bunge tukaielekeza Serikali itafute fedha za kununua mazao ya

wakulima. Kwa hiyo, kuna mambo mawili yanagongana hapo, tunahamasisha wakulima walime, lakini mwisho wa siku hakuna masoko ya kutosha ambayo yalipaswa yafanywe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, leo tunataka kwenda kwenye kilimo chenyewe pamoja na athari za UVIKO-19 Serikali ina wajibu wa kuwasaidia wakulima hawa ili tusiendelee kulalamika. Kwa hiyo, nadhani kuna mahali ambapo hatutimizi wajibu wetu kama Taifa. Naomba na nilishasema hapa kwenye Bunge lako siku za nyuma, sehemu ambayo ina wasomi wengi ukiangalia Maprofesa, Madokta na baadhi ya watu ambao wamesoma vizuri nenda ukaangalie ni sekta ya kilimo, wako pale Wizarani pamoja na maeneo mengine. Wamefanya *researches* za kutosha, wametoa ushauri wa kutosha, lakini tatizo lililopo tuna tatizo la kutenga fedha za kukisaidia kilimo cha nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongelea habari ya bajeti ya bilioni 80, wakati tunasema sisi tunataka kufikia malengo ya kuongeza kilimo cha umwagiliaji ambacho kinahitaji uwekezaji wa kutosha. Hatuko *serious* kama Taifa kama hatujaingia kwenye eneo hili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtaturu nikuhakikishie wale Maprofesa na Madokta walioko Wizara ya Kilimo hawana hata robo eka wao wenywewe. Kama wewe unayajua mashamba yao nipeleke siku moja nikaone. Ahsante, endelea kuchangia. (*Kicheko*)

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunikumbusha hilo. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, tupo kwenye *theory* zaidi, hatupo kwenye *practical*. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali, kama kweli tunasema tunataka kuwekeza, wengi wetu toka jana na juzi wamesema, tuhakikishe tunapata angalau trilioni moja iwekezwe ndani ya sekta ya kilimo ili tuweze kupata Maafisa Ugani wa kutosha, tuweze kuwa na mbolea ya uhakika, lakini zaidi tuwe na uhakika wa Maafisa Ugani ambao ni wataalam

wa kilimo kwenye vijiji vyetu. Tusipofanya hivyo, hatuwezi kuvuka na hatuwezi kukibadilisha kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea habari ya kilimo cha kutegemea mvua, leo hii wenzetu wa hali ya hewa wametuambia kwamba, tutakuwa na mvua chini ya wastani msimu unaokuja. Je, mkakati uko vipi katika eneo hili kupitia Mpango huu ambao tunaenda kuuweka? Tunayo taarifa nzuri tunaletewa na Serikali, hali ya hewa wametuambia hatutakuwa na mvua ya kutosha, sisi kama Taifa tumejiandaaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, tunasubiri baadaye tuje tuseme kulikuwa na changamoto ya mvua chache wakati tulijua kabla. Kwa hiyo, nadhani kwenye eneo la uwekezaji tumesema hapa kuhusu mabwawa, tumesema hapa namna ya kilimo cha umwagililaji, lakini tumejiandaaje kweli kuwasaidia wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda kila halmashauri hapa inaongelea habari ya upungufu wa Maafisa Ugani, ambao ni wataalam. Leo wakulima wengi wanalima kilimo cha kurithi, kilimo kilekile cha mazoea ambacho mtu anapata debe mbili, tatu kwenye eka moja, kitu ambacho anapoteza muda tu. Kwa hiyo, ombi langu kwenye eneo hili, Mpango uweze kubainisha bayana namba gani tutaweza kutoka kumsaidia mkulima ambaye yuko pale kijijini ambaye kwa hakika anaweza kuendelea kusaidia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu namna ambavyo amejitahidi kupita kila mahali anahamasisha kilimo hiki. Anahamasisha kilimo mbalimbali...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge makofi kwa Waziri Mkuu jamani. (*Makofi*)

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpigie makofi mengi Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kweli kabisa. katika eneo la kilimo amehangaika sana, kushoto, kulia na kasi. Endelea Mheshimiwa Mtaturu. (*Makof*)

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nimembatiza Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ndio Afisa Ugani Mkuu katika nchi yetu. Anafanya kazi nzuri ya kuhamasisha kilimo, pasipowezekana panawezekana kwa namna ambavyo anakaa na sisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ninao alikuja Singida amekaa na sisi siku nzima bila kutoka kwenye kit. Tukaweka mkakati wa namna ambavyo zao la alizeti litaenda kusaidia nchi hii katika mafuta ya kula.

Kwa hiyo, kwenye hili Mheshimiwa Waziri Mkuu tunampongeza na sisi kama Wabunge tuiombe Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, maeneo hayo tunakwenda vizuri. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nikupe Taarifa uende nayo Mheshimiwa Mtaturu, Singida safari hii kwenye alizeti mtakuwa wa pili baada ya Dodoma. (*Makof*)

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa sababu, wewe mwenyewe umesema ndani ya *Hansard* imeandikwa, tunaendelea tutakukumbusha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niongelee eneo la miundombinu. Ili uweze kuleta uchumi, uchumi uimarike lazima uwe na miundombinu mizuri ya kutoa mazao kwenye maeneo ya wakulima. Eneo hili nitakumbusha barabara ambazo zimetajwa miaka yote; mfano, Barabara ya Mkiwa – Itigi kwenda Makongolosi. Barabara ile ilitengewa fedha, ikasemwa tutaanza kwenye Mpango uliopita tutajenga kilometra 50, lakini juzi wamesema kilometra 20 na mpaka sasa tunavyoongea bado haijatangazwa hata kutangazwa. Hili nalo ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Barabara ya Singida – Kwamtoro kwenda Kiberashi mpaka Tanga; nayo barabara ile iitengewa kilometra 20, mpaka leo haijaanza. Tunategemea nini kama Mpango huu hauwezi kwenda kutekelezwa na kuwa na mpango.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili, Mheshimiwa Mtaturu.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba nirudie tena kusema Serikali ijipange vizuri kuleta mpango mzuri ambao utakuja kutusogezza mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nawaza tu kwamba, kama ingeweze kana iilitakiwa maofisa wale wanaowasaidia akina Mheshimiwa Bashe kule Wizara ya Kilimo, wale Wakurugenzi, nani, wasifanye kazi zaidi ya miaka 10, ili watope wakalime. Hawezi mtu anakaa pale miaka yote, anasubiri miaka 60 ya nini? *(Makofii)*

Nenda sasa wewe hizi sera zako nzuri ulizoziveka hapa Wizarani, hebu nendeni mkazitekeleze. Ingekuwepo *circle* ya namna hiyo labda pangebadilika, lakini ninyi wenzetu wengine wanakaa wanapannga tu; maana tafuta hawa Maprofesa wa kilimo nani ana hata nusu eka ya zabibu? Nani ana eka moja ya alizeti, yuko wapi? Nani ana eka mbili za mpunga pale? Hakuna. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametupa afya na uzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa hakika anafanya kazi kubwa sana ndani ya nchi yetu. Mheshimiwa Rais wetu anakidhi matarajio ya Watanzania, Watanzania ambao wana matarajio makubwa sana, lakini wanatuombea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru wale waliotengeneza Wimbo wa Taifa, kila siku asubuhi watoto wetu wakijipanga mstari pale wanasema wabariki viongozi wote, maana yake na sisi tunaombewa. Sasa utaratibu wa kubarikiwa maana yake na wewe ufanye mambo mema, usipofanya mambo mema maana yake ni kinyume chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Rais anafanya mambo mema kwa hakika na wale ambao ni wasomaji wa Biblia ukienda kwenye Mathayo 25 kuanzia mstari ule wa 40 utaona kuna jamaa pale waliambiwa: “...nilikuja kwako nikiwa na kiu hukunipa maji, nilikuja kwako nikiwa na njaa hukunipa chakula...”

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mama Samia kwa kweli haya yote sisi watu wa Hai tunasema anastahili baraka maana kama ni maji ametuletea mradi wa bilioni 3.5, lakini kama kwenye upande wa chakula ametupa, tumeppata fedha za skimu, tumeppata fedha za maji. Kwa kweli, anafanya kazi kubwa sana, nimpongeze sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Hapa kwa Waziri Mkuu niseme jambo; nilikuwa nahangaika sana masuala ya ushirika hapa, lakini kupitia yeye na Wizara ya Kilimo na Naibu Waziri leo nasema Ushirika wa Hai umeanza kufufuka. Ile mikataba ya hovyo iliyokuwepo tulienda na Naibu Waziri tukazungumza, mengine tukayavunja tukaweka utaratibu mzuri kwa vile vyama 20 ambavyo tumeanza navyo bado vingine 20. Sasa haya ni mafanikio mazuri ya kazi nzuri anayofanya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajielekeza kwenye mchango wa leo, naomba nitumie nafasi hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Serikali wanaomsaidia Mheshimiwa Rais kuanzia ngazi ya juu mpaka ya chini. Hawa watu wakati mwingine tunawasahau, wanatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee, watumishi wa afya ambao wametuvusha kwenye kipindi kigumu sana cha *corona*. Wametuhudumia vizuri, hawakuogopa, hawakurudi nyuma, naomba niwapongeze leo na ikae kwenye kumbukumbu kwamba, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri waliyoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu niipongeza pia, Kamati yetu. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana na kama Mheshimiwa Waziri atachukua maoni haya tunaenda kutoboa, tunaenda kuinua killimo chetu na tunaenda kubadilisha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niboreshe eneo moja tu na niwaombe kama wanaweza kwenda kufanya *review* ili iingie kwenye kumbukumbu, fedha zile walizosema ziongezwe milioni 450 hazitoshi. Kama kweli tunataka kubadilisha uchumi wa nchi hii kwa sababu, *formular* ya uchumi ni rahisi sana, hapa ili uchumi ukue tunatakiwa kuongeza uzalishaji, *productivity*. Sasa tunaongeza uzalishaji wapi, lazima twende kwenye killimo, hatuna ujanja mwingine. Sasa hii milioni 400 waliyopendekeza, nasema iende kwenye trillioni moja, ikishindikana bilioni 800. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe na bahati nzuri leo umekuwa ukiweka chumvi vizuri sana kwenye michango yetu. Naomba na hili tuisimamie, isipungue bilioni 800 ili kweli haya yote tunayoongea yawefe kutekelezeka fedha hii iongezwe. Kwa hiyo, niombe ile Kamati itafute namna nzuri ya kusahihisha au wewe Mwenyekiti wetu utuongozesha fedha hiyo iongezwe ili ikafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zenyewe tunazozisema, kama tunataka kilimo, lazima hatua ya kwanza tuupime

udongo wetu. Kwa sababu, wananchi wanalima, lakini wanalima kienyeji wanapata shida; tujue kuna *calcium* kiasi gani, kuna *potassium*, sijui vitu gani, udongo wetu tupime. Tukitoka hapo tuwe na maji ya hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mama Samia Suluhu ametuambia tunaletewa magari yale. Magari haya yawekwe kwenye mfumo mzuri, tuna skimu za kutosha ambazo zikijengwa tunaweza kupata maji, kwa hiyo, fedha hizi tunazozimba zielekezwe kwenye maji. Tukitoka hapo tuhamie kwenye hatua nyingine ya kuwa na mbegu sahihi, za kwetu. Hawa Maprofesa wanaosemwa ni kweli wamejaa pale Wizara ya Kilimo wa kutosha na wameandika mavitabu kibao, ukienda pale kilimo utakuta lundo la mavitabu. Tunataka yale mavitabu yatoke Wizarani yaje huku tuyaone, watusaidie, wafanye utafiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ifike mahali suala la mbegu liwe ni suala la kiusalamu wa nchi yetu. Kwa nini nasema hivyo? Ni kwa sababu mbegu hizi wanazonunua wananchi hatuna uhakika nazo. Sawa zinafanyiwa utafiti, ile *movement* ya mbegu kwenda kumfikia mlaji wa mwisho hatuna ulinzi nazo. Mtu anaweza kutengeneza mbegu *fake* hapa, hebu fikiria mtu analima shamba eka 10, lakini anaenda kupanda mbegu *fake*, kwa nini mbegu *fake*? Sawa imefanyiwa utafiti, kule mlaji wa mwisho nani anayejua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani mbegu hizi zipite kwenye mkondo wa Kamati zetu za Usalama, zilinde mbegu yetu ifike kule kwa mlaji ikiwa ile mbegu iliyokusudiwa. Ukipishakuwa na mbegu sahihi tunaendelea maeneo mengine ya kuongeza ubora wa mazao yetu. Nilitembelea nchi jirani hizi za kwetu hapa, nikakuta mazao yetu, hizi mbogamboga zinakwenda nchi Jirani, zinaongezewa thamani ya mazao na wanauzwa kwa fedha nyingi, sisi kwetu tunauza kabla ya kuongeza thamani ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana sisi pale Hai tume-*design* soko letu tofauti kidogo. Kwenye soko letu tukasema hapana, sisi tunataka kuwe na viwanda vidogo

kama mtu analeta bidhaa yake sokoni, akinunua kwa bei ya jumla kuwe na viwanda nya kufanya *sorting*, kuwe na viwanda nya kufungasha, ili bidhaa ikitoka hapa iende sokoni kwenye soko la kimataifa ikiwa imekamilika, maana yake imefungashwa vizuri. Ndio maana tunaiomba sana Serikali itusaidie fedha za kusaidia soko la Kwa Sadala ambalo litakuwa ni soko la mfano. Sisi hatujaweka sijui maeneo ya saluni, sijui maeneo ya ukumbi, tumesema hapana tunataka soko letu limsaidie mkulima na huu ndio uwekezaji mzuri ambaao nauzungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza kuhusu habari ya mbolea. Hili ifike mahali tuamue, tulisimamie kabisa kama ni kutafuta wawekezaji, kama ni Serikali kuingilia ndani. Hizi fedha ninazozionba billioni 800 au trillioni moja zifanye kazi ya kuwa na kiwanda hiki. Wameshafanya *study* ukiwaauliza watakwambia, ukienda vizuri unauliza enhee, hivi kwani kutengeneza kiwanda cha mbolea ni shilingi ngapi? Wanazo *analysis* vizuri, wameandika kwenye vitabu, lakini sasa nani afanye?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike mahali tukishindwa kupata mwekezaji Serikali ifanye kwa maslahi mapana ya kuinua uchumi wetu. Hii asilimia tunayoambiwa asilimia 65 kwamba, hawa ndio wamepata ajira. Kama asilimia 65 ndio wamepata ajira, pengo linatokea wapi kwenye pato la Taifa tunabaki na asilimia 26? Maana yake kuna watu wanatoroka hapa. Wanatoroka kwa nini, hatuwawezeshi. Tuwawezeshe warudi ili uwiano uliopo kwenye ajira uwe ndio uwiano ulioko kwenye pato la Taifa, hapo tutakuwa tumeinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze hapa wakati wa bajeti iliyopita, wakati tunajadili Mpango uliopita tuliambiwa kutakuwa na Bodi ya Uwagiliaji. Niombe Waziri atakaporudi hapa atuambie mchakato wa kuanzisha hii Bodi ya Umwagiliaji ambayo naamini itaenda kuhakikisha wakulima wetu wana vyanzo nya kutosha nya maji, Bodi hii itaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, wenzangu wamechangia sana kwenye kilimo, niombe ifike mahali

utuongoze, umesema Bunge hili linaenda kuwa la kuimarisha kilimo, kweli tukafikie hapo na tusimame imara kabisa kwa sababu huu ndio ufunguo wa kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamé kidogo niombe.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda hauko upande wako. (*Kicheko*)

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Saashisha Mafuwe. Mheshimiwa Omar Ali Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ulenge*.

MHE. OMAR ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Mpango huu. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Mpango huu. Kwa kweli utasaidia kujenga Taifa letu lenye uchumi utakaoendelea na kudumu katika nchi yetu na wananchi kupata manufaa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie katika maeneo mawili makubwa; eneo la kwanza nataka nichangie kwenye uvuvi wa bahari kuu na eneo la pili nitajikita kwenye kilimo cha mwani. Kwani katika Mpango huu Mheshimiwa Waziri amezungumza kwa kiwango kikubwa kuhusu habari ya uvuvi wa bahari kuu na ameonesha kwamba, mpango ule wa kupatiwa meli nane zile za uvuvi bado, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeuangalia kwa kina sana. Hata hivyo, bado nahisi kwamba, kutokana na mazingira ya uvuvi wa bahari kuu, basi kuna haja katika Mpango huu uelekeze zaidi kwenye hizi meli za uvuvi, basi zisiwe nane badala yake zile meli ziongezeke zaidi na zaidi zielekezwe katika maeneo ambayo yana uvuvi wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uvuvi ni sekta moja ambayo inatuwezesha kuishi maisha ya rah ana starehe katika maisha yetu ya kila siku. Hakuna mtu hata mmoja anayeishi bila ya kutegemea minofu ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unataka kujua kwamba uvuvi au samaki wana faida kubwa katika maisha ya mwanadamu, twende pale *canteen* tu ukawaangalie Waheshimiwa wanavyohangaika kushughulika na minofu ya samaki. Hii ni kuonesha kwamba uvuvi wa bahari kuu unawenza kutusaidia kutupatika pato la Taifa, lakini kujenga maisha yetu ya kila siku. Hata tunaweza tukampunguzia Waziri wa Afya wagonjwa wengi ambaao anawatibusi kwa kila siku kutokana na hali ya afya zao kutokuboreka, lakini zinaboreka kwa sababu ya minofu ya samaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia samaki hawa hawa ndio wanaowawezesha wananchi wetu wakaishi wakiwa na afya bora za kuweza kufanyakazi kwenye kilimo, kwenye viwanda na shughuli mbalimbali tunazozitegemea za maisha yetu ya kila siku. Hii ni kuonyesha kwamba sekta ya uvuvi ni sekta ambayo inahitaji kupewa kipaumbele kama vile tunavyoipa kipaumbele sekta ya kilimo kwa sababu hizi ni sekta pacha kama unataka kuleta maendeleo katika nchi basi lazima sekta ya uvuvi uiangalie kwa kiwango kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwenye sekta hii ya uvuvi lakini kwenye kilimo cha mwani, kilimo cha mwani ni kilimo ambacho kinategemewa sana katika Taifa hili kwa sababu mwani wenzetu wanasafirisha tunasafirisha mwani zaidi Zanzibar kwa matani na matani kuupeleka nje kama nchi ya Philippines, Marekani na Wachina wenzetu nchi hizi wanajikita sana kuuchukua mwani wetu kwa sababu mwani wenye ni ubora lakini ni mwani ambaao unatengeneza vitu vingi sana na vitu vyenye thamani wanatengenezea Madawa, ni chakula pia unasaidia mwani katika mambo mbalimbali katika kukuza uchumi wao mataifa ya nje zaidi ya China na Philippines. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama ikiwa tunataka tuwatoe wananchi wetu kwenye dimbwi la umaskini kwa vile nchi tumeitangaza ni nchi ya viwanda Tanzania kwa hiyo sasa tuangalie kujenga viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mwani. Kwa sababu kila tukichakata mwani basi mwani unapanda thamani zaidi kulikoni kuuza mwani ambaeo haujachakatwa. Kwa hiyo, hili tulichukue kama katika mpango wetu tuhakikishe kwamba tunajenga viwanda vidogo vidogo vitakavyoweza kuchakata mwani ambaeo sasa tutauongezea thamani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie tu mwani kama utauponda ponda ukawa kama unga basi thamani yake ni tofauti na mwani unaousafirisha ukiwa katika *ma-bundle* ambaeo haujachakatwa hii ni kuonyesha kwamba huu mwani unaweza ukatusaidia sana katika kukuza uchumi na kuwapunguzia umaskini wananchi wetu wa Tanzania kwa jumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kuzungumza kilimo cha mwani kule Zanzibar mwani ndiyo kilimo ambacho kinategemewa kwa kiwango kikubwa sana ukienda kama Kisiwa cha Pemba kuna sehemu ya Kiui Minungwini, kuna Maziwa ng'ombe, kuna maeneo ya mkoani huku Kangani maeneo mengi tu ambayo yanategemewa kwa ajili ya kuzalisha huu mwani na wananchi kupata faida. Shida ni kwamba wananchi wetu wanalima kilimo cha mwani bila ya kuangaliwa soko ambalo linaweza kuwakuzisha katika kukuza uchumi wao wa kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mazao ya baharini hayahitaji msimu wa kumwagiliwa humwagilii maji, maji ndiyo wenyewe. Kwa hiyo huhitaji kwenda kumwagilia wala huwezi kusema kwamba kuna ukame bahari haina ukame kila siku inakua kwa sababu mabadiliko ya tabia nchi kila siku kina cha bahari kinaongezeka sasa hii ni kuonyesha kwamba ikiwa tutajikita kwenye kilimo hiki cha mwani na kwa kuhakikisha wananchi wetu tunawawezesha ninaimani kwamba tutaweza kufika pahala pakubwa na uchumi wetu utaweza kukua. ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Omar Ali Omar Mbunge wa Wete ndiyo Wete, ahsante sana nilikutaja Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ulenge* na utafatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na Utukufu kwa kunijaalia kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu. Lakini kipekee kabisa nimpongeze mtekelezaji mkuu wa malengo ya nchi yetu mama yetu Samia Hassan Suluhu kwa ubunifu mkubwa anaoufanya katika kuongoza Taifa letu. Kipekee kabisa nimpongeza kwa hizi shilingi triliioni 1.3 ambazo kwa hakika miradi yote imekwenda kuwalenga wananchi wa chini moja kwa moja. Anastahili pongezi na tumuombee kwa Mwenyezi Mungu aendelee kufanya kazi zake kwa umahiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, katika kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo naomba kuishauri Serikali katika biashara ya bandari. Ametangulia kuzungumza mwenyeekiti wangu wa kamati lakini naomba na niseme yafuatayo. Serikali imeboresha miundombinu ya bandari zetu kubwa lakini kiukweli Serikali hajajipanga kukamata soko la *land locked countries*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kule Mashariki ya Kongo kuna shehena nyngi sana ambazo zinatupita Serikali sasa ianze kufanya makubaliano ya kufanya *joint operation* katika bandari ya Kalemi eneo la Kalemi au bandari ya Kalemi kuna reli ambayo inatuunganisha moja kwa moja mpaka Zambia. Kwa hiyo, tukifanya *joint operation* katika bandari ya Kalemi maana yake tunaweza kuzipata shehena zinazoingia na kutoka katika bandari ya Kongo Mashariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, suala zima la kufanya *joint operation* katika bandari za wenzetu siyo suala la ajabu tulishawahi kufanya *joint operation* katika *Port Bell* Bandari ya Uganda, na sasa hivi ninavyozungumza tayari Durban

imeshafanya makubaliano na *DRC* na Zambia na Malawi ili kuweza kupata soko lile la Mashariki ya Kongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *disadvantage* ambayo Durban wanayo hawana *direct contact* ya maji moja kwa moja na *DRC*. Lakini sisi Mwenyezi Mungu ametujaalia tunayo *direct contact* na *DRC* lakini hatujaamua kuitumia fursa ile ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niishauri Serikali au niishauri Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari waanze sasa mazungumzo na nchi ya *DRC* ili tuweze kupeleka mitambo yetu katika bandari ya Kalemie na tuweze kuli-*win* soko lile katika Mashariki ya Kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa taarifa zilizopo tayari wenzetu wa nchi Jirani wanalimendea soko lile la Kongo Mashariki tayari meli yao ya SGR inaelekezwa kule ili ku-*win* mizigo ile inayoingia na kutoka Kongo Mashariki sasa ni wakati wetu sahihi wa kuamua kufanya mazungumzo ili tuweze kuli-*win* soko lile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya matengenezo bandari ya Tanga lakini sasa ili bandari ya Tanga iweze kuleta faida na tija inayotarajiwa ni lazima mambo yafuatayo yafanyike. Kwanza reli ya Tanga mpaka Arusha ambayo imeshakarabatiwa iweze kufanya kazi. Serikali imetengeneza kilometra 470 Tanga mpaka Arusha lakini reli ile mpaka sasa haifanyi kazi sasa ili bandari ya Tanga wapate wateja wa Kilimanjaro na Arusha ambao wanakimbilia Mombasa reli ile ni lazima ifanyakazi. Serikali ijipange sasa katika mwaka unaokuja wa fedha bandari ile ya Tanga iweze kuunganishwa na soko la Arusha na la Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile reli ile ya Tanga mpaka Arusha ikiweze kusogezwa mpaka Musoma ambapo kuna bandari kule pia tutaweza kuli-*win* soko la Uganda kupitia kule Victoria. Lakini vile vile reli ile ikiweza kufika Arusha na tayari barabara ya Tanga, Handeni Kibirashi mpaka Singida imeanza kujengwa maana yake tutalivuta soko la

Rwanda kwenda Tanga ni karibu zaidi kuliko kukimbilia kwenda ... mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya *investment* kubwa vile vile Serikali ifanye *simultaneous* mambo mengine bila kuchelewesha *delayya return of that investment*. Lakini umuhimu wa barabara ya Handeni Kibirashi mpaka Singida sasa hivi pia umuhimu wake ni rahisi mno kusafirisha mitambo pamoja na vifaa vingine vya ujenzi vinavyokwenda kujenga bomba la mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali kilometa 20 ambazo zimetengwa kufanywa wakati huu ziongezwe barabara ile iweze kuisha kwa haraka kwa maslahi mapana ya Taifa hili. Naomba kuzungumzia suala zima la utekelezaji wa miradi yetu kupitia *force account* na nalisema hili kwa mapenzi makubwa kwa nchi yangu. Kuna usemi unasema kwamba *if you think education is expensive then try ignorance* na mimi nasema *if you think...*

MWENYEKITI: Hapo Mheshimiwa inabidi *u-declare interest* umo haumo?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya *na-declare the interest* kwamba na mimi ni mkandarasi mdogo mdogo lakini vile vile nazungumzia *professional liability* ambayo kwenye *force account* haipo. Lakini vile vile ninacho kiangalia ni ubora wa vinavyozaliwa kwenye *force account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba halmashauri zetu ambazo sasa *force account* ndiyo imekuwa inatekeleza kwa kiwango kikubwa hazina wahandisi na tunapokwenda kununua *material* ya ujenzi kwa kutumia zile Kamati za Manunuzi zilizoundwa hawafanyi *test* za *material* nondo hata kama unakwenda kuinunua kwenye hilo duka nondo lazima *ui-test* kabla ya kuipeleka *site*. Kuna *test* ambazo zinatakiwa kufanywa kwa nongo kama *bending test*, *tensile strength test* zinabebwa na kupelekwa *site* bila hizi *test* kwa sababu hakuna wahandisi halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tunaponunua hatu kokoto kuna *test zake* ambazo zinatakiwa zifanywe kabla ya kusema kokote hii itaenda kutumika mahala fulani sisi tunabeba tunapeleka *site* ni *liability* kubwa sisi tunaamini tuna-save lakini naomba sana tufanye tathmini ya kina katika majengo yote ambayo yamejengwa na *force account* ili tuone kweli kuna saving? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwambia hakuna *saving* kwa sababu gani Mheshimiwa *CAG* amesema kuna baadhi ya halmashauri nyingi zimeshindwa kufanya *retirement* baada ya kununua manunu hii maana yake ni nini? Serikali imeweka mwongozo wa kufanya kazi kupitia *force account*. *PPRA* wametengeneza *guidelines* lakini *guidelines* ile haitumiki ndiyo maana wameweza kununua moja kwa moja bila ya kutengeneza *framework contract* ili uweze kushindanisha bei kati ya *supplier* mmoja na mwingine lakini wewe unakwenda *direct* kwenye duka kwenye kiwanda unanunua wakati hakuna *framework contract* otherwise kusingkuwa hakuna *retirement* ya *materials*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikwambie kitu kimoja kule Dar es Salaam kuna jengo lilidondoka pale Chang'ombe tunaliita Chang'ombe *village* Mhandisi aliyesimamia lile jengo alifungwa lakini katikati ya Jiji kuna jengo lilidondoka Mhandisi aliyesimamia lile jengo alifungwa lakini katika *force account* hakuna *professional liability*...

MWENYEKITI: Nimeambiwa kumbe ya pili tayari

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba kutoa hayo kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Hii inataka mjadala siku moja kama tungepata tungejadiliana sana kuhusu *force account* tuko washabiki wa *force account* hatujapata namna ya kuteremka tu na sisi tutoe ushuhuda wetu wa jinsi ambavyo *force account* imetusaidia na jinsi ambavyo wakandarasi wangepewa hizo kazi wala tusingeenda. Maana sisi kwenye

force account tunakujengea darasa, kwa milioni 20 lina vioo *aluminum*, lina *tiles*, limepigwa *line* za umeme, na imepigwa *super* darasa 20 million na madawati yake yako ndani.

Sasa mpe mkandarasi kama utapata hiyo lakini ina siku yake hiyo wakati mwингine Mheshimiwa *Engineer* maana yake wewe mtaalam wala hatukatai huo utaalamu wenu. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud tulikutaja atafatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante awali ya yote napenda kuipongeza sana Wizara ya Fedha na Kamati yake ya bajeti kwa Mpango huu ambao sasa umetuletea na sisi tuuchakate na kuongeza mawazo yetu. Kwa dhati kabisa kwanza napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kutimiza mwaka mmoja, lakini pia napenda kumpongeza kwa hotuba yake nzuri sana aliyotoa wakati wa sherehe zile ambayo inaleta maono na mwanga mkubwa kwa maisha ya Wazanzibar na Watanzania kwa ujumla pia kuinua uchumi wa nchi na uchumi wa Zanzibar. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea natoa pongezi sana kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama Samia Suluhu Hassan kwa ukakamavu wake na ushupavu wake na uthubutu wake katika kuliongoza Taifa letu na kutuletea sisi wananchi wa Tanzania maendeleo katika kukamilisha miradi iliyoanzishwa na kuibua miradi mipyga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza kwenye sekta ya kilimo, katika kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo kwa maana ya kupata mazao bora na mazao yenye tija na kuinua uchumi wa nchi na kuongeza ajira ndani ya nchi nashauri Serikali iwekeze kwenye viwanda vya mbolea ndani ya nchi. Kama majirani zetu wanakuja kuwekeza viwanda hapa nchini malighafi za uzalishaji zinatoka hapa ndani ya nchi kwanini sisi wenyewe tusiwekeze kwanini wao waweze wana nini sisi tushindwe tuna nini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini uwezo huo tunao wa kujenga viwanda vya mbolea kwa sababu tumewekeza miradi mikubwa sana ya kimaendeleo na ya kimkakati na sasa hivi yako ukingoni kukamilika. Naamini tukiwekeza kwenye viwanda vyetu vya mbolea kwa sababu tutakuwa tunaangalia nini mahitaji ya ardhi yetu na udongo wa nchi yetu tutajua afya ya udongo wa nchi yetu kwa kutumia wataalamu wetu kwenda kupima afya ya udongo na kujua ni mbolea gani ambazo zinahitajika kwa mahitaji ya nchi zikiwemo hizo *UREA, MPK*, mbolea ya samadi tutajua tunahitaji mbolea gani kwa mahitaji ya wananchi wetu katika kuinua kilimo chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hapo hapo kilimo tuwekeze pia kwenye viwatilifu bora kwa sababu kuna hatari ya kuingiza viwatilifu ambavyo viwatilifu vile vinakwenda kuathiri mazao ya wananchi baada ya kutumia nguvu kubwa ya uwekezaji matokeo yake baada ya kuvuna wanaharibu mazao yote na hili nimelishuhudia kuna kijana mmoja alijitokeza kulima mipapai, mipapai kaimwagilia imekubali lakini ikafanya ukungu mweupe akaenda kutafuta dawa baada ya kupata dawa mipapai yote imegeuka dume hakupata hata papai moja. Sasa hapo tunaona kwamba tunahitaji viwatilifu bora ambavyo vitasaidia wakulima wetu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe sijui kama yuko hapa mipapai imegeuka dume yaani baada ya kiatilifu! Mheshimiwa Khadija endelea. (*Kicheko*)

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo hili nishalizungumza mara nydingi ambalo mimi binafsi linaniuma sana tunasema tunakwenda kusomesha wataalam wabobezi wa uzalishaji wa mbegu bora ubobezi wa mbegu unahitaji taaluma kubwa na inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa tuna wataalamu wetu wabobezi na walishafanyakazi na *research* kubwa na wakazalisha mbegu lakini wamestaafu. Matokeo yake

wazalishaji mbegu bora wale wamechukuliwa mataifa jirani wanazalisha mbegu na zinarudi Tanzania tunazinunua tena sisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali katika hili hebu tuangalie kwenye hiki kipengele cha ajira kwa hawa wataalamu wenye ujuzi maalum na adimu tunafanyaje ili waendelee kutusaidia kwa sababu kama wanaweza kuzalisha nje ya nchi mbegu inamaana tayari akili zao zinafanyakazi na hawajachoka wanaweza wakaendelea nchini kuzalisha zile mbegu na mbegu zikatapakaa kwa wananchi wetu bila ya kupata hasara ya kutumia mbegu ambazo hazina uhakika na hazina ubora. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kilimo cha kukidhi mahitaji yetu kwa maana ya sisi wenyewe lakini akiba ya chakula na kuwekeza pia kwenye uzalishaji wa nje kupata fedha za kigeni. Nashauri Serikali kilimo biashara kianzie sokoni kwa maana tutizame soko linahitaji nini na mazao ya ubora wa kiwango gani ili sasa wakulima wetu wanaotaka kujingiza kwenye kilimo biashara wajue wanalima mazao gani? Kwa ubora gani? Uhifadhi wa mazao pale ghalani na vifungashio kwa ubora gani? Ili hilo soko liweze kupatikana kwa urahisi. Kwa sababu tusilime tu bila kujua soko linahitaji nini na kwa wingi gani na kwa ubora gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea kidogo nakuja kwenye mabadiliko ya tabianchi na upande wa mazingira kwa sababu na mimi mwenyewe ni mdau wa mazingira kwa sababu na mimi nahifadhi uoto wa asili kule Tabora. Masuala ya mabadiliko ya tabianchi liwe suala la kitaifa pamoja na kutegemea fedha ambazo zitatoka kwa wafadhili, lakini tuwe na bajeti yetu wenyewe ndani ya nchi ambayo tutaitumia kwa mabadiliko ya tabianchi kipindi hicho yatakapotokea majanga na maafa mbalimbali. Kwa sababu mabadiliko ya tabianchi yatakwenda kuathiri hata hicho kilimo ambacho tunakipigania, uvuvi pamoja na uzalishaji wa mifugo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango umesema watahamasisha matumizi ya nishati mbadala na mimi

naunga mkono matumizi ya nishati mbadala hasa kwa wakaushaji wa tumbaku kule Tabora, wapatiwe nishati mbadala kukaushia tumbaku kwa sababu wanakata miti mingi na wanaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huo huo wa kuhifadhi mazingira naomba Wizara zote za Serikali ambazo zinakuwa na miradi mikubwa ya kimkakati wanaharibu sana ikolojia na mazingira mfano, anapoweka umeme kuna ukataji wa miti mingi, kwenye mawasiliano, kwenye barabara kuna uharibifu mkubwa wa ikolojia, vyanzo vyaa maji na mambo mengine.

Nashauri kila Wizara inapokuwa na miradi yake ya kimkakati naya kimaendeleo itenge fedha kwa ajili ya kurejesha uharibifu wa mazingira ambaao waliharibu kwa kukata miti na kuharibu ikolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema hapa wataongeza upandaji miti, tunashauri kwamba tusiwe tunapanda miti sasa tugeuze msamati tuwe tunaotesha miti kwa maana ukisema kupanda miti tunaipanda baadaye mingine inaachwa haikui, lakini tukiiotesha ina maana tuishughulikie mpaka ile miti ikue.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Khadija Aboud kwa kuturekebisha kiswahili kuotesha miti na siyo kupanda miti hasa Wasukuma wasikilize sana kiswahili hiki vizuri. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Cherehani Mbunge mpya wa Ushetu.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika mpango huu ambaao umeletwa kwetu na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza naanza mchango wangu kwa kuuliza swali. Je, nchi yetu sasa ipo na uchumi upi? Uchumi wa Kati au ule Uchumi wa Kimaskini tulipokuwa kule nyuma. Nasema hayo kwa sababu kwa mujibu wa Mapendekezo ya Mpango wametueleza kwamba mwaka 2019 nchi yetu uchumi ulikua kwa asilimia Saba, lakini mwaka 2020 umeporomoka mpaka asilimia 4.8 na sababu kubwa ni ugonjwa wa *Covid*, sasa *Covid* inaendelea, lakini uchumi umeporomoka sasa tupo wapi? Tunaomba Serikali itueleze ili wananchi wajue kwamba je, tunaendelea kuwa katika uchumi wa Kati au tunarudi kule? Tunaporomoka na uchumi wetu kurudi kwenye uchumi wa kimaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopanda katika uchumi wa kati ni kwamba tunakosa hata vigezo vya kukopa mikopo ya masharti nafuu. Tunakwenda kukopa mikopo ya biashara, wamesema wengi kuhusu deni, lakini mimi ningependa kujua nchi sasa itaendelea kukopa kwa vigezo vipi? Tunarudi kule tunakwenda ku-*negotiate* upya ili tuweze kukopa masharti nafuu au tunaenda na mikopo ile ambayo inaiva kwa muda mfupi na ina riba kubwa na inaweza kusababisha Watanzania kushindwa kulipa kodi au baadaye kutufanya sisi tuweke miradi yetu ambayo tumekopa kutengeneza ili iwe sasa tuiweke rehani kuweza kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua hayo ili wananchi wajue kwamba sasa hivi tupo wapi tupo kwenye uchumi wa kati kama ilivyokuwa au tumerudi kule chini kwenye uchumi wetu tuliokuwa nao wa kimaskini. Ni maswali tu hayo nataka kujua ili na watu wengine tuelewe kwamba sasa tunakwenda mwendo upi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa vijana hapa wananiambia kwamba sasa na Bibi achangie michango, mimi kweli nachangia na sasa hivi nataka niongelee wazee. Nimegundua kwamba kwenye Bunge hili wazee tupo wengi, lakini tunanyamaza kuhusu mambo yetu yanayotuhusu. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikupeleka kwenye kitabu cha mpango nimejaribu kukipitia ule ukurasa wa 127 nimejaribu kuchukua hiki kitu kidogo hapa ambacho nimeona walivyotuweka wazee katika Mpango huu. Ukurasa wa 127 wametuambia kwamba katika kile kipengele cha Ustawi wa Maendeleo ya Jamii kwamba kuimarisha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa makundi mbalimbali ya kijamii yenye uhitaji hususani wahanga wa majanga, watu wenyewe ulemavu, wazee basi niishie hapo. Sasa mimi nikajuliza hasa huu mpango unaenda sisi wazee kutusaidia kisaikolojia ili iweje, kwa sababu tumeshindwa kulipwa *pension* hatutibowi bure, sasa mmetuweka katika hali ya kutusaidia kisaikolojia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu nilichotegemea katika mpango na nilisema sana kwenye bajeti, nilitegemea mpango utuoneshe namna wanavyokwenda kutunga sheria kwa ajili ya Sera ya Wazee ya Mwaka 2003. Sera hii imepitwa na wakati. Nilitegemea kwamba mngetueleza kwamba sasa tunakwenda kutengeneza sheria ili wazee wapate *backup* katika mambo ambayo tunataka kuwafanya. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapomwambia Mzee atibiwe bure akaenda kwenye dirisha akakuta hakuna dawa anakwenda kwa nani, atalalamika wapi, kwa sheria ipi, Mheshimiwa Jenista unaniskiliza hapo, hakuna sheria na tangu mwaka 2003 hii sera mmeilalia kwa sababu gani, Wazee katika nchi yetu wametupwa katika jamii sawa kwamba watunzwe na Watoto, wapo wazee ambao watoto wao hawana uwezo wa kuwatunza. Wazee wa Kitanzania wanaishi *miserably* kabisa katika nchi yao. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Katibu hebu weka saa yako vizuri muongezee dakika mbili kwa sababu ni kweli kabisa ili Mheshimiwa Jenista amsikie vizuri, maana hapa ni kweli kabisa yaani wazee wao wameambiwa wataimarishwa na watapata msaada wa kisaikolojia katika mpango mzima huu.

Mheshimiwa Conchesta endelea. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hawa Mawaziri ni Vijana, wanafikiri sisi hatusomi hivi vitabu, umeshatuelekeza tusome na kweli tunajipinda mimi nasoma kusema ukweli, nasoma kwanza naenda kutafuta kile kipengele cha wazee wakina Conchesta sisi wanatusemea nini?

Katika ukurasa huo huo nenda kwenye kipengele cha saba wamesema kuimarisha Huduma za Ustawi wa Jamii kwa Wazee, Watoto na Watu wenyewe Mahitaji Maalum, *how*, mnakwenda kutuimarisha vipi, kwa sababu kama hakuna kitu chochote kwenye elimu huku wamesema tutafanya hiki tutafanya hiki kwetu wanasesma ni kisaikolojia na kisaikolojia mnatufanyiaje sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani nimeshangaa sana kwa sababu nchi hii imetekeleza kabisa Wazee tukubali, tunakubaliana kabisa kwamba tunapaswa jamii kutunza Wazee, lakini pale ambapo Wazee Watoto wao wamekosa kuwatunza Serikali inapaswa kuweka mkono wake. Nchi nyingine zinajenga hata majumba kwa ajili ya Wazee, Wazee wanapata matibabu, wazee hawa wanaonufaika ni wale ambao wapo katika mfumo rasmi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umetupa semina *UTT*, jana Benki Kuu tumeweza kujua lakini ni ile kada ambayo sisi tuna uwezo wa kwenda kuwekeza vipande, lakini wale waliopo huku wakulima wanateseka nchi haina mpango wowote haioneshi lolote kuonesha ni namna gani wazee wanaweza kulindwa, wanaweza kutunzwa, wanaweza kuhakikisha kwamba wanapata matibabu yao, wanaweza kuishi kwa neema katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitulinde kisaikolojia tu tunataka mtuambie, neno hili limenichanganya sana kwa sababu nikaijuliza sasa hivi wanataka kutufanyia *psychology* ya nini? Kwa hiyo kuna mipango mingine kwa kweli msiseme by the wayndio maana mnaona watu wanalamikia kilimo, kilimo kinapaswa kuwepo ili watu waweze kupata chakula na Wazee na wenyewe waweze kustawi. Lakini wapo Wazee

ambao bado wana uwezo wa kufanyakazi ukienda kwenye Halmashauri Vijana na Wanawake wamepewa mikopo na sheria ipo Wazee wapi na wapi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi nashukuru umesimama ufanuzi saikolojia hii. (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli anasoma kwenye mpango kipo kipengele cha Ustawi wa Wazee kwa kuwaimarisha kisaikolojia hatuwezi kukikwepa, hatuwezi kukikwepa wapo baadhi ya Watanzania ambao wanaangukia kwenye kipengele hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ningemuomba asome na vipengele vingine vya mpango ambavyo pia vimezungumzia ni kwa kiasi gani Serikali itakwenda kuangalia Ustawi wa Wazee.

Kwa hiyo, ninamuomba tu Mheshimiwa Mbunge nimpe taarifa kwamba hiyo ni sehemu moja, lakini zipo sehemu nyingine na hapo amesema yapo na mengine pia ambayo, tunaweza tukamsomea hapa na hayo mengine ambayo pia ni *package* ya wazee ikiwa ni pamoja na hiyo ya saikolojia kwa wale Wazee ambao wanahitaji kusaidiwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba tu nimpe taarifa Dada yangu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo Mheshimiwa Conchesta unaipokea?

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kupokea, Mheshimiwa Jenista anakumbuka kwamba tulishapendekeza kwamba hata wazee wanaweza kupata hata *pension* ya shilingi 20,000 tu katika nchi hii sasa baadaye naona alikwepa wakati ndiye

ye ye alikuwa anasimama imara kutetea hiyo sera mpaka hapo kimya hakuna chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndiyo maana Wazee Watanzania wanazidi kuzarauliwa.

MWENYEKITI: Alipokuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii ilikuwa ndiyo hoja, Mheshimiwa Jenista. (*Kicheko*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sasa baada ya kutoka huko kwenye Uenyekiti akaenda huko kwininge akaona Wazee awaweke pemberi hapana! Tuhakikishe Bunge hili likitetea wanawake, likitetea vijana.. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Sasa anasimamia kuwapatia huduma ya kisaikolojia! (*Kicheko*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, eee!

MWENYEKITI: Amekuja kivingine sasa (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba...

MWENYEKITI: Kuna taarifa uko wapi, endelea Mheshimiwa Waziri, samahani.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchangano wake Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ameuliza kama tuko kwenye uchumi wa kati na pia akaeleza kwamba uchumi wa nchi umeshuka. Sasa naomba nimpe taarifa tu, Mheshimiwa Conchesta

kwamba la kwanza kwenye mpango wa ukuaji wa uchumi huwa tunaangalia tofauti ya uchumi kati ya mwaka mmoja na mwingine kwa ukuaji siyo kwa uzalishaji ni kwa ukuaji. Kilichotokea 2019 ambacho ulisema tumekua kwa asilima 7.1 ni kwamba hiyo 7.1 unachukua uzalishaji wote wa mwaka 2019 unatoa uzalishaji wote wa mwaka 2018 halafu unagawanya kwa uzalishaji wote wa 2018 unazidisha mara 100 kwenye *market prices* ndiyo unapata ukuaji wa asilimia Saba. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa 2020 ni kwamba uzalishaji wa mwaka 2020 bado ulikuwa ni mkubwa kuliko 2019 isipokuwa tofauti ya mwaka 2020 ukitoa ile 2019 ukagawanya 2019 ukazidisha mara 100 unapata asilimia 4.2. Kwa hiyo, ukuaji upo pale pale, uchumi haujashuka na kwamba tuko kwenye uchumi wa kati kwa sababu Tanzania tarehe Mosi Julai, 2020 tulitangazwa na Benki ya Dunia kwamba tumevuka kiwango cha chini cha kipato cha mtu mmoja mmoja kwa kuchukua uzalishaji wote gawanya kwa idadi ya watu kufikia dola 1,080 kuvuka 1,038 ambayo imewekwa kidunia. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri tunakushuru taarifa yako ni ya hakika ila anachoniambia namsikia huko akisema unazidi kumchanganya kisaikolojia. (*Kicheko*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

MHE. ESTER A. BULAYA: Eeh! kwa kweli Mama endelea.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kama kuna kitu ambacho kimeharibu nchi hii ni *ma-book* hawa vijana wetu wanatuandikia *ma-book*, *ma-book* unaweka kwenye kabati ndiyo maana mpaka sasa hivi tunalia kilimo miaka yote hii. Kwa sababu ya mipango ya *ma-book*. Unaandika Misahafu hiyo *ma-book minus, plus* sasa hiyo ndiyo mmeileta, sisi tunachotaka kuambiwa ni kwamba uchumi umetoka asilimia saba

umekuja asilimia Nne na kwa sababu asilimia saba ndiyo imetufanya tuwe kwenye ... sasa nimekosea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima ueleze Watanzania kwamba hapana na hayo uyaseme katika lugha nyepesi, usituletee *one hundred minus x* uwaambie watu wakuelewe kwa sababu watu huku nimeuliza kitu ambacho wanauliza kwamba sasa tunarudi huku na je, utaweza kukopa kwa masharti nafuu hayo ndiyo utueleze kusudi tuweze kuelewa. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Kengele ya pili Mheshimiwa. (*Kicheko*)

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Kwa kweli yaani sasa hapa, Waheshimiwa tutake tuisitake kwa uchumi wa kati ambao tupo na uchumi huo mwingine tunapoelekea huo mkubwa kabisa, kwa kawaida ya *population trends* huwa ni kwamba *population* ya wazee inakuwa kubwa zaidi. Unapokuwa maskini unakuwa na *population* ya Watoto kubwa zaidi, lakini unapozidi kwenda nchi bora wazee wanazidi kuwa wengi zaidi.

Kwa hiyo, lazima katika sera zetu na mipango yetu tuanze sasa kwenda mbele tuwe tunajali hoja za Wazee. Kwa sababu hawa wanazidi kuwa wengi zaidi kuliko Watoto, kwa sababu watu wanazidi kuwa wanazaa mtotommoja, wawili. Mnavyozidi kuwa na uchumi bora zaidi watoto wanazidi kupungua. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mbunge mpya wa Ushetu Mheshimiwa Cherehani. (*Makofi*)

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa nafasi ya

pekee aliyonijalia kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, pia nimshukuru sana Rais wetu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi pamoja na Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi kwa hekima na busara ya pekee kabisa ya kuweza kupeleka jina langu mbele ya wapiga kura wa Ushetu na niwashukuru sana wapiga kura wa Ushetu kwa kutupa kura nyingi za kishindo kwa kuweza kushinda kwa asilimia 96.69. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana Kamati kwa mapendelekezo haya nilikuwa nayapitia pitia pamoja na ugeni wangu, lakini mimi ni mkulima nina-*declare interest* yangu na niwashukuru Wabunge wengi kwenye eneo la wakulima wamelijadili kwa mapana na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa dira na mwanga kwenye ushirika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikumbuka jinsi Waziri Mkuu alivyopambana kuhakikisha ushirika unasimama, ameweza kurudisha mali nyingi za ushirika, amerudisha majengo mengi ya ushirika, amerudisha *ginnery* nyingi za ushirika, lakini kwenye mpango huu sijaona suala la ushirika linaguswa. Niseme tu kwamba pamoja na Wizara ya Fedha kufanya mambo mazuri, lakini wajikite sana katika kuhakikisha vyama hivi ambavyo vimerudishiwa mali za ushirika viweze kusimama na *ginnery* zote ziweze kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mali zilizorudishwa nikisema upande *KNCU* mali zote zilirudishwa nimefanya ziara kwenye maeneo hayo nikiwa kama kiongozi wa ushirika, mali nyingi zimerejeshwa lakini zinachakaa kwa sababu zinashindwa kuendelezwa na zinatakiwa ziendelezwe hasa viwanda zipewe fedha, vifufuliwe mazao ya wakulima yanunuliwe. Nimetembelea kiwanda cha *KNCU* ni kikubwa sana lakini ukienda wakulima wanalia hali ya kahawa yao hainunuliwi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba, katika mapendelekezo haya, kwa upande wa Wizara ya Fedha waweze kupeleka fedha kwenye viwanda. Wapeleke fedha

kwenye viwanda vya SHIRECU; SHIRECU wanunue pamba; wapeleke fedha Nyanza. Kuna *ginnery* ambazo ukizikuta ni nzima, zinachohitaji ni kuwa *boosted* kidogo tu. Mfano, kuna *ginneryya* Kasamwa iko vizuri sana, inahitaji ipelekewe fedha, iingizwe kwenye Mpango iweze kufufuliwa, wananchi wa eneo la Kasamwa watauza pamba yao kwa bei nzuri kupitia ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano na niipongeze Wizara ya Kilimo mwaka 2019 na mwaka 2020 wameweza kufufua viwanda vitatu; kiwanda cha Chato, Kiwanda cha Mbongwe na Kiwanda cha KOM Illichopo Kahama. Tumeweza kuingia sokoni na Wizara ya Fedha kupitia Benki ya *TADB* ya Kilimo wamepeleka fedha. Tumeingiza ushindani na tumeweza kununua pamba kwa bei ya shilingi 1,050 hadi shilingi 1,750 kwa wakulima. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba *ginnery* ya Kasamwa, Manawa, Sola, Funze, Luguru, hizi *ginneryziangaliwe* kwa jicho la karibu sana, zifufuliwe na wanaushirika waweze kupata faida kubwa, ushindani uongezeke. Ushindani unapoongezezeka na watu wakapata bei nzuri, wakulima hawa wataenda kununua *cement*, mabati, nondo na wataendelea kuchangia mapato ya Serikali kupitia bidhaa hizo na watajenga nyumba nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa zao la Tumbaku, nataka nichangie kidogo kwa sababu nami pia ni mkulima wa Tumbaku. Mwaka 2012/2013 zao hili liliweza kuingiza fedha za kigeni zaidi ya Dola milioni 320 kwenye nchi hii; lakini wataalamu wetu hawa ambao wamesoma na wamesomeshwa na Serikali wameshindwa kulisimamia hili zao na mpaka leo limeshuka hadi kilo milioni 37. Shilingi milioni 420 *ukizi-convert* kwa leo tulikuwa tunaenda kwenye zaidi shilingi bilioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, nikwambie tu, tozo zimekuwa nyingi mpaka zimewakatisha tamaa wanunuzi wetu. Nikikumbuka hata kampuni ya *TOTC* ilikuwa inanunua kwa zaidi ya vyama 70, ambapo imeondoka

na imeacha hawa wakulima hawana mahali pa kuuzia. Sasa naionba Wizara ya Fedha, kiwanda hiki kipo Morogoro, ni kikubwa sana, kinazalisha na kusaga zaidi ya tani 120,000 kwa mwaka. Toka mwaka juzi, 2019 kimeachwa, kampuni imeshaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kiwanda kama kingeweza kufanya kazi, Serikali ikaongea na kampuni hii ikaweza kurudi, wakulima hawa wakauza tumbaku zao, soko likapanda, kiwanda kikafanya kazi, ajira zikaongezeka, nina imani hata mazao yetu ya wakulima yanaweza yakanunuliwa vizuri na bei ikaongezeka kwa wakulima wetu. Kwa hiyo, naomba kushauri kwamba tozo zipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata leo, pamoja na tozo nyininge ambazo zipo, bado upande wa wakulima tumeletewa *Withholding Tax* ya 2%. Wabunge wote wameongelea suala la pembejeo kwamba lipewe ruzuku na 2% ukiziunganisha kwenye makampuni ambazo zimekatwa, wakulima hawa wamekatwa zaidi ya dola 700 na kitu na hii ndiyo ilikuwa faida ya wakulima. Sasa leo hii bei ya mbolea imepanda. Fedha hizi ambazo wakulima walitakiwa waende kununua mbolea zimekatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikikueleza, sisi kwenye upande wa wakulima huwa gharama za uendeshaji na gharama za uzalishaji. Sasa haya makato yamekuja katikati ya msimu ambao mkulima anatakiwa achukue fedha yake, haijaingizwa kwenye gharama ya uendeshaji. Mkulima ambaye amefanya kazi miezi kumi na mbili, kilimo kinaanza mwezi wa Saba, halafu soko anakuja kuanza mwezi wa Tano msimu unaokuja; anajiandaa sasa fedha yake na yeye angalau hata shilingi 500,000 aipate kwa mwaka, imekuja kukatwa. Sasa fedha ya kununua mbolea hana na bei imepanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri maeneo haya, wakulima wetu wanateseka sana, hali ni ngumu sana. Fedha hizi zirejeshwe kwa wakulima kwa msimu huu. Hata kama ni makato sasa yanakuja, yaingizwe kwenye utaratibu

ambao hata wakulima tutaziingiza kwenye gharama za uzalishaji, tutaziingiza kwenye gharama za uendeshaji, lakini leo hii hazipo kabisa kwenye mjengeko wa bei. Tunaweza tukalalamikia ruzuku lakini matatizo mengine yanababishwa na wataalamu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Fedha wakae karibu, wapeane taarifa, watembee njia moja ili kupunguza adha kwa wakulima wetu. Tunahitaji mkulima naye afufuke, alime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna jambo alilisema na nilimpungeza sana kwamba tuna matajiri wasiopungua 5,000. Sasa hao matajiri tunahitaji pia wawemo humu.

MWENYEKITI: Mabilionea.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mabilionea 5,000. Sasa tunahitaji mabilionea hawa na wakulima wawemo; wapunguziwe tozo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi kwenye suala la pembejeo, ni kweli zimepanda kwa kiasi kikubwa sana. Sasa pembejeo imepanda, lakini bado tunaenda kuwanyang'anya na kile kidogo walichokusanya wakulima. Dola 708,000 ni zaidi ya shillingi bilioni moja ambazo zimechukuliwa kwa wakulima wetu ambao walitakiwa wanunue cash na msimu umeshaingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuitia Bunge lako Tukufu, fedha hizi ningerudia kwamba zirejeshwe kwa wakulima, kama ni tozo, basi tujipange kwa msimu ujao tuweze kuwapelekea na tuweze kuwafundisha wakulima wetu na tuwape elimu.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekititi, la mwisho, mfumo. Wakulima hawa hatujawaingiza kwenye mfumo wa usajili. Tunalalamika lakini wataalamu wetu wako kule. Wakulima wetu nchi hii wasajiliwe, waingie kwenye mfumo, tuwatambue mmoja mmoja, tujue namna ya kuwahudumia. Tukifanya hivyo hatutateseka. Bila hivyo, tutaendelea kusema kuna Bwana Shamba na Maafisa Kilimo; watambulike kwenye mfumo. Tukifanya hivyo, hata namna ya kuwafikia na kuwajua walipo na wataalamu wetu ambao watalipwa mshahara na Serikali, tutajua kwamba huyu leo amehudumia wakulima wangapi na wako maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Washeshimiwa Wabunge, makofi kwa Mheshimiwa Cherehani. (*Makof*)

Kwa sababu hiyo inaitwa ni *maiden speech in Parliament*, inaingia katika rekodi zake kama hotuba ambayo amezungumza mara kwanza akiwa Mbunge Bungeni. Kwakweli ameongea vizuri. Tunakupongeza sana Mheshimiwa Cherehani.

Kwa Waheshimiwa msiomfahamu vizuri, Mheshimiwa Cherehani ye ye mwenyewe ni mkulima sana tu. Katika vile vipindi tuliyokuwa tunajifunza jana na juzi vya masuala ya ujasiriamali, kama unataka kidogo uzoefu wa masuala ya kilimo *is a very important reference*. Amekuwa kiongozi wa ushirika mwaminifu kabisa. Taratibu zetu tulizoweka ni kwamba viongozi wa ushirika watacaa vipindi viwili tu, lakini ye ye ilibidi washirika waombe mamlaka aongezewe kipindi cha tatu kwa utumishi uliotukuka. Mmeona hata kura zake, maana walikuwa wanachagua mkulima mwenzao kwa *96 percent*. Hiyo ni *confidence* ya hali ya juu sana. Tunakupongeza sana na karibu sana. (*Makof*)

Hivi tulishakupangia Kamati? Tayari au bado?

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado.

MWENYEKITI: Bado eeh!

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Ndiyo.

MWENYEKITI: Basi Kamati ya Kilimo hiyo hiyo. (*Makofi*)

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi. Ametoka eeh! Mheshimiwa Monni Mbunge wa Chemba.

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi walau nami nichangie kidogo kwenye mwongozo huu wa Mpango. Kwanza kabisa nichukue fursa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema ambaye amekuwa akitujalia afya njema na uhai na tumekuwa tukikutana hapa mara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Nina hakika kwamba Watanzania wote sasa wana matumaini makubwa, kazi inaendela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwongozo wa Mpango huu nataka nichangie katika sehemu mbili muhimu; sehemu ya kwanza ni kilimo na pia sehemu ya pili ni barabara. Kabla sijachangia nichukue fursa hii pia kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Mwongozo wa Mpango unatupa sisi fursa ya kuwaeleza nini kiwepo kwenye Mpango unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa kwenye kilimo ni utekelezaji wa mipango ambayo ipo.

Nimejaribu kusoma Mpango wa mwaka 2019/2020 mambo mengi yameandikwa, lakini sisi wakulima kiukweli kabisa Serikali hajjawekeza vya kutosha. Maneno haya yamesemwa na kila Mbunge, lakini mimi najaribu kuangalia tu kwa takwimu. Kwa mfano, ukiangalia kwenye zana za kilimo, mpaka sasa hivi sisi tuna asilimia 20. Hizo asilimia 20 yenye we ni kwenye maandalizi tu, yaani ile hatua ya kwanza kabisa ya kuchambua ardhi ndiyo tunatumia labda matrekta na zana nyingine, lakini kwa mantiki kamili ya kutumia zana za kilimo bado tupo chini ya asilimia nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo, hakuna namna ambayo tunaweza tukaisaidia nchi hii ambayo asilimia kubwa ya Watanzania wapo kwenye sekta hii ya kilimo. Ni changamoto kubwa kweli kweli. Sasa hivi tunapoongea, ukifanya ziara kwenye maeneo yote ya Tanzania au hasa Majimboni, mbegu zenye we hazijafika. Sasa unaanza kujiuliza maswali mengi sana, kwamba kwenye Mpango tumeweka tayari, maana yake hata tukija kusema sasa tuwekeze shilingi trilioni moja, bado changamoto hii itakuwepo pale pale. Kwa maana tumeweka kwenye Mpango, tumepitisha kwenye bajeti, lakini mbegu hiyo bado mpaka sasa hivi haijafika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo nalionia, ni lazima tuhakikishe tumewekeza vya kutosha kwenye kilimo. Kama hatutafanya hivyo hakuna namna ambavyo tutakwepa watu wengi kuhamia mjini. Ukiangalia *population* kubwa ya Dar es Salaam ya vijana wengi wanaoitwa Wamachinga ni kwa sababu hakuna kazi kwenye kilimo hicho. Hatujawekeza vya kutosha kwenye kilimo. Tukiwekeza vya kutosha tutapunguza gharama hizo ambazo zimewekezwa kwa ajili ya Wamachinga; majengo yanayojengwa, fedha zile tungewekeza kwenye kilimo, vijana wale wasingekuwa na sababu ya kukimbilia mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi naiona katika mwono huo. Mimi pia nalima, lakini najaribu kuangalia mazingira ya kilimo kile, anaweza akaja kijana akalima

mwaka mmoja akaamua bora aende mjini akauze bidhaa mkononi kwa sababu ya mazingira yenyewe yalivyotengenezwa. Nataka niwaombe sana Wizara ya Fedha iangalie namna ambayo itatenga fedha za kutosha waingize kwenye kilimo. Tutaweka Mpango leo, lakini kama fedha hazitaenda huko nina hakika kabisa vijana wengi watakimbilia mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka pia niongelee kuhusu barabara. Tuna barabara yetu; halafu unaweza kujiuliza maswali mengi sana, kwamba tuna barabara ambayo inaunganisha mikoa minne. Mwenzangu Mheshimiwa Mtaturu alikuwa ameiongolea pale kwamba barabara inaunganisha mikoa minne, eti imetengewa kilometra 20 kati ya kilometra 420 na kitu. Sasa sijui wataalamu huwa wanachambua kwa kuangalia vigezo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia barabara hii, ndio barabara kubwa iliyobaki, lakini barabara hii ukiangalia faida, niliwahi kumwambia Waziri; hivi nyie mnavyoweka mipango na kujenga hizi barabara mnatumia vigezo gani? Unawezaje kuacha barabara inayounganisha mikoa minne, unaenda kujenga barabara ya kuunganisha wilaya na wilaya halafu umetenga kilometra 70?

Mimi nafikiri kama walivyoshauri Kamati ya Bajeti, wameandika maneno mazuri sana pale, kwamba tukajenge kwanza barabara zile ambazo tayari zipo kwenye mpango zimalizike *then* ndio tuingie kwenye barabara nyingine. Pengine hii itaweza kutibu lile tatizo ambalo wewe unaliona, kwamba wanakuja na Mpango, Wabunge wanasesma, lakini mwisho wa siku hakuna ambacho kinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana kwamba una barabara muhimu kuliko zote halafu hiyo ndio inatengewa fedha kidogo sana. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kama yupo hapa, Waziri wa Ujenzi wakati ujao, sisi tupo Wabunge wanane ambao tunaguswa na barabara hiyo; nataka nimwambie, ukileta tena kilometra 20 sisi hatutakuwepo tena hapa Bungeni. Kwa sababu ni

barabara ambayo ukiangalia faida zake ni kubwa zaidi.
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunaenda kupanua Bandari ya Tanga, mizigo yote ambayo inatakiwa kwenda Rwanda na Burundi, lazima ipite kwenye barabara hiyo. Ni kwa namna gani unaenda kujenga barabara nyingine huko kilometra 70, kilometra 80 ya kiwango cha lami...

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa nimekuona.

TAARIFA

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wasiofahamu, barabara inayozungumziwa hapa ni ya Handeni – Kibilashi – Kiteto – Kondoa – Singida kilometra 460. *(Makofi)*

MHE. MOHAMED L. MONNI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeipokea taarifa bila wewe kuniuliza, lakini ni ukweli, najaribu kueleza namna ambavyo barabara ile inaweza kusaidia. Najaribu kuangalia, hivi barabara zinajengwa kama unaongeaongea Bungeni au ni Serikali? Ina maana kama haitakuwa Mbunge, barabara hiyo haitajengwa? Kuna vitu vingi vinachanganya sana, kwa namna ambavyo umuhimu wa hii barabara ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana kwamba nimesoma vizuri ushauri ambao umetolewa na Kamati ya Bajeti na ninaomba wauzingatie, wasituweke kwenye mtihani wa kuja kupambana na mipango yao waliyotupangia. Nashauri kama walivyoshauri Kamati ya Bajeti kwamba barabara zile ambazo zipo kwenye Mpango, ambazo zimepangwa muda mrefu sana, zijengwe zimalizwe ndiyo mlete tena mipango mingine ya kujenga barabara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Usikate tamaa Mheshimiwa Monni, ni kuendelea kusema, ndiyo kazi yako. Barabara ya Dodoma - Kondoa – Babati ilikuwa vumbi, waliokuwepo walisema sana mpaka leo ni lami.

Kwa hiyo, ni kuendelea tu kuzungumza, kuendelea kuzungumza na vipaumbele vinabadilika na kadhalika, lakini iko siku hata hiyo barabara pia wala hatutaiongolea, Serikali itakuwa imeshaifanyia kazi.

Mheshimiwa Kwagilwa nilikuona, hebu changia sasa useme vizuri. (*Kicheko*)

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mchango wangu ni mfupi sana. Ukerasa wa 116 wa Mapendekezo yaliyosomwa, yaliyoletwa hapa na Serikali, kipengele cha 3.3.7.3 - Ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma; pana miradi pale imeorodheshwa kama 11. Sisi kwenye Taarifa ya Kamati tumeeleza jinsi ambavyo miradi hii ya *PPP* imeorodheshwa kwa miaka na miaka bila kutekelezwa na matokeo yake kwenye Mpango huu tunaotarajia kwenda kuwa nao, Serikali imeongeza mradi mwagine mmoja mpya. Mradi huu ndiyo umenisukuma nzungumzie eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu, kipengele K, unasema: "kuendeleza upembuzi yakinifu wa mradi wa kusimika boyla la kuegesha meli za mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Bandari za Tanga."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una *conflict of interest* na maslahi ya nchi, kuuweka kwenye utekelezaji wa

kutumia sekta binafsi na kwa maneno rahisi, kuandaa huu mradi kwa kumpa mtu binafsi aufanye, kwa maneno rahisi kabisa naweza kusema hii ni hujuma kwa nchi yetu na ni jambo halikubaliki. Tunipoangalia, tunakwenda kutengeneza *TICTS* nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi, mradi huu wa kutengeneza boyo la kuegesha meli za mafuta, unagusa bandari, tena bandari mbili. Bandari ni uchumi... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwagilwa tuwekee vizuri ili uende tu vizuri, yaani kwamba Serikali hapa imeweka katika orodha ya *PPP*. Kwa hiyo, ni orodha ya watu binafsi na Serikali yenye. Nawe unasema kwamba ni binafsi peke yake, labda tuwekee vizuri tu.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasema hivyo kwa sababu mradi upo kwenye upembuzi yakinifu, inamaanisha mradi haujaanza kujengwa, ina maana unaikaribisha Sekta Binafsi au mtu binafsi ashiriki kuanzia kwenye kujenga hilo boyo na kwa lugha nyingine kujenga kipande cha bandari; umkabidhi kipande cha bandari ili ajenge gati kwa ajili ya meli kubwa za mafuta na gesi kuja kushusha pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inagusa habari ya usalama wa nchi, lakini inagusa habari ya uchumi wa nchi, vile vile bandari ni lango la nchi yetu. Kumpa mtu binafsi au kumshirikisha kwenye hizi hatua za awali za kujenga, kumpa miundombinu ile ya bandari, siyo jambo sahihi sana kwa mustakabali wa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelezea jambo hili kwa sababu ukiongelea meli kubwa za mafuta unaongelea pia na meli kubwa za gesi. Sisi tunazalisha gesi. Tumetoa gesi, tumeshaichimba, tumewekeza *billions of money* kwenye gesi na kila mwaka shirika letu linaloshughulika na habari za gesi na mafuta linatumia bilioni 50 kila mwaka kwa ajili ya utafiti kwenye mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kana kwamba hiyo haitoshi, tayari tumeshakopa Benki ya *Exim*, Dola za Kimarekani bilioni 1.2 kuitoa gesi kutoka Madimba pale Mtwara, kuitoa Songosongo Lindi, kupitia Somanga Fungu, tumeifikisha Pwani na iko Dar es Salaam. Sasa gesi yetu ile ni *natural gas*. Tumeshafikisha Dar es Salaam, Serikali haina juhudu yoyote inayofanya ya kuisambaza gesi kwa wateja. Imeshafika Dar es Salaam, lakini badala yake imerukia inataka impe mtu binafsi aingize gesi nchini. Hiki kitu hakiko sawa. Hakiko sawa kwa sababu huyu mtu au hii sekta binafsi ikipewa kuwaruhusu...

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Niko tayari kupokea taarifa, iko wapi? Nimekuona sasa, endelea.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Reuben, Mbunge wa Handeni Mjini, kwamba anapoendelea kushangaa hilo ashangae pia kwamba gesi hiyo ambayo inatoka Mtwara kuja mpaka Dar es Salaam inatumika kwa asilimia 20 tu. Maana yake bado gesi yetu ya ndani haijapata soko. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kwagilwa, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii, tena naipokea kwa uzito sana, hasa ukizingatia kwamba taarifa hii imetolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe wazalendo kwenye mambo haya. Mambo haya kwa sababu yanashirikisha mikataba na *experience* inaonesha kwamba tumekuwa tukifanya vibaya sana kwenye mambo ya mikataba, hasa inayogusa rasilimali kubwa kama hii. Nashauri hapa tusiingie kwenye huu mtego. Tulishaingia huko

tukafanya mambo ya hovyo na ya ajabu ambayo hayawezi kuzungumzika, tusirudi huko. Tusirudi huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu, upembuzi yakinifu uendelee na ukikamilika ufanywe na Serikali. Kwa hiyo naishauri Serikali iondoe huu mradi kwenye hii orodha ya miradi inayopanga kuitekeleza kama *PPP*. Ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewashauri hili kwenye Kamati, tulifikiri wameelewa lakini wamekuja nalo kwenye *floor* huko na ndiyo maana na sisi tumeona tusione haya tuje tuseme hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka niliseme ni kwamba katika Mpango huu uliopita kwa maana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Bahati mbaya ni kengele ya pili Mheshimiwa Kwagilwa.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, oh, ni ya pili?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, mchango huu unatosha. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Wakati wa kuhitimisha tutawaomba Wizara ya Fedha mkumbuke kutufafanulia hili kwa sababu tumeambiwa linagusa maslahi yetu ya kiusalama pia, kwa hiyo tutapenda tujue, je, bado mnafikiri ni vizuri kuendelea na *line* hiyo au ni vizuri kuchukua ushauri ambao mlishepewa na Kamati ya Bajeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Francis Ndulane, uwe mchangiaji wetu wa mwisho jioni ya leo.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia napenda tu kutoa taarifa kwamba, leo alfajiri nilipokea taarifa ya kusikitisha ya kuondokewa na mzee wetu, aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM kati ya mwaka 2012 hadi 2017 katika Wilaya ya Kilwa. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu Mwenyekiti wetu, Yusuf Bakari Kopakopa mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa taarifa hiyo, naomba niendelee kuchangia sasa. Kwanza nalshukuru Serikali yetu ya Awamu ya Sita ikiongozwa na mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya kwa Watanzania katika kuwalettea maendeleo na kuondoa kero mbalimbali ambazo zimekuwa zikitokea kupitia miradi ya maendeleo ambayo imekuwa ikifanikishwa na Serikali yetu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, siyo kwamba namkatiza Mheshimiwa Ndulane, lakini yuko vizuri kabisa, mnamuona yuko na karatasi zake vizuri kabisa bila wasiwasi wowote ule. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ndulane, endelea bwana na tunakupa pole kwa msiba wa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu, poleni sana.

MHE. FRANCIS K. NDULANE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa kweli Serikali yetu imefanya kazi kwa ufanisi mkubwa ndani ya kipindi kifupi na kwa kweli mambo mengi yameonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu unafahamu vizuri sana ramani ya jimbo langu, kuna mambo yamefanyika, haya kwa mfano ya madarasa, kwenda shule za sekondari na shule shikizi mpaka katika maeneo ambayo yalikuwa hayatarajiwi. Hii imeleta hamasa kubwa kwa wananchi wangu kuweza kui-support Serikali yetu. Vilevile maji, madawati na huduma nyingine. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutuongoza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa nina angalizo tu; taratibu nyingi zimetolewa za ufuatiliaji na usimamizi wa miradi hii. Naomba katika kipindi hiki cha utekelezaji wa miradi sisi Wabunge wote tutakapotoka hapa Bungeni twende tukafuatilie na kuisimamia vizuri hiyo miradi ili tija iweze kupatikana. Vilevile kitengo cha ukaguzi wa ndani katika kila halmashauri kiweze kuimarishwa vizuri na kitumike kufuatilia vizuri miradi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyongeza napenda katika Mpango sasa ambao tunauendea wa 2022/2023 tuweze kuona changamoto nyingine za miundombinu, hasa hii ya elimu na afya ziweze kutekelezwa vizuri. Kwa mfano, kuna eneo la mabweni; mpaka sasa hivi kuna baadhi ya shule zetu za kata ziko mbali sana na kule wanapotoka wanafunzi. Nafikiri kwamba kunahitajika ujenzi wa mabweni ya wavulana na wasichana katika kuboresha huduma ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo katika jimbo langu ninakotoka, shule za kata ziko umbali wa kilometra mpaka 43, kilometra 15, sehemu nyingine 17 toka shule iliko. Kwa hiyo naiomba Serikali yetu katika Mpango wa 2022/2023, basi tuone namna ambavyo huduma ya mabweni, lakini pia huduma ya matundu ya vyoo, vifaa vya maabara na maabara zenyewe, iweze kuimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita katika eneo la kilimo. Tumekuwa na Benki hii ya Maendeleo ya Kilimo, kwa kweli imefanya kazi nzuri, lakini kuna changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake. Benki hii imetoa pesa nyingi, zaidi ya bilioni 100, tangu ilipoanzishwa mwaka 2014,

lakini kumekuwa na shida katika kuwafikia wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yangu ya Kilwa nina kaya zisizopungua 42,000 ambazo napenda kukuthibitishia mpaka kufikia wakati huu hakuna kaya hata moja ambayo imefikiwa na benki hii. Kwa hiyo naomba hii benki iongezewe mtaji ili iweze kuhudumia wananchi mpaka wale wa vijijini kabisa badala ya kuhudumia wananchi ambaao wako katika zile skimu maalum za kilimo kama umwagililaji na nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *alternative* ya pili kwenye hili inawezekana mtaji ukawa mdogo katika *ku-support* hii *TADB*, basi naomba vilevile ikiwezekana tuanzishe Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ambaao uta-*operate* kutokea kwenye halmashauri zetu na utashirikiana na *AMCOS* zetu, utashirikiana na *SACCOS* zetu zilizopo katika maeneo ambayo wakulima wanatoka hasa hawa wadogowadoo wa vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba upatikanaji wa pesa za mikopo za *TADB* unahusisha kujaza fomu nyngi ambazo wanavijiji wetu hawawezi kupata huo mkopo kiharaka, hasa ukizingatia kwamba Ofisi za *TADB* ziko mbali sana na maeneo ya vijijini. Hapa karibuni nilikuwa nauliza kwa mfano watu wa Singida wanapata wapi huduma za *TADB*, nikaambiwa wanapata Dodoma. Sasa yule mwananchi wa kule ndanindani kabisa Singida atafikaje Dodoma kirahisi, inakuwa ni ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kilwa tunapata huduma kutokea Mtwara. Kwa hiyo nafikiri wakiongozewa mtaji, basi wanawenza wakatusaidia, lakini vilevile tukiunda Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo ambapo mikopo itatolewa bila riba, hii itasaidia sana wakulima wetu wa vijijini kuweza kuinuka kiuchumi na kuweza kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la michezo. Msimu uliopita tulikuwa na *performance* nzuri sana

hasa kwenye mashindano ya vilabu ya kimataifa, lakini mwaka huu mambo yamekwenda ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata michezo mingine pia, tuliona Simba na Namungo ambavyo zilifanya vizuri msimu uliopita na kutuweka katika ramani ya juu kabisa Barani Afrika na duniani kwa ujumla, lakini mwaka huu haikuwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia Timu yetu ya Biashara *United* ikishindwa kusafiri kwenda kucheza mechi ya marudiano Nchini Libya. Pia hata katika michezo wa *volleyball* tumeshuhudia timu yetu ya Taifa ambayo ilitakiwa kwenda kushiriki mashindano kule Nchini Burundi ikishindwa kufika kwenye mashindano na hatimaye kufungiwa kama ambavyo Biashara *United* pia ilifungiwa.

Kwa hiyo niiombe Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara ya Michezo kwa pamoja zishirikiane katika kuona namna ambavyo tutaweza kuzilea timu zetu za Taifa pamoja na timu hizi za vilabu ambazo zinapata nafasi ya kucheza katika mashindano haya ya kimataifa ili ziweze kutuwakilisha vizuri, zisipate huo upungufu ambao ulijitokeza, hasa wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Francis Ndulane. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza shughuli zake kwa sasa.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(*Bunge lilitrudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kushukuru kwamba tunaendelea vizuri na mjadala wetu ambapo tunatakiwa tupokee, tujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha huohuo wa 2022/2023.

Nashukuru sana kwamba uchangiaji unaendelea vizuri na kesho ndiyo tunahitimisha, si ndiyo, au ni Jumatano? Ni Jumanne, si ndiyo? Kesho tunahitimisha, watakaochangia kesho watakuwa ndio wa mwisho na baadaye tutamwita mtoa hoja, asije akasahau kwamba kesho tunahitimisha.

Kwa kifupi eneo la kilimo ndilo ambalo limechangiwa sana ukiondoa Mheshimiwa Concheter aliyetusisitiza kuhusu wazee kupata huduma ya kisaikolojia, lakini eneo la kilimo ndilo limesisitizwa sana, kwamba wataalam wetu wa Wizara ya Fedha waangalie sana Sekta ya Umwagiliaji na miundombinu yake kwa maana ya mabwawa na kadhalika. (*Makofii*)

Pia imeongeleta habari ya ruzuku ya mbolea na ikiwezekana ujenzi wa kiwanda cha mbolea hii ambayo tunaagiza kutoka nje. Kwa sababu tunaagiza Saudi Arabia na wapi huko mbolea wakati na sisi tuna gesi vilevile, kwa hiyo tunaweza tukazalisha mbolea sisi wenyewe.

Ukosefu wa masoko umeongeleta kwa mazao ya kilimo; fedha za *NFRA* kwamba ziongezwe ili kusaidia katika ununuzi wa baadhi ya mazao na hasa nafaka. Sekta ya Uvuu nayo ni sehemu ya sekta ya kilimo na umuhimu wake. Sekta ya mifugo ni sehemu ya sekta ya kilimo.

Imesitisizwa habari ya kupima udongo wetu, imesitisizwa habari ya kuwa na mbegu zetu wenyewe na kufanya tafiti. Mtagundua kwamba mbegu zimezidi kupotea, mbegu zilizokuwepo miaka ya sabini, sitini huko kurudi nyuma zinapotea, hata kama ni za mahindi huwezi kupata zile. Hata mbegu za maboga zinapotea, hata matango yaliyokuwa

ya asili leo huwezi kupata tango lile, leo tuna matango haya ya kisasa ya kutoka maabara. Mbegu nydingi sana za mtama, za nini, siyo zile, zinazidi kupotea. Wanazichukua huko na huku zinazidi kupotea, tunaletewa mbegu ambazo wametengeneza akina Monsanto na wenzao, tunaingia kwenye tatizo kubwa sana la kutegemea mbegu za watu wengine. Hakuna mtu maskini kama mtu ambaye hana mbegu, yaani ukishakosa mbegu wewe maskini sana. Kwa hiyo kwenye eneo la mbegu lazima tujipange vizuri na mpango wetu basi uangalie maeneo hayo.

Eneo la kuongeza ubora wa mazao yetu ya kilimo limeongelewa. Limeongelewa eneo la viuatilifu na umuhimu wake, Mheshimiwa Khadija ametutolea mfano hapa, mapapai yalipuliziwa viuatilifu yakabadilika yakawa madume matupu au unakuta viwavi jeshi ukipuliza kiuatilifu ndiyo kwanza vinanenepa yaani, vinazidi kushambulia mahindhi yakiwa madogomadogo. Viuatilifu ni shida kubwa na ni bei kubwa. Halafu mkulima akinunua akienda aki-*apply* wala hapati matokeo aliyyotarajia na ameshaingia gharama. Tumeona jinsi ambavyo kilimo ni gharama.

Tumekumbushwa kuhusu zana za kilimo; matrekta na zana nydinge zote zinazohitajika. Hatuwezi kuwategemea vijana wetu wakaenda katika kilimo halafu walime kwa jembe la mkono. Yaani kijana awe na vidato vyake halafu akashike jembe la mkono, kazi hiyo hawatafanya. Kwa hiyo tunapowavutia vijana kuingia katika kilimo maana yake lazima zana za kilimo zitumike zaidi. Kwa maana hiyo wanaweza wakavutiwa zaidi.

Tumekumbushwa vile vile na Mheshimiwa Cherehani kuhusu ile asilimia mbili ya *withholding tax* kwenye mazao ya kilimo, ilipita tu *very unfortunately*. Kwenye mpango wa mwaka unaokuja huku kuwe na mpango wa kuondoa hiyo *withholding tax*, maana Bunge Iijalo la Bajeti hiyo hatutaelewana kabisa hiyo. Kwa hiyo Wizara ya Fedha muanze kuona nini cha kufanya. Sababu zake Mheshimiwa Cherehani amezieleza na sisi tulishaligusia huko nyuma.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kumalizia kabisa, unajua tunapanga bajeti ya trillioni 30 *plus*, lakini tuijulize hivi kwa nini trillioni 1.3 ya mama Samia imechangamsha nchi, yaani nchi imechangamka. Kila mahali pamechangamka na trillioni 1.3, lakini sisi huwa tunapanga 30 hapa. Maana yake ni kwamba, hebu Wizara ya Fedha tuongozeni vizuri, kuna mahali hatukai sawasawa inavyoelekea. Maana tunajuliza yaani tunafurahia hii 1.3, Mheshimiwa Ummmy, yaani huko mambo yetu mazuri. (*Kicheko*)

Hapa ndiyo maana tunampongeza sana Rais wetu, kwanza kwa uwazi wa hizi fedha, zilivyofika, Waheshimiwa Mawaziri mlivyokaa na kuzigawanya, hamjawa na hiyana wala nini, mmejtahidi kabisa, mmegusa kila mahali. Ni jambo jema sana. Basi ni vizuri na hii bajeti yetu inayokuja mwakani hebu sasa hizi zetu wenyewe tujitahidi, sijui tufanyeje, sijui tutenge 1.3 pembeni, hii Waziri wa Fedha asilingille kuigawa, aitenge pembeni, halafu baadaye sasa mnakaa Serikali mnaimwaga kama ilivyomwagika hii ya IMF na mama. Sijui lakini ni *food for thought*, kwamba fedha hii kwa kweli inachangamsha uchumi, inagusa maeneo mengi sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa *Engineer* Ulenge hata alipokuwa anazungumza habari ya Wakandarasi ambayo ni muhimu na ya maana sana, wala simpingi, lakini sisi tunachofurahia *force account* ni kwamba mafundi wetu ndanindani kule vijijini, yaani sasa hivi wako na shughuli wanapata pesa. Kwa hiyo mzunguko wa fedha ya hii 1.3 unakwenda moja kwa moja kwa wananchi wanaoshughulika na haya mambo ya ujenzi kule chini, jambo ambalo ni zuri sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno haya, basi niwakumbushe Kamati ya Uongozi tuna kikao kifupi hapa *lounge* kwangu hapa, nawaomba tukutane hapa kwa jambo la dharura kidogo. Niwakumbushe wale wengine kesho saa tatu kama ilivyo ada, halafu saa nane kamili tunaendelea na Bunge kama kawaida.

Sasa kwa vile shughuli za leo zimekamilika na muda wetu uko palepale kwa uendeshaji wa kisayansi kabisa, nitumie nafasi hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana. (*Makofii/Kicheko*)

*(Saa 1.00 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 9 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana)*